# Nipashe

Jumatano Oktoba 9, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580044

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US




## JPM awaamuru DC, Polisi kumlipa mil. 15/- mama aliyeibiwa ng'ombe

UKURASA 2


Fungamano dhidi ya Iran lafifia Ukurasa 20

Jasusi wa Marekani aliyevujisha siri ya nyuklia kwa Urusi Ukurasa 18

siasa

JUMATANO OKTOBA 9, 2019 Nipashe HABARI BORA NA KAMILIFU

Magufuli na harakati za ukombozi wa pili Ukurasa 14

AJENDA YA MWANAMKE TURUFU YA USHINDI UCHAGUZI 2019/20120

Na Grace Mwakalinga, MBEYA

USHIRIKI wa Wanawake katika nafasi mbalimbali za maamuzi hususani kisiasa bado ni mdogo, hali ambayo inakinzana na azma ya kujenga jamii isiyokuwa na ubaguzi kama ilivyobainishwa kwenye dira ya Taifa 2025.

Dira hiyo imehimiza usawa kwenye mgawanyo wa madaraka. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977 pamoja na sheria mbalimbali za nchi.

Taasisi ya Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) kwa kushirikiana na Asasi mbalimbali za kupigania haki za wanawake nchini ikiwamo Mtandao wa Wanawake na Katiba, Women Fund Tanzania, zimeandaa Ilani ya Uchaguzi ya Wanawake katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2019 na Uchaguzi Mkuu wa Tanzania 2020.

Ilani ya Uchaguzi ya Wanawake ambayo ilizinduliwa Septemba 27 mwaka huu wakati wa kilele cha Maadhimisho ya Tamasha la 14

INAENDELEA UK.16

Nigeria ilivyofufua uhusiano na taifa la Afrika Kusini Ukurasa 15

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) Selemani Jafo. PICHA: MTANDAO

IMF mbioni kurejesha msaada wa fedha DRC Ukurasa 17

UKURASA 13

# Kikwete ataja mambo 9 Nyerere kukumbukwa

• **Asema** ndiyo yaliyoifikisha nchi ilipo sasa, asisitiza umuhimu viongozi kujishusha... *Endelea ukurasa 2*



Rais mstaafu, Jakaya Kikwete, akisisitiza jambo katika Kongamano la Kumbukizi ya miaka 20 ya kifo cha Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**


## YALIYOMO

UKURASA WA 5

**DC AGOMA KUFUNGUA SEMINA ZA POSHO**

MKUU wa wilaya, amekataa kufungua au kufunga semina yoyote itakayofanyika yenye lengo la kulipana posho kwa...

UKURASA WA 7

**KONTENA 143 ZANASWA ZIKIWA NA BIDHAA BANDIA**

TUME ya Ushindani (FCC) imekamata makontena 143 kati ya 3,312 yaliyokaguliwa wakati wa ukaguzi wa kushtukiza na...

UKURASA WA 26

**SABABU KUSHUKA MFUMUKO WA BEI**

MFUMUKO wa bei kwa mwaka ulioishia Septemba 2019 umepungua na kufikia asilimia 3.4, huku bidhaa zisizo za vyakula...


## Vigogo wengine waachiwa msamaha wa Rais

UKURASA 3

## Jaji Mkuu atoa angalizo ulipaji fedha za uhujumu

UKURASA 2

MICHEZO SIMBA YAFUATA DAWA AZAM KWA WARUNDI UK.32

MAONI, KATUNI UK.6

# JK ataja mambo 9 Nyerere kukumbukwa

**Na Romana Mallya**

RAIS mstaafu wa awamu ya nne, Jakaya Kikwete, ametaja mambo tisa ambayo Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, atakumbukwa na viongozi wanapaswa kuyaiga na kuyaishi.

Kikwete aliyataja mambo hayo jana katika Kongamano la Kumbukizi ya Miaka 20 ya Kifo cha Baba wa Taifa, lililofanyika katika Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Kivukoni jijini Dar es Salaam.

Kikwete alitaja jambo la kwanza la kumkumbuka Nyerere kuwa ni ukombozi wa nchi. Alisema Nyerere alisimama mstari wa mbele kuhakikisha ukombozi wa nchi unapatikana kutoka kwa wakoloni.

"Kwa maono yake ya mbali alipopewa uongozi wa TANU, kila walivyokaa na kujadili maslahi, walibaini siasa za kuwaletea watu uhuru na kuamua kuundwa Tanu na yeye kuwa Rais.

"Kwa vile, hawakuruhusiwa kufanya kazi na siasa, akaamua kuchagua kuacha ualimu Pugu na kupiga siasa isiyokuwa na mshahara. Kazi yake ikawa kuzunguka kudai uhuru ambao hakuwa na uhakika kama utapatikana na kama utapatikana, utapatikana lini. Kwa moyo wa upendo kwa wenzake alijitoa kwa ajili ya maslahi ya wengi.

Alilitaja jambo lingine kuwa ni utayari wa kujitoa. Katika hilo alisema Nyerere aliacha kazi yenye mshahara kwa matumaini kuwa nchi ikipata uhuru Watanzania wote watafanikiwa. Alisema Nyerere amewafundisha kuwa na moyo wa tayari kujitolea kwa maslahi ya wengi.

Kikwete alitaja jambo la tatu la kukumbukwa ni Watanzania wamshukuru kwa karama alizopewa kwa kuendesha harakati za kudai

INAENDELEA UK.8



Magari yakipita kwa shida kwenye maji ya mafuriko katika eneo la Gold Star, kutokana na mvua zilizonyesha, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Jaji Mkuu atoa angalizo ulipaji wa fedha uhujumu

**Na Mwandishi Wetu**

JAJI Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahimu Juma, amesema suala la watuhumiwa kukiri na kulipa fedha linapaswa kufanyika kwa hiyari ili kukwepa watu kukimbilia Mahakama Kuu au Rufani.

Aidha, amesema jambo hilo ni zuri na siyo geni kufanyika Tanzania bata, huku akitoa mfano kuwa linatekelezwa Zanzibar, Kenya na Marekani.

Jaji Mkuu aliyasema hayo jana alipokutana na uongozi wa Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika, tawi la Tanzania (Misa Tan), kujadili maeneo ya ushirikiano katika kuimarisha utoaji na upatikanaji wa taarifa kwa umma.

"Sheria ya kukiri makosa inasisitiza hiyari, Mahakama zinatakiwa kwamba makubaliano yaliyofanyika ni hiyari, kwa kuwa ikikosekana hiyari mapema ikifika Mahakama Kuu au Rufani ni tatizo," alisema.

Alisema wananchi wanapaswa kuelimishwa uzuri wa jambo hilo, na kwamba kamati ya kanuni ya Jaji Mkuu ilipendekeza jambo hilo tangu mwaka 2013 na walitengeneza nyaraka. "Ni jambo zuri sana na muhimu, linasaidia kupunguza msongamano magerezani, msongamano wa upelelezi, inasaidia wananchi kuwa wakweli... kama umefanya kosa unakuwa mkweli,"

INAENDELEA UK.8

# Magufuli awaamuru aliyeibiwa ng'ombe alipwe mil.15/-

**Na Beatrice Moses**

VIGOGO watatu wa serikali na Jeshi la Polisi, wamejikuta katika wakati mgumu baada ya Rais John Magufuli kuwaamuru kumlipa Sh. milioni 15 mjane, Felister Mkomo, aliyelalamika kuibiwa ng'ombe 25.

Viongozi ambao ni Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Rukwa, Mkuu wa Wilaya ya Nkasi na Mkuu wa Polisi Wilaya ya Nkasi, wamepewa siku tano kumlipa mama huyo.

Hayo yalijitokeza kwenye mkutano wa hadhara na wananchi katika uwanja wa Sabasaba, Nkasi wilayani Rukwa.

Rais Magufuli aliwataka wafugaji waache kuibiana mifugo, huku akisisitiza vikundi vya ulinzi wa mifugo viimarishwe, pia aliwahoji wananchi iwapo kuna wezi wa mifugo wanaowajua ambao walikamatwa na kuachiwa na polisi.

Miongoni mwa wananchi waliojitokeza kuwataja wezi wa mifugo ni Mkomo, ambaye alimweleza Rais kuwa aliibiwa ng'ombe 25, na kuwa walimkamata mwizi na kumfikisha polisi. Alisema licha ya kushikiliwa na polisi siku mbili, mtuhumiwa aliachiwa kwa dhamana, huku polisi wakidai kwamba amekubali atalipa Sh. 500,000 kwa kila ng'ombe, hivyo alitakiwa kumlipa Sh. milioni 12.5 kwa kuwa ng'ombe wawili kati ya 25 walipatikana.

"Tumeenda kwa Mkuu wa Wilaya kama mara mbili hatukusaidiwa, tuliende usalama hatukusaidiwa, tulienda Takukuru hatukusaidiwa, tukaenda mkoani kwa mkuu wa polisi akawaita," alisema mama huyo.

Rais Magufuli alimwita Mkuu wa Wilaya, Said Mtanda na kumhoji, hivyo alijieleza kuwa anamfahamu mama huyo na amelishughulikia jambo lake kwa kuzungumza na Mkuu wa Polisi wa Wilaya.

Myanda alisema alimwagiza kuhakikisha mdhamini wa mtuhumiwa wa wizi anakamatwa na kufikishwa mahakamani, baada ya mtuhumiwa kutoroka.


## UBALOZI WA UINGEREZA NA CANADA DAR ES SALAAM

## MNADA WA HADHARA:

**UNIVERSAL AUCTION CENTRE** Kwa idhini waliyopewa na Ubalozi wa **Uingereza na Canada** watauza kwa mnada wa hadhara Magari, Generator na Funicha za nyumbani na za Ofisini tarehe 12 October, 2019 Jumamosi kuanzia saa 4:00 asubuhi. Mnada utafanyika Golden Resort Sinza, Lion Street.

**Fenicha zitaanza kuuzwa kuanzia saa 4:00 asubuhi:** Sofa set, Sofa Bed,Chest drawer, Book Shelve, Meza za ofisi, Viti,File Cabnet, Vitanda, Magodoro,TV, Washer, Dryer, Water Dispansor, A/c split units, Photocopy, Computer set na vingine vingi.

**Magari na Generator yataanza kuuzwa saa 5:00 asubuhi.**

| Idadi | Aina | Model | Mwaka | Ushuru |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Land Rover Discovery 4 S/ Wagon | Diesel Engine | 2012 | Haujalipwa |
| 2 | Land Rover Free lander 2 S/ Wagon | Diesel & Petrol Engine | 2012 | Haujalipwa |
| 1 | Mercedes Benz Saloon | WDB Diesel Engine | 2002 | Umelipwa |
| 2 | Isuzu P/Up double cabin | 4JB1 Diesel engine | 2006/7 | Haujalipwa |
| 1 | Toyota Surf Station Wagon | 1KZ Diesel Engine | 1995 | Umelipwa |
| 1 | Generator 27 KVA | Perkins Diesel Engine | 2001 | Haujalipwa |
| 3 | Air Conditioner (Central Cooling Unit) | Cooling – 19.08 KW. | - | Haujalipwa |

Mali zote zinaweza kukaguliwa Golden Resort Sinza, Lion Street kuanzia tarehe 10 mpaka 11 Octoberr, 2019,saa 4:00 asubuhi mpaka saa 11:00 jioni.

**MASHARTI YA MNADA.**

1. Mnunuzi wa Fanicha atatakiwa kulipa malipo yote kwa mweka hazina (cashier). Na mnunuzi wa Gari au Generator atatakiwa kulipa 25% pale pale na salio lilipwe ndani ya siku 4 za kazi ukishindwa kulipa kwa muda huo Gari au Generator litauzwa kwa mshindi mwingine aliyefata na dhamana haitarudishwa.
2. Malipo kwa njia ya VISA na Master cards za CRDB bank yanakubalika.
3. Mali zote zitauzwa kama zilivyo bila dhamana.
4. Mnunuzi atawajibika kulipa ushuru na kodi zingine zote.
5. Mali yote iliyouzwa itatakiwa kuondolewa baada ya kulipa malipo yote pamoja na kodi
6. Kila mtu atatakiwa kuwa na bid namba itakayo patikana getini.

**Kwa maelezo zaidi waone:**
**UNIVERSAL AUCTION CENTRE**
**PLOT NO: 5 "E" LION STREET SINZA**
**CELL NO: 0754 284 926, 0757 284 926**
**E-mail: universalauction@hotmail.com DAR ES SALAAM**

115451602

**HABARI KITAIFA**

# Vigogo wengine waachiwa msamaha wa Rais

**Na Beatrice Shayo**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu imemhukumu Mkurugenzi wa Kampuni ya Aste Insurance Brokers, Astery Ndege kulipa fidia ya Sh. 293,446,400.23, hasara aliyosababisha kwa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (Nida) baada ya kukiri makosa yake.

Uamuzi huo ulitolewa jana katika mahakama hiyo, baada ya Ndege kukiri makosa yake ya kusababisha hasara ya zaidi ya Sh. bilioni 1.1.

Mshtakiwa huyo aliandika barua ya kuomba msamaha kwa Mkurugenzi wa Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini (DPP) na kuingia makubaliano.

Hakimu Mkazi Mwandamizi, Salum Ally, alisema mshtakiwa atatakiwa kulipa faini ya Sh. milioni nne kwa mashtaka mawili yanayomkabili ikiwamo ya kuongoza genge la uhalifu na kusababisha hasara hiyo.

Alisema kuwa amezingatia kitendo cha mshtakiwa kukiri kosa lake na sheria inayoelekeza mshtakiwa kulipa faini.

Awali, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Ladislaus Komanya, aliwasomea washtakiwa wote mashtaka 50 badala ya mashtaka 100 yaliyokuwa yakiwakabili awali.

Washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni Meneja Biashara wa Nida, Avelin Momburi na Ofisa Usafirishaji, George Ntalima, Mkurugenzi wa Sheria, Sabina Raymond na Xavery Kayombo.

Komanya alidai washtakiwa wanakabiliwa na mashtaka 50, yakiwamo ya kutumia nyaraka kumdanganya mwajiri, kughushi, kutoa nyaraka za uongo, kutakatisha fedha na kusababisha hasara ya Sh 1,175,785,600.93 kwa NiDA.

Washtakiwa wote walikana mashtaka isipokuwa mshtakiwa Ndege alikiri mashtaka ya kujihusisha na genge la uhalifu na kusababisha hasara ya zaidi ya Sh. bilioni moja.

Pia Mkurugenzi Mkuu wa Benki M Tanzania, Sanjeev Kumar (63), ameachiwa huru baada ya kutakiwa kulipa fidia ya zaidi ya Sh bilioni 6.03 kutokana na kukiri makosa yake na jana, alilipa Dola za Kimarekani 300,000 sawa na Sh. milioni 690.

Mahakama imemtaka Kumar kulipa fidia hiyo ndani ya miezi 24 na endapo atakiuka makubaliano hayo Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP) atamchukulia hatua.

Hukumu hiyo ilitolewa jana jijini Dar es Salaam katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu.

Uamuzi huo umekuja baada ya upande wa mashtaka kumfutia mashtaka ya uhujumu uchumi na kumsomea mashtaka mawili ya kuisababishia serikali hasara.

Baada ya kusomewa mashtaka yake, mshtakiwa alikiri kufanya makosa hayo.

Akisomewa hukumu yake na Hakimu Mkazi Mkuu Huruma Shaidi, alisema katika mashtaka hayo mawili mshtakiwa atatakiwa kulipa faini ya Sh. milioni moja kwa kila kosa.

Alisema mshtakiwa atatakiwa kulipa fidia ya Sh. 6, 039,103,579 na atailipa kwa miezi 24, kwa kila mwezi kulipa kiasi cha Sh. milioni 222.8.

Hakimu Shaidi alisema hati ya kusafiria ya mshtakiwa huyo itabaki katika Ofisi za DPP na safari zake zote zitafuatiliwa na ofisi hiyo.

Kabla ya kusomwa kwa hukumu hiyo, Wakili wa Serikali, Jaquline Nyantori, alidai kuwa hawana rekodi ya makosa ya nyuma ya mshtakiwa hivyo, aliomba mahakama itoe adhabu kulingana na makubaliano ili iwe fundisho kwake na wengine.

Wakili Nyantori alidai kuwa wameingia makubaliano na mshtakiwa huyo baada ya kukiri kosa la kuisababishia serikali hasara wameamua kuondoa mashtaka ya kughushi, kutakatisha fedha, kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na kuwasilisha nyaraka za uongo.

Baada ya kusoma makubaliano hayo, Hakimu Shaidi alimuapisha mshtakiwa na kumuuliza kama alisaini kwa hiari yake na kudai alifanya hivyo kwa hiari yake.

Akisoma mashtaka mapya, Wakili Nyantoru alidai katika shtaka la kwanza, Januari 20, 2016 mshtakiwa huyo akiwa Mkurugenzi Mkuu wa Benki M Tanzania kwa vitendo vyake alivyovifanya aliisababishia serikali kupata hasara ya Sh. 6,039,103,579.

Alidai katika shtaka la pili, mshtakiwa huyo anadaiwa Januari 20, 2016 akiwa katika Jiji la Dar es Salaam kwa njia ya ulaghai ndani ya Benki M Tanzania akijua ni udanganyifu alijipatia Dola za Marekani 287,000.

Katika hatua nyingine, mfanyabiashara David Mudi na wenzake wanne, wamehukumiwa kulipa fidia ya Sh. milioni 40 katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu baada ya kupatikana na hatia katika kesi ya uhujumu uchumi kwa kujihusisha na nyara za serikali bila kibali.

Washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni Mohamed Salum Mohamed, Mustapha Bakari, Salum Wakili na Shabani Haji.

Washtakiwa hao walipewa adhabu hiyo jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu mbele ya Hakimu Mkazi Janet Mtega.

Washtakiwa hao walipewa adhabu ya kifungo cha nje kwa sharti na kutofanya kosa hilo tena na washirikiane na serikali kutoa taarifa za watu wengine wanaojihusisha na makosa kama hayo.

Hakimu aliwaeleza washtakiwa hao kuwa, watalipa fidia hiyo ya Sh. milioni 40 kwa utaratibu uliooneshwa katika hati ya makubaliano.

Washtakiwa hao ni miongoni mwa waliomwandikia barua Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kukiri na kuomba msamaha.

Washtakiwa hao wanadaiwa kati ya Novemba mosi hadi 16 mwaka 2015, Zanzibar na Dar es Salaam, walijihusisha na usafirishaji wa kobe 201 wenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 30 bila kibali kutoka kwa Mkurugenzi wa wanyamapori.


TRA

**MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA**

## TAARIFA KWA UMMA

Mnamo tarehe 14 Juni, 2018, Waziri wa Fedha na Mipango alitangaza msamaha maalum wa riba na adhabu kwa Walipakodi wenye malimbikizo ya madeni, na wale ambao wako tayari kuweka wazi madeni ya nyuma kwa hiari yao wenyewe na kulipa kodi ya msingi kwa utaratibu ulioanishwa katika (Amri Na. 282A ya Msamaha wa Riba na Adhabu), 2018.

Mpango maalum wa msamaha wa riba na adhabu ni fursa maalumu ya muda mfupi iliyotolewa. Utaratibu huu ulianza 01 Julai, 2018 hadi Juni 30, 2019 na ilihusisha malimbikizo ya madeni ya kodi yaliyokuwepo.

Hata hivyo, Serikali kupitia Sheria ya Usimamizi wa Kodi (Msamaha wa Riba na Adhabu), (Nyongeza ya muda wa kulipa)2019 , iliongeza muda wa malipo ya kodi ya msingi kufikia tarehe 31 Disemba 2019 kwa walipakodi ambao;

a) waliomba msamaha wa riba na adhabu za kodi kwa Kamishna Mkuu;
b) waliopatiwa msamaha wa riba na adhabu za kodi;
c) waliingia makubaliano na Kamishna Mkuu ya kusamehewa riba na adhabu za kodi kama ilivyoanishwa katika Amri Na. 282A ya Msamaha wa Riba na Adhabu), 2018;
d) walianza kulipa kodi ya msingi kwa mkupuo au kwa awamu; na
e) mpaka kufikia tarehe 30 Juni, 2019 walishindwa kulipa kiasi cha kodi ya msingi kilichokubaliwa kwa ukamilifu.

Hivyo, wastahiki wote wa msamaha waliopatiwa msamaha wa riba na adhabu za kodi mnakumbushwa kulipa kodi ya msingi kama ilivyoainishwa kwenye mikataba ya makubaliano wa malipo kabla au kufikia tarehe 31 Disemba, 2019 na kwamba hakuna nyongeza zaidi ya muda itakayotolewa.

Izingatiwe kwamba, pindi mstahiki wa msamaha aliyepatiwa msamaha wa riba na adhabu za kodi kupitia Sheria ya Usimamizi wa Kodi (Msamaha wa Riba na Adhabu), 2018 atashindwa kutekeleza sehemu ya masharti ya mkataba wa makubaliano wa malipo, Kamishna Mkuu atabatilisha mkataba wa makubaliano wa malipo na kudai kiasi cha kodi kilichosalia kama vile hakukuwa na msamaha alioutoa. Aidha, hatua za ukusanyaji zitachukuliwa kuanzia tarehe 2/1/2020 bila taarifa nyingine.

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

**Dr. Edwin P. Mhede Ph.D**
**KAMISHNA MKUU**

215445702

# Mahakama yawaweka kando wazee washauri

**Na Mwandishi Wetu**

JAJI Kiongozi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Dk. Eliezer Feleshi, amesema Mahakama inakusudia kupunguza kuwatumia wazee washauri wa Mahakama katika kuamua mashauri mahakamani.

Badala yake amesema itabaki ikiwatumia katika mashauri ambayo yataonekana yana ulazima wa kuwatumia wazee hao.

Akizungumza wilayani Bunda mkoani Mara katika ziara ya kikazi kukagua shughuli za Mahakama, Jaji Kiongozi alisema wazee hao watatumiwa na Mahakama kwenye mashauri ambayo yatakuwa na ulazima wa kuwatumia, lakini yale ambayo siyo lazima, wazee hao wataacha kutumiwa.

Jaji Kiongozi alisema baadhi ya wazee washauri wa Mahakama hujihishirikisha na vitendo vya rushwa na wakati mwingine huwatisha Mahakimu wanapokuwa wakitekeleza wajibu wao.

Alisema matumizi ya wazee washauri wa Mahakama wakati mwingine husababisha mashauri kuchelewa kumalizika kutokana na kuchelewa kwao kufika mahakamani na kusababisha mashauri kutokusikilizwa kwa wakati.

Akizungumza kuhusu rushwa, Jaji Feleshi alisema Mahakama kama taasisi haijishirikishi na vitendo vya rushwa bali vitendo hivyo hufanywa na baadhi ya watumishi wasio waaminifu ndani ya Mahakama.

"Tuachane na maneno mepesi mepesi kuhusu rushwa kwa kuwa taarifa zipo, pelekeni Takukuru, hakuna anayemlinda mtu," alisema Jaji Kiongozi.

Alisema Mahakama itashirikiana na Serikali katika kupambanana na rushwa, hivyo aliwataka wananchi wenye taarifa juu ya vitendo hivyo kuwasilisha Takukuru.

Akizungumza na watumishi wa Mahakama ya Wilaya ya Bunda, Jaji Kiongozi aliwataka kufanya kazi kwa bidii, uadilifu na kubeba matarajio ya taasisi kwa kutoa huduma bora kwa wananchi.

Aliwataka Mahakimu kumalizika mashauri kwa wakati pamoja na kutoa nakala za hukumu na mienendo ya mashauri katika muda uliopangwa.

Kwa mujibu wa utaratibu, nakala za hukumu ni siku 21 tangu kumalizika kwa shauri na mienendo ya shauri hutolewa ndani ya siku 30.

Aidha, aliwataka watumishi hao kujenga tabia ya kutafuta na kufahamu taarifa mbalimbali za Mahakama kupitia Tovuti pamoja na Blog ya Mahakama ya Tanzania.

Mkuu wa Wilaya ya Bunda, Lydia Bupilipili, aliwashauri watumishi hao kujenga mazingira yatakayowafanya wananchi kuendelea kuiamini Mahakama ya Tanzania kwa kutoa huduma bora kwa wananchi.

Jaji Kiongozi ameanza ziara ya kikazi ya siku tano Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Musoma ambapo atakagua shughuli mbalimbali za Mahakama wilaya za Bunda, Serengeti, Tarime na Musoma.




Mwandikishaji daftari la wapiga kura katika uchaguzi wa serikali za mitaa, kituo cha Kishoka Chang'ombe jijini Dodoma, Domina Kimario (kulia), akimsaidia mkazi wa mtaa huo, Rozalia Garawa, kuweka saini kwa kutumia dole gumba, wakati wa siku ya kwanza ya zoezi la uandikishaji lililoanza jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mizigo bandarini Dar yaongezeka kwa 6.0%

**Na Salome Kitomari**

SHEHENA ya mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam imeongezeka kutoka tani za uzito 16,197,818 mwaka 2017/18 hadi 17,166,079 mwaka huu, ikiwa ni ongezeko la asilimia 6.0.

Akizungumza na wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA), Deusdedit Kakoko, alisema ongezeko hilo ni la tani 968,261 ikiwa ni kiwango cha juu kuwahi kufikiwa kati ya mwaka na mwaka katika historia ya mamlaka hiyo.

Alisema shehena ya kichele ambayo ni nafaka na bidhaa nyingine za aina hiyo ilipungua kwa wastani wa asilimia 2.7 kwa mwaka na kwa mwaka 2018/19 ilikuwa tani za uzito 2,191,697 ikilinganishwa na tani 1,896,748 za mwaka 2017/18.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi huyo, shehena ya kawaida kwa miaka mitano kuanzia 2014/16 hadi 2018/19 kulikuwa na ongezeko la shehena inayopakuliwa kutoka nje kwa asilimia 2.0.

Alisema kwa kipindi cha mwaka 2018/19 shehena ya kawaida iliyopakuliwa ilikuwa tani za uzito 5,681,419 ikilinganishwa na tani 5,224,330 za mwaka 2018/18 sawa na ongezeko la tani 457,088.

Alisema shehena ya kawaida ilikuwa ni tani 2,717,723 zikilinganishwa na tani za uzito 2,720,554 za mwaka 2017/18 sawa na upungufu wa tani za uzito 2,831.

Kakoko alisema shehena ya mafuta iliyohudumiwa kwa kipindi cha miaka mitano ilikuwa ikiongezeka kwa wastani wa asilimia 5.4 kwa mwaka.

Pia, shehena iliyohudumiwa kwa mwaka 2018/19 ilikuwa tani milioni 6.052 ikiwa ni ongezeko la tani 48,634 sawa na asilimia 0.8 ikilinganishwa na tani milioni 6.003 zilizohudumiwa mwaka 2017/18.

Kadhalika shehena ya makontena iliongezeka kwa asilimia 2.4 kwa mwaka, ikiwa ni ongezeko la asilimia 8.0.

Kakoko alisema kwa kipindi cha miaka mitano mapato na matumizi yaliongezeka kwa wastani wa asilimia 7.6 kwa mwaka, kiasi cha kupata ziada ya Sh. milioni 464.4, ikiwa ni pamoja na kuongeza kiasi cha fedha kinachopelekwa serikalini.

Alisema michango katika mfuko mkuu wa serikali iliongezeka kutoka Sh. bilioni 124.24 mwaka 2017/18 hadi Sh. bilioni 141.6 mwaka 2018/19.

## TRA yahimiza ushirikiano mipakani

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

KAMISHNA Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Dk. Edwin Mhede, amezitaka taasisi zinazofanyakazi mipakani kushirikiana ili kurahisisha biashara kwenye mipaka hiyo na kuongeza mapato ya kodi. Dk. Mhede aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na watumishi wa TRA wa vituo vya Forodha vya Kasumulu na Ipyana, vilivyopo Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya katika mpaka wa Tanzania na Malawi.

Alisema taasisi za serikali zinazofanyakazi mipakani zinategemeana hivyo ni vema watumishi hao wakawa na mawasiliano ya karibu ili kurahisisha utendaji kazi, ufanisi mpakani na biashara kati ya Tanzania na nchi zingine zilizopo katika Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

"Ni vema mkawa na vikao hata vya kunywa chai pamoja ili kuimarisha uhusiano na mawasiliano na wenzenu wa taasisi zingine zilizopo hapa mpakani ili kurahisisha utendaji kazi na kuongeza tija katika kazi zenu," alisisitiza Dk. Mhede. Pia, aliwataka watumishi wa taasisi hizo kutambua kuwa wamepewa dhamana ya kusimamia shughuli za serikali katika mpaka wa Kasumulu na mipaka mingine hivyo ni wajibu wa kila mtumishi kufanyakazi kwa bidii ili kutimiza malengo ya serikali ya kurahisisha ufanyaji wa biashara mipakani.

"Ningependa kila mtumishi atambue umuhimu wake kwa taifa hili na dhamana aliyopewa kwa maslahi ya Watanzania wengi," alisisitiza. Taasisi zinazofanya kazi katika mpaka wa Kasumulu ni pamoja na Idara ya Uhamiaji, Shirika la Viwango (TBS), Wakala wa Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), Tume ya Nguvu za Atomic (TaEC), Jeshi la Polisi, Idara Afya, Kilimo, Uvivu, Mifugo, Wakala wa Huduma za Misitu (TFS) na Wakala wa Vipimo (WMA).

Kituo cha Forodha na Ushuru wa Bidhaa Kasumulo kiunahudumia mizigo na abiria kutoka nchi za Malawi, Afrika Kusini, Zambia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) na nchi zingine kusini mwa Afrika. Takwimu zinaonyesha kuwa katika kipindi cha Julai 2016 hadi Septemba 2019 jumla ya tani 243,145 zenye thamani ya Sh. bilioni 567 zimesafirishwa kwenda nchi mbalimbali za SADC kupitia mpaka wa Kasumulu na jumla ya tani 145,937 zenye thamani ya Sh. bilioni 233 ziliingia nchini na jumla ya Sh. bilioni 47.4 zilikusanywa kama kodi katika mpaka huo pekee. Kamishna Mkuu wa TRA, amewapongeza watumishi wa TRA kwa kufanyakazi kwa bidii na kufanikiwa kukusanya jumla ya Sh. trilioni 1.767 katika kipindi cha mwezi Septemba 2019 pekee. Makusanyo ambayo hayajawahi kufikiwa tangu kuanzishwa kwa TRA.

"Nia ya serikali ni kujitegemea kwa kukusanya mapato ya ndani, hivyo sasa ni lazima tufanye kazi kwa bidii tukusanye zaidi ya hiyo trilioni 1.7 ili tuvuke lengo la makusanyo na kuiwezesha serikali kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo," alisisitiza.

Vile vile, aliwataka watumishi wote wa TRA kufanyakazi kwa kufuata maadili ya utumishi wa umma ikiwamo kujiepusha na vitendo vya kuomba na kupokea rushwa kwa sababu kwa kufanya hivyo watakuwa wamekiuka dhamana kubwa waliyopewa ya kukusanya mapato ya serikali yanayowezesha utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kimaendeleo.

# DC agoma kufungua semina za posho

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

MKUU wa Wilaya ya Kahama, Annamringi Macha, amekataa kufungua au kufunga semina yoyote itakayofanyika wilayani hapa yenye lengo la kulipana posho kwa washiriki wake.

Macha alisema hayo juzi wakati akifunga semina ya watoa huduma 36 kutoka katika idara ya afya ya Halmashauri ya Ushetu yeye lengo la kutoa elimu juu ya mfumo wa ukusanyaji taarifa za utoaji huduma za afya na udhibiti wa mapato kwa njia ya elekroniki (GOT-HOMIS).

Alisema kuna baadhi ya watumishi wamekuwa wakiendesha mafunzo mbalimbali kwa lengo moja la kuhalalisha matumizi ya fedha na kujilipa posho jambo ambalo kwa serikali ya awamu ya tano halikubaliki.

"Kama kutakuwa na mafunzo ya namna hiyo yenye lengo la kujipa posho siwezi kuja kabisa na wala mtu asihangaike kunitafuta kwani siwezi kupoteza muda wangu," alisema.

Mkuu huyo wa wilaya alisema ameamua kushiriki katika semina hiyo baada ya kujiridhisha kuwa malengo yake yalikuwa kutoa elimu ya kielekroniki kwa watumishi wa idara ya afya ambayo ni muhimu katika maisha ya kila siku ya binadamu.

Aliwataka wanasemina hao ambao ni watoa huduma katika vituo vya afya na zahanati, kutambua kuwa wagonjwa wengi katika maeneo ya vijijini hutibiwa katika zahanati na kupona huku akisisiza kuwa hospitali za wilaya au zile mkoa ni za rufani tu.

Macha alisema kuwa hospitali za rufani hupokea wagonjwa walioshindikana ambao hutoka katika zahanati au vituo vya afya ambavyo kwa kiasi kikubwa viko maeneo ya vijijini ambako ndiko kwenye kundi kubwa la wananchi wanaohitaji huduma za afya kwa hali ya juu.

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Ushetu, Dk. Nicodemus Senguo, alisema mafunzo hayo ya kutumia kompyuta kwa watumishi wa afya katika zahanati 22 na vituo vya afya vitatu, yatasaidia kuongeza mapato ya halmashauri na kudhibiti mianya ya upotevu wa fedha.

## Tamwa yampongeza JPM kukemea mimba wanafunzi

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha Wanahabari Wanawake Tanzania (Tamwa), kimempongeza Rais John Magufuli, kwa kuzungumzia kwa uwazi na kukemea hadharani suala la ongezeko la mimba kwa wanafunzi mkoani Rukwa.

Taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari na Mkurugenzi Mtendaji wa chama hicho, Rose Ruben, ilisema chama hicho miongoni mwa malengo yake ni kupunguza mimba za utotoni na unyanyasaji wa kijinsia.

Alisema mimba za utotoni zinaitia hasara serikali inayotoa kiasi kikubwa cha fedha kwa ajili ya elimu bure, shule za msingi na sekondari, na kwamba mimba hizo ndicho chanzo cha vifo vya uzazi na maradhi ikiwamo Ukimwi.

Kwa mujibu wa Reuben, taarifa za hivi karibuni zinaonyesha kuwa baadhi ya wanaohusika kuwapa mimba wanafunzi ni walimu, polisi na madereva bodaboda wasiofuata maadili.

"Wakati makundi hayo yanaaminiwa katika kuwapa ulinzi wanafunzi. Kama Rais Magufuli alivyosisitiza, Tamwa inawasihi wazazi na walezi wawafundishe watoto kuepuka vitendo vya ngono na tunaziomba taasisi za dini kuwaelimisha watoto wa kike kujiepusha na vitendo hivyo," alisema.

Aliwaomba viongozi wa dini watoe mawaidha ya kuwakanya wanaume wanaolaghai wanafunzi.

Rais Magufuli ambaye alikuwa ziarani mkoani Rukwa alisema kwa takwimu alizopata kulikuwa na wanafunzi 229 waliopata mimba mkoani humo mwaka jana pekee.


**MAMLAKA YA DAWA NA VIFAA TIBA**

TMDA
Tanzania Medicines & Medical Devices Authority

**TAARIFA KWA UMMA**

Oktoba 08, 2019

**MATANGAZO YA DAWA KATIKA MITANDAO YA KIJAMII**

1. Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) ni Wakala wa Serikali chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto yenye jukumu la kudhibiti ubora, usalama na ufanisi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi.
2. TMDA inapenda kuutangazia umma kuwa kumekuwepo na utangazaji au uwekaji wa taarifa za dawa kwenye mitandao ya kijamii bila ya kuwa na kibali maalum kutoka Mamlaka. Mitandao hiyo ni kama Whatsapp, Blogs, Facebook, Twitter, Youtube, Instagram, LinkedIn, MySpace, Pinterest na kadhalika.
3. Matangazo hayo ni kinyume na Kanuni za Udhibiti wa Matangazo ya Dawa na Dawa za Mitishamba za 2010 (Tanzania Food, Drugs and Cosmetics (Control of Drugs and Herbal Drugs Promotions) Regulations, 2010).
4. Aidha, dawa zinazotolewa kwa cheti cha daktari (Prescription Only Medicines) haziruhusiwi kutangazwa kwenye vyombo vya habari ikiwemo mitandao ya kijamii. Matangazo ya dawa ni lazima yapewe kibali cha kutangazwa kutoka TMDA.
5. Kwa taarifa hii, TMDA inawaelekeza waingizaji, wauzaji, wasambazaji wote wa dawa na umma kwa ujumla, kuacha kuweka matangazo yoyote ya dawa zinazotolewa kwa cheti cha daktari kwenye mitandao hiyo na kuhakikisha kuwa matangazo ya dawa yanayotolewa yanakuwa na taarifa za matumizi sahihi ya dawa na yameidhinishwa na Mamlaka kutumika kutangaza dawa husika.
6. TMDA inatoa rai kwa wananchi wote kuendelea kutoa taarifa ikiwa watabaini kampuni, kikundi, mitandao au mtu yeyote anayejihusisha na utangazaji wa dawa zinazotolewa kwa cheti cha daktari kwenye mitandao ya kijamii hapa nchini.
7. Aidha, hatua stahiki zitachukuliwa kwa wale watakaoendelea kutangaza dawa zinazotolewa kwa cheti cha daktari kwenye mitandao ya kijamii hapa nchini.
8. TMDA itaendelea kufanya udhibiti wa ubora, usalama na ufanisi wa Dawa na Vifaa Tiba. Jukumu la kulinda afya ya wananchi ni letu sote hivyo wadau wote tushirikiane katika kutekeleza maagizo haya kwa mujibu wa kanuni.

**Imetolewa na:**
**Kaimu Mkurugenzi Mkuu,**
**Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA),**
**Mtaa wa Mwanza, Kitalu T, Kiwanja Na.6**
**S.L.P 1253, Dodoma Au**
**S.L.P 77150, Dar es Salaam**
**Simu: +255 22 2452108/2450512/2450751**
**Simu bila Malipo: 0800110084**

215452102

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Tumsifie Rais kwa kuwatunza wasichana

**ASANTE** Rais John Magufuli, kwa kumtetea binti wa Tanzania ambaye amesikia ukiwakanya wanaowapa mimba wanafunzi na wazazi na walezi wanaowaoza watoto kuacha uovu huo.

Angalizo la Rais alilolitoa jana mkoani Rukwa na Katavi linaungwa mkono na kila mmoja na hasa watetezi wa haki za wanawake na watoto. Wakati Rais anawaonya wanaochezea hatima ya watoto, anazungumzia zaidi suala la elimu.

Anakumbusha kuwa serikali inagharamia elimu kila mwezi kwa kutoa mabilioni ya ruzuku na haitakubali fedha zinazokwenda shuleni zisiwanufaisha wasichana.

Anasisitiza elimu kwanza, kwa vile anafahamu kuwa elimu ni moja ya eneo nyeti na muhimu katika kuwawezesha wanawake kumudu maisha yao na za familia zao. Ndiyo maana anawaonya wanaowadhulumu wasichana na mabinti kuwa taifa haliwezi kuvumilia. Rais anasema kila mwezi yanatolewa mabilioni kusomesha watoto wake wa kike na wa kiume na kuachana na mienendo inayodunisha jamii. Anawakumbusha kuwa watoto wadogo 229 wamepata mimba katika mkoa huo, lakini hajasikia wanaume 229 wakiwa wamefungwa jela.

Anaonya kuwa haya si mambo ya kuvumiliwa tena kwa sababu sheria zipo, vyombo vya dola na viongozi wapo na wanatakiwa kuchukua hatua. Tunaungana na Rais kwa kueleza kuwa si wakati wa kuvumilia anguko hilo la mabinti wawe shuleni au mitaani. Kama taifa hatuwezi kuisahau mikutano mikubwa ya dunia iliyozungumzia masuala ya ustawi wa wanawake ya Cairo -Misri na Beijing nchini China.

Mkutano wa Beijing ni muhimu kwa taifa hili kwa vile ulisimamiwa na Balozi Getrude Mongela na ajenda zilizozungumzwa humo nyingi ni mchango wake ambao kama taifa tunatakiwa kuuenzi kwa kuwasomesha na kuwaendeleza wanawake.

Kama Rais alivyosema hiyo ni aibu na kuwataka, wabunge, madiwani, viongozi wa dini, mashehe na machifu walisimamie linaleta doa kwenye mikoa yao.

Angalizo hili la Rais ni muhimu kwani elimu pekee ndiyo itakayowahakikishia wanawake maisha bora kwani bila, elimu hakuna maendeleo na ukandamizaji wa watoto na jamii hautakoma. Kwa Tanzania suala la wanawake na mabinti kuwa nyuma kimaendeleo halina ubishi. Ndiyo maana Rais anasema wasichana wawe kama nyara za serikali kila mmoja awalinda.

Ikumbukwe kuwa kwenye elimu ndiko ambako wanawake na mabinti wako nyuma zaidi. Mathalani, tunapozungumzia idadi ya watoto ambao walitakiwa kuwa shuleni lakini hawapo, wengi watakuwa wasichana.

Tukitaja takwimu za watoto walionyanyaswa, wengi ni wa kike, kadhalika kila jambo litawataja wanawake kuwa ndiyo wanaoumia zaidi. Kwa hiyo tuungane na Rais kuwalinda na kuwapa wasichana elimu kwani ndiyo dawa pekee ya kuondoa umaskini wa taifa letu. Kuwasomesha ni kuwahakikishia uwezo mkubwa na nguvu za kutosha zitakazowawezesha kufanya maamuzi sahihi kwa ajili ya maisha yao na ya nchi yao.

Ikumbukwe kuwa ni lazima wanawake kama raia wa taifa hili wawe na afya bora na hiyo iwe sababu nyingine ya kuwawezesha kusoma na kupata elimu bora. Faida nyingine muhimu kwa taifa inayotokana na elimu ya wanawake ni kuwa na ujuzi, kupata taarifa mbalimbali (information) na kujiamini kwa kila wanalofanya. Iwe afya ya uzazi, malezi bora na uwekezaji huko ndiko utakakowezesha kuwa na familia na wazazi bora, wafanyakazi mahiri na makini na raia wema.


Tukumbuke kuwa mwanamke aliyeelimika si rahisi kujiingiza katika mambo yasiyo na maadili yanayoangamiza maisha.

Mathalani kuuza mihadarati na kufanikisha matumizi ya dawa hizo miongoni mwa vijana.

Tunaamini kuwa wanawake wasomi na walioelimika ni watendaji na wachapakazi mahiri ofisini na nyumbani.

Hivyo tuungane na Rais kuwalinda na kuwatetea wasichana mitaani na shuleni.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Raphael Kibiriti

## Muungwana Lazima Nilonge

# Ma-RC, DC simamieni malipo pamba ya wakulima nchini

**MSIMU** wa kilimo katika baadhi ya maeneo nchini ambayo hupata mvua za masika kati ya mwezi Oktoba hadi Machi, tayari umeshaanza na wakulima katika hekaheka mbalimbali za uzalishaji katika mashamba yao.

Na kama takwimu kutoka vyanzo mbalimbali zinavyobainisha, kilimo ni shughuli kuu ya kiuchumi kwa takribani asilimia 70 ya Watanzania karibu milioni 55 kwa sasa, wengi wakiishi vijijini ambako ndiko hasa kilimo kinaendeshwa kwa kiwango kikubwa.

Mojawapo ya maeneo hayo ni Kanda ya Ziwa ambayo ni maarufu kwa uzalishaji wa mazao mbalimbali ya chakula kwa ajili ya usalama wa chakula na lishe, bila kusahau mazao ya biashara, likiwamo zao maarufu la pamba katika kanda hiyo.

Hata hivyo, wakati msimu ndio huo umeshaingia na harakati mbalimbali za kilimo zikiendelea zikiwamo za ununuzi wa pembejeo kwa maana ya mbegu bora, dawa za kuua wadudu waharibifu wa mazao na mbolea bado kuna kilio kwa baadhi ya wakulima wa pamba.

Wakulima kutoka katika baadhi ya maeneo yakiwamo ya Kanda ya Ziwa.

Kilio anachokizungumzia Muungwana ni cha baadhi yao kutolipwa fedha mpaka sasa wakati msimu wa kilimo ukianza, baada ya kuwa wameuza pamba kwenye Vyama vya Ushirika vya Msingi (AMCOS).

Hali iko hivyo hata baada ya ahadi ya serikali kuwa wakulima wote watakuwa wamelipwa haki yao hiyo kabla ya msimu huu wa kilimo ili wajiandae vyema.

Msimu ambao pamoja na mengine, unamhitaji mkulima awe na fedha kwa ajili ya mahitaji mbalimbali ya kilimo, yakiwamo yaliyobainishwa hapo juu.

Septemba 21, mwaka huu, akiwa Chato katika moja ya ziara zake, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa alitoa ahadi kuwa wakulima wote waliouza pamba kwenye vyama vya ushirika watalipwa fedha zao.

Kwamba serikali ilikuwa imeingilia kati na kuruhusu wanunuzi wa pamba wachukue fedha benki ili pamba yote inayonunuliwa kwa wakulima iweze kulipwa.

Kwa mujibu wa taarifa alizozipata Muungwana kutoka maeneo mbalimbali ya Kanda ya Ziwa, kuna baadhi ya kampuni za ununuzi hazijapeleka fedha kwa wakulima sasa ikiwa ni zaidi ya mwezi mzima.

Kwa mfano katika Wilaya ya Maswa, mkoani Simiyu, kuna baadhi ya kampuni za ununuzi hazijawapelekea wakulima fedha zao kwa zaidi ya wiki sita sasa, pamoja na kuwa zimeshasomba pamba ya wakulima kutoka kwenye maghala ya AMCOS.

Kwamba wanunuzi wameshachukua pamba ya wakulima na kuipeleka kwenye viwanda vyao na baadhi ya kampuni zinaendelea kusomba pamba hiyo kutoka katika maghala ya AMCOS, lakini kuwapelekea wakulima fedha zao, bado imekuwa ngumu.

Kama ilivyobainishwa hapo juu, baadhi ya maeneo tayari yako kwenye msimu wa kilimo, lakini kuna wakulima ambao hawajalipwa fedha zao!

Muungwana anaona hali hii kimsingi inakwamisha juhudi za wakulima za kuongeza uzalishaji katika shughuli hii wanayoitegemea kwa udi na uvumba ili kuboresha maisha yao, na hivyo kuondokana na lindi la umaskini.

Katika moja ya maelekezo yake kuhusiana na sakata hili, Waziri Mkuu aliagiza wakuu wa mikoa na wilaya kuwasimamia wanunuzi.

Kwamba kuwasimamia ili kuhakikisha kuwa fedha wanayochukua kutoka benki kwa dhamana ya serikali ili wakawalipe wakulima wa pamba, inatumika kwa kusudi hilo.

Sasa inapotokea kwamba kuna baadhi ya wakulima wana zaidi ya mwezi hawajalipwa fedha zao, wakati wanunuzi tayari wamesomba pamba yao, Muungwana anaona hapo kuna upungufu katika usimamizi wa maelekezo ya Waziri Mkuu.

Ni kwa maana hiyo Muungwana anawaasa wakuu hawa wahakikishe wanunuzi wanawalipa wakulima fedha zao, ili waweze kugharamia pamoja na mengine mahitaji ya kilimo, ikichukuliwa msimu wa kilimo tayari umeshafika kwenye baadhi ya maeneo.

## HABARI KITAIFA



Kamishna Jenerali wa Magereza, Phaustine Kasike (wa pili kulia), akikagua matofali ya kuchoma katika mradi wa ufyatuaji tofali za kuchoma katika Gereza la Wilaya ya Mbozi akiwa katika ziara ya kikazi mkoani Songwe hivi karibuni. **PICHA: MAGEREZA**

# Kontena 143 zanaswa na bidhaa bandia

**Na Jumbe Ismailly,** SINGIDA

TUME ya Ushindani (FCC) imekamata makontena 143 kati ya 3,312 yaliyokaguliwa wakati wa ukaguzi 31 wa kushitukiza na kukutwa yakiwa na bidhaa bandia.

Akizungumza na waandishi wa habari kwenye viwanja vya maonyesho ya wajasiriamali mjini Singida, Ofisa Mawasiliano na Uhusiano ya Umma wa FCC, Adefrida Ilomo, alisema tume hiyo imepokea na kushughulikia mikataba 46 ya mlaji katika kipindi cha mwaka 2018/19.

"Tume imefanya ukaguzi katika kontena 3,312 na kati ya hayo, 143 yalikutwa yakiwa na bidhaa bandia. Pia tume ilifanya ukaguzi wa kushtukiza mara 31 katika mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Mwanza, Arusha, Mbeya na mipaka ya Sirari, Namanga, Horohoro, Holili, Kasumulo na Tarakea," alisema.

Naye Mwanasheria wa FCC, Exavery Katinda, alisema tume hiyo imeendelea kutoa elimu katika shule za msingi za jiji la Dodoma na Manispaa ya Morogoro na kuendesha klabu za kumlinda mtumiaji wa bidhaa katika shule tano za jijini Dodoma na zingine katika Manispaa ya Morogoro.

Kwa mujibu wa ofisa huyo wanafunzi katika klabu hizo hufundishwa masuala ya kumlinda mtumiaji bidhaa na udhibiti wa bidhaa bandia ili wawe walimu katika jamii.

Sambamba na wanafunzi kupatiwa elimu hiyo, Katinda alisisitiza kuwa tume pia imeendesha mafunzo kwa wadau mbalimbali wakiwamo maofisa upelelezi wa makosa ya jinai wa mikoa na wilaya wa jeshi la polisi kwa kanda zote za kipolisi katika kipindi cha kuanzia Oktoba, mwaka jana hadi Februari, mwaka huu.

Wengine waliopatiwa mafunzo hayo ni wadau wa viwanda, wananchi na wajasiriamali katika Maonyesho ya 43 ya Biashara ya Kimataifa (Sabasaba), Maonesho ya Wakulima (Nanenane) katika viwanja vya Nyakabindi, Bariadi mkoani Simiyu, maonyesho ya wajasiriamali ya Bugene, Buseresere, Chato na Maonyesho ya Wajasiriamali Singida.

# W/biashara wapozwa manyanyaso ya Kenya

**Na Zanura Mollel,** NAMANGA

MBUNGE wa Longido Mkoani Arusha Dk. Steven Kiruswa, amewataka wafanyabiashara wa mifugo kufuata taratibu zilizoweka na serikali hadi hapo meza ya maridhiano kati ya Kenya na Tanzania yatakapofanyika kuhusu manyanyaso wanayoyapata Kenya.

"Subirini Oktoba 15, tunakutana na viongozi wa Kenya, na tutapata mwafaka juu ya kero na mateso mnayoyapata mkipeleka mifugo Kenya," alisema.

Akizungumza na wafanyabiashara hao katika soko la kimataifa la mifugo Kata ya Kimokouwa kijiji cha Eworendeke, ,alisema hawezi kukinzana na maamuzi ya serikali juu ya kukataza wafanyabiashara wa Tanzania kupeleka mifugo kenya.

"Mnahitaji changamoto zenu zitatuliwe, subirini serikali zikutane,ila siwezi kusema mpeleke mifugo Kenya wakati mnadai usalama weni ni ndogo."

Aliwaeleza baadhi wana tabia ya kutumia maamuzi ya kuzuiwa kupeleka mifugo Kenya, hivyo kupita njia zisizo rasmi ( panya), na kuwataka kuacha tabia hiyo kwani huko ni kupotezea nchi mapato.

"Mpaka umemwaga maaskari wa kutosha kuanzia Wilaya ya Rombo hadi hapa Longido, mtakamatwa na hatua mtachukuliwa, tiini mamlaka ya serikali?" alihoji.

Kuhusu malalamiko ya Passport za Single Journey, alisema alishawasilisha taarifa Ofisi ya Uhamiaji.

Alifafanua kuwa, ili kupata passport kubwa ni lazima mhusika awe na kitambulisho cha Taifa, hivyo aliwataka wafanyabiashara hao kuhakikisha wanajisajili Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA)..

Aidha, alisema kuwa wanaweza kuomba passport ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mbardada Ole Mbaridi, Mkazi Wa Monduli, alidai baadhi ya wafanyabiashara hawajapata taarifa juu ya kuzuiwa kwa mifugo kwenda Kenya, hivyo wafanyabiashara wengine kuendelea kuleta mifugo sokoni, na hakuna suluhu ya kupeleka Kenya.

"Mifugo ipo hapa, hatujui tufanyeje, hatukupata taarifa kama hali si shwari...serikali tunaomba itusaidie," alisema.

Mwenyekiti wa wafanyabiashara wa wifugo soko hilo, Saruni Laizer, alisema wafanyabiashara wana taarifa, lakini wengine wanaonekana kuwa wakaidi kuhusiana na maamuzi yaliyotolewa na serikali.

"Minada yote ina viongozi ambao ni wenyeviti, taarifa wanazo na niliwaambia wawaeleze wafanyabiashara kusitisha biashara ya mifugo hadi hali itakapokuwa shwari," alisema.

Afisa Tawala wilayani hapa, Malaki Tate, alisema msimamo wa serikali utabaki pale pale hadi suluhu itakapopatikana..

## Asilimia 94 Watanzania wanawasiliana kwa simu

**Na Happy Severine,** SIMIYU

NAIBU Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Atashasta Nditiye, amesema kuwa Mfuko wa Mawasiliano kwa wote ambao ni chombo cha serikali umewezesha asilimia 94 ya Watanzania kuwasiliana kwa njia ya simu popote walipo kutokana na kufikishiwa miundombinu ya minara ya simu.

Alisema mfuko huo umejipanga hadi mwaka 2020 kufikia asilimia 100 ya Watanzania wote kuwa na mawasiliano.

Alitoa kauli hiyo jana wakati wa hafla ya kukabidhi kompyuta 100 zilizotolewa na mfuko huo kwa shule 10 za Mkoa wa Simiyu.

Alisema kuwa mfuko katika kutekeleza sera ya taifa ya Tehama, umekuwa ukitoa vifaa vya Tehama katika maeneo mbalimbali nchini lengo likiwa kuhakikisha Watanzania wengi zaidi wanawasiliana na kujifunza kwa njia ya Tehama wakiwamo wanafunzi kwenye shule za sekondari.

"Mpaka sasa Mfuko wa Mawasiliano kwa wote (UCSAF) umefanikiwa kuwawezesha Watanzania asilimia 94 kuwasiliana kwa kutumia simu zao na malengo ya mfuko ni kufikia asilimia 100 kufikia mwaka 2020," alisema Mhandisi Nditiye.

Pia alisema mfuko huo umekuwa ukitoa vifaa vya Tehama zikiwamo kompyuta kwenye shule za sekondari mbalimbali nchini na kugundua kuwa vifaa hivyo havitumiki kwa kazi iliyokusudiwa licha ya kuwafundisha walimu Tehama kwa ajili ya kuvitumia, lakini bado hawajaviona.


Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MERU**
(Barua zote za kiofisi zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)

Mkoa wa Arusha
Telegram: Meru
Simu: (+ 255) 027 254-1112
Faksi: (+ 255) 027 254-1112
Barua pepe: ded@merudc.go.tz
website: www.merudc.go.tz

HALMASHAURI YA WILAYA MERU DISTRICT COUNCIL

Ofisi ya mkurugenzi mtendaji,
S. L. P 462,
USA RIVER
ARUSHA

26/11/2018

**TANGAZO KWA UMMA**

**UUZAJI WA VIWANJA KATIKA MRADI WA NGURUDOTO ESTATE**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Meru kwa kushirikiana na Kampuni ya **ZULFIROZ ESTATE LTD** wanawatangazia wananchi wote kuwa zoezi la upimaji wa viwanja katika eneo la Ngurdoto limekamilika.

Eneo lipo karibu na Hoteli ya Ngurudoto na Shule ya St. Jude takribani Km 1.25 kutoka Barabara ya Rami iendayo Arusha National Park na Km 3.5 kutoka barabara kuu ya Moshi- Arusha. Kuna viwanja kwa ajili ya **makazi, makazi na biashara, biashara pamoja na viwanja vya matumizi ya ibada.**

Bei ya kiwanja ni Tsh. 19,000/= kwa mita moja ya mraba. Kiwanja kinalipiwa ndani ya muda wa mwezi mmoja. Utaandaliwa hati baada ya kukamilisha malipo ya kiwanja.

Kwa yeyote anayehitaji kiwanja afike ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Meru kuchukua fomu na kuchagua kiwanja kuanzia tarehe ya tangazo hili.

Wananchi wote mnakaribishwa

IMETOLEWA NA:

Grace A. Mbilinyi
**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MERU**

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA MERU
S.L.P. 462 USA RIVER
MERU - ARUSHA

215451302

Jordan University College
Constituent College of St. Augustine University of Tanzania
P.O. Box 1878, Morogoro, Tanzania

Ref:0310/HR/19/1 7th October 2019

**ANNOUNCEMENT**

**Position: Lecturers**
- ICT (1), Accounting & Finance (1)

**Reports to the Head of Department**
**Duties**
- Teaching in formal courses and seminars, undertaking individual research and participating in bigger multidisciplinary research projects; preparing manuals, simulations and case studies for training; provide close supervision and guidance to students; working on consultancy projects; coaching junior teaching/research staff and any other duties as may be assigned to him/her by his/her reporting officer.

**Requirements:**
- Lecturer must have PhD in his/her area of specialization. Master's and Bachelor's degree in the relevant field with minimum GPA of 4.0 and 3.8 respectively

**Position: Assistant Lecturers**
- Law (1), Accounting & Finance (1), French Language (1)

**NOTE:** French language teacher, candidates with Bachelors are also invited to apply as tutorial Assistants.

**Reports to the Head of Department**

**Duties**
- With guidance of senior staff members conduct lectures, research and consultancy projects, tutorials, seminars, marking tests, assignments, examinations and submitting results of the same timely. Preparing case studies and any other duties as may be assigned to him/her by his/her supervisor

**Requirements:**
- Assistant Lecturers must have Master's and Bachelor's degree in the relevant field with minimum GPA of 4.0 and 3.8 respectively

**Position: Bursar of the College (1)**
Reports to the Deputy Principal for Finance & Administration (DPFA)

**Duties:**
- Advises the University College Management on financial management and fiscal control
- Develops and maintains an up to date transparent MIS on account at all levels
- Directs and supervises the preparation of periodical financial report and ensures that they are submitted to the appropriate authorities on time
- Prepares the University Budget estimates in both recurrent and development expenditure
- Ensures sound internal controls are in place
- Participates in preparing financial circulars, revenues and expenditure policies of the university
- Ensures that external and internal financial queries are resolved as per the laid down procedures
- Supervises, appraises and identifies staff development and training needs
- Coordinates timely audit of the university financial transactions
- Performs any other duties as may be assigned by supervisor.

**Requirements:**
- Holder of CPA (T) or equivalent qualifications PLUS Master's degree in either Accounting OR Finance from a recognized institution with at least 9 years relevant working experience of which at least five years must be at a senior managerial position in a reputable organization. The candidate must be a person of high integrity with ability to plan, organize and supervise. Self-motivated and ability to work efficiently even under pressure. He/she must have excellent communication skills in both English and Kiswahili. Ability to deliver accurate and high quality output timely.

**Position: Assistant Accountant II (2)**

**Reports to the Bursar of the College**
- Preparing and balancing various subsidiary ledgers;
- Completing bank reconciliations
- Summarizing monthly accounting transactions for posting into the general ledger
- Processing payment and receipts transactions
- Verifying balances in account books and rectifying discrepancies.
- Carrying out regular investigations of accounts
- Verifying JUCo's income from sources to bank and satisfies self that expenditure is properly incurred according to approved policy and efficiently charged to relevant heads;
- Checking that inventory of furniture, equipment, and other moveable assets is maintained accordingly.
- Assisting in audit assignments

**Requirements:**
- Holder of Bachelor Degree in accounting or Accounting and Finance; CPA (T) OR its equivalent qualifications is a PLUS. Candidates with auditing knowledge are more preferred.

**Position: Administrative Officer**
Responsible to the Deputy Principal for Finance & Administration (DPFA)

**Duties and Responsibilities**
- Responsible for the overall status of the DPFA's office
- In charge of general order and cleanliness of the DPFA's office
- Working closely with HR and Bursar's Office in matters of administration and Finance for the DPFA
- Attending meetings presided or attended by the DPFA both internal and external, as a silent observer, but taking notes that are of interest to the DPFA
- Assist the DPFA in preparing various statutory reports.
- Responsible for daily networking both internally and externally;
- Managing arrangements for the copying and dispatch of all documents as may be directed;
- Maintaining office records,
- Ensuring effective transfer of files and records;
- Responsible for managing the confidential data storage for the office, ensuring that confidential documents and personal documentation are kept under secure conditions;
- Performing any other duties as deemed essential for the proper operation of the DPFA's office.

**Requirements:**
- Candidate must be a holder of Bachelor Degree in either arts or social sciences from a recognized institution with at least three years' experience as office administrator. The candidate must be computer literate in Ms Word & Ms Excel with ability to write in both English and Kiswahili languages. Candidates with knowledge of accounts or finances will have added advantages.

**Position: Procurement Officer**
**Reports to the Principal**
**Duties & Responsibilities:**
- Securing reliable supplies.
- Taking charge of purchasing and related activities including market research and supplies appraisal;
- Receiving and processing all requisitions for purchases
- Scrutinizing all purchases orders prior to forwarding them to the DPFA
- Providing advice on all matters related to purchasing function
- Follow up overdue orders
- Preparing monthly, quarterly, min year and annual stock report
- Preparing draft proposals for policies and procedures pertaining to procurement
- In consultation with the bursar organizing and administering purchasing and supplies unit ensuring that systems of purchases and stock control including movement of stocks between departments are operationally sound;
- Overseeing arrangements for the purchase of equipment and materials (other than furniture) required by the College including their effective use;
- Coordinating purchase and effective management of stores;
- Perform any other duties assigned by one's reporting officer.

**Requirements:**
- Holder of master's degree in Procurement and Supply Chain Management PLUS Procurement Supply Chain Professional (PSCP) Certificate with at least six years working experience of which at least three years in a managerial position.

**Position : HR Assistant**

**Report to HRD**
**Duties and Responsibilities**

**Requirements:**
- To assist the HR in achieving Office Objectives including;
- Organizing & Scheduling meetings related to HR Office
- Working as first person in handling employees' service requests and queries related to HR Office
- Providing Orientation to New Staff members
- Opening new files and indexes cards
- Maintaining an up-to-date register of office files (documents) sent out or received
- In charge of Open Registry and Confidential Registry
- In charge of attendance Register
- In charge of sport and games and other welfare matters required for members of staff
- Providing clerical and administrative support services to the HR Office
- Performing any other duties may be assigned by supervisor

**Requirements:**
- BA in HRM, Public Administration or Records from a recognized institution. Working experience of at least three years in HR or Administration department is required. The candidate should have good communication skills, Self-motivated and computer literate in both MS Word & Excel.

**Application Instructions:**

- Send your application consisting of cover letter indicating the position you are applying for in the SUBJECT email, CV in English and Copies of Academic Certificates and transcripts through the following address not later than **15th October 2019.** You are encouraged to send your application electronically through the given email.

**Deputy Principal for Finance and Administration,**
**Jordan University College,**
**P. O. BOX 1878,**
**Morogoro-Tanzania**
**E-mail: dpfa@juco.ac.tz.**

215452302

- Only shortlisted candidates will be contacted. This advertisement is also available on JUCo website: www.juco.ac.tz. Commencement of Employment for Successful Candidates is immediately.

# JK ataja mambo 9 Nyerere kukumbukwa

**INATOKA UK. 2**

uhuru kwa maneno na kupatikana kwa maneno bila kumwaga damu.

"Usione vinaelea vimeundwa. Ni maarifa na uhodari wake ndinyo uliotufikisha hapa. Wako wenzetu haikuwezekana hili walilazimika kutumia nguvu," alisema.

Alitaja jambo la nne kuwa ni imani ya haki na umoja kwa kushirikiana na Abeid Amani Karume kuanzisha taifa la Tanzania jambo ambalo ni urithi mkubwa.

"Hii ni moja ya tunu ya taifa ambayo haikuwapo kwenye ramani lakini wameitengeneza Nyerere na Karume. Wako wengine Afrika wamejaribu ikashindikana. Namibia imeshindikana, sisi tumeweza na tuna miaka 55 sasa na tuna miaka 155 ijayo tutakuwapo," alisema. Jambo la tano alilitaja kuwa ni ujenzi wa taifa lenye umoja, amani na mshikamano miongoni mwa raia.

"Nchi yetu ina makabila 120, dini mbalimbali. Wapo ambao walikuwa hawajaegemea upande wowote si Wakristo si Waislamu. Kwa sasa tuna vyama vya siasa mbalimbali bado nchi ina amani. Kuna matajiri na maskini, wapo wasomi na maprofesa, wapo wasiojua kuandika lakini bado wote wanaishi pamoja. Wenzetu wana makabila mawili na dini moja imeshindikana," alisema.

Jambo la sita , alilitaja kuwa ni kuheshimu utu wa mtu. Alisema pamoja na ukubwa wote aliokuwa nao kama Rais, alikuwa wa kawaida mbele ya wengine na alikuwa anakaa na kuhusiana na watu.

"Ulikuwa ukikaa naye hupati hofu kwamba umekaa na Rais. Ni mtu ambaye alikuwa anaweza kusema weka ndani, ukawekwa ndani lakini Mwalimu hakua hivyo. Alikuwa mnyenyekevu, mpole lakini si kwamba yuko hivyo basi ukagonge naye mkono. Huwezi kufanya hivyo, alifanya hivyo akisisitiza utu na dhamana ya uongozi" alisema.

"Dhamana ya uongozi haikufanyi wewe uwe mtu zaidi ya mwingine yeyote aliyepo pale, haikufanyi wewe kwamba uwe na haki zaidi kuliko mtu mwingine ambaye si kiongozi. Ni jambo kubwa kwa viongozi kutambua kwamba kujishusha hakukufanyi usiwe kiongozi. Ukiwa na wanadamu wenzako ujue nao ni wanadamu kama wewe," alisisitiza.

Kikwete alitaja jambo la saba kuwa Mwalimu aliamini uhuru wa Tanganyika hauna maana kama bado hata nchi moja ya Afrika itakuwa bado imetawaliwa ndiyo maana alihakikisha kudai uhuru wa nchi mbalimbali.

"Jambo la nane, Mwalimu Nyerere aliwapenda vijana na alitambua umuhimu wa kuwalea na alikuwa karibu na Umoja wa Vijana. Alitupatia fursa ya kuanza kujifunza uongozi si wa juu. Kuanzia chini, tulijifunza kusema, kutoa mawazo na kujifunza kutambua jinsi nchi inavyoendeshwa," alisema.

Jambo la tisa, alisema Mwalimu Nyerere aliamini katika meza ya mazungumzo na kutolea mfano mwaka 1988, wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) walifanya maandamano kupinga wabunge kujiongezea mishahara. Alisema katika maandamano hayo, kulisambazwa makaratasi yenye hoja ya kisiasa ya vyama huru vya siasa, vyama huru vya wafanyakazi na uhuru wa kugoma. "Kama kawaida Nyerere alikuwa akiongoza nchi na chama. Katika kikao cha Kamati Kuu (ya CCM) tulijadili tukio hili kubwa. Mwalimu alisema pamoja na hayo kulikuwa na makaratasi haya nataka msome wote halafu tutayarishe majibu.

"Tukasoma tukamaliza tukasema huu ni uhaini wakamatwe watiwe kizuizini. Mwalimu Nyerere akasema mawazo hayapigwi rungu, mawazo yanashindwa na mawazo yaliyo bora zaidi. Maadam wamejenga hizi hoja sisi hoja zetu ni zipi," alihoji.

"Nyerere ametuachia urithi wa mambo mengi muhimu. Katika nyanja zote za maisha ya Watanzania ni wajibu wetu kuutambua na kuudumisha na baadhi yake yameshakuwa tunu la taifa," alisisitiza.

Kikwete aliwataka Watanzania, viongozi wa CCM na vyama vingine vya siasa, makabila, madhehebu yote washikamane katika kusimamia tunu hizo.

# Jaji Mkuu atoa angalizo ulipaji wa fedha uhujumu

**INATOKA UK. 2**

alisema na kuongeza:

"Nchi nyingine ni tofauti sana kwa kuwa Ulaya kuna chombo cha upelelezi cha kupima ukweli kinachoonyesha anayedanganya na kusema ukweli, imepunguza upelelezi."

"Siku zote suala hili linapokuja linakutana na upinzani, maana hata Marekani walikataa na baadaye ikafanikiwa, hili jambo jema tusipoliripoti vizuri likaeleweka linaweza kuonekana siyo kitu kizuri na kujikuta inaondolewa kwa sababu ya namna ya uelewa wake," alisema.

Jaji Juma alisema sheria inazungumzia suala hilo katika mahakama zote na wote wanaohusika na Mahakama, na kwamba ni nchi nzima na siyo sehemu ndogo ya jamii.

**WANAHABARI WATUMIE SHERIA**

Kadhalika, aliwataka waandishi wa habari kutumia nguvu ya kisheria kudai taarifa kwa kuwa imewekwa kwenye sheria ya upatikanaji wa taarifa ya mwaka 2016.

"Kwa bahati mbaya hizi nguvu hazitumiki, tumebaki kuomba kama ni fadhila badala ya kutumia nguvu za kisheria kudai kwamba sheria imekupa nguvu kwa taasisi yako kupata taarifa," alisema.

Aidha, alisema sheria hiyo inatoa shuruti kwa taasisi kuwa lazima watoe taarifa zinazotakiwa na umma, na kwamba hakuna namna ya kukataa kutoa taarifa.

"Sheria ilivyotamka hivyo inaipa nguvu tamko la kikatiba, nyinyi mmepewa nguvu zaidi badala ya kutegemea zidi fadhila na kuomba...ni namna gani utatumia sheria kushurutisha ili habari zitoke," alisema Jaji Juma. Kwa mujibu wa Jaji Mkuu, watumishi wa umma wanawajibika kuhakikisha taarifa mbalimbali zinakuwapo wakati wote ili wananchi au waandishi wasipate shida kuzipata.

Jaji Mkuu alisema kuwa Mahakama inafanyakazi katika mazingira ya uwazi na kuruhusu kukosolewa kwenye hukumu zake mbalimbali, ilimradi asikosolewe Jaji.

Awali, Mwenyekiti wa Misa-Tan, Salome Kitomari, alisema ushirikiano kati ya taasisi hiyo na Mahakama ulianza baada ya utafiti wa upataji taarifa wa mwaka 2014 kwa Mahakama kupata kufuli la dhahabu kutokana na kufungia taarifa.

"Mahakama chini ya Jaji Mkuu wa wakati huo, Othman Chande, ililichukua kufuli hilo kama fursa ya kufungua uhusiano na Misa Tanzania. Kuanzia wakati huo, mafunzo ya huduma bora kwa mteja na upataji taarifa kwa watumishi wa Mahakama na hadi Mei mwaka huu watumishi 300 wa kanda tofauti wamenufaika," alisema.

Kitomari aliwataja wanufaika ni makarani, watunza kumbukumbu, watumishi wa mapokezi, makatibu mahsusi, walinzi na mahakimu wa mahakama za mwanzo na maafisa waajiri na tathmini ilionyesha kuna mabadiliko makubwa katika huduma kwa wateja.



Meneja Mauzo wa Kimataifa wa Farmers Centre na Farmbase, Dk. Jones Mushi (kulia), akitoa maelezo kwa wananchi waliotembelea banda lake, katika maonyesho yaliyoenda sambamba na mkutano wa wadau wa sekta ya mifugo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mzee asotea mafao mwanawe miaka minne

**Na Salome Kitomari**

MZEE Ismail Nguvu (75), ameliomba Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF) kulipa mafao ya mwanawe Nasibu Nguvu, aliyefariki dunia mwaka 2016.

Kijana huyo ambaye alikuwa mchangiaji kwenye mfuko wa PPF uliounganishwa na NSSF mwaka jana, alikuwa mwanachama wa mfuko huo namba 2320865 ambaye alichangia Sh. 4,874,970.72. Nasibu alikuwa mfanyakazi wa hoteli ya Holday Inn jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana jijini Dar es Salaam, alisema wameshafuatilia mara nyingi kabla ya mifuko kuunganishwa hadi inaunganishwa bila mafanikio.

Alisema mwanawe ameacha mke na watoto na walitarajia fedha hizo zitatumika kuwasomesha lakini kila siku wanapigwa danadana.

"Mwanangu unavyoniona hapa mimi ni mgonjwa, lakini hakuna mtu wa kufuatilia haki ya mwanangu. Kila nikifuatilia zilipokuwa ofisi za PPF na baadaye NSSF naambiwa faili lake lipo kwenye hatua nzuri," alisema.

"Tumefuatilia sana, tunaambiwa tusubiri hundi ambayo imetumwa kwenye akaunti ya msimamizi wa mirathi. Sasa ni miezi 15 sasa hakuna mafanikio yoyote," aliongeza.

Alisema kijana wake alichangia mfuko huo akiamini kama kutatokea tatizo lolote katika maisha yake fedha hizo zitasaidia kama ilivyotokea kifo lakini fedha zake hazijulikani zilipo na mifuko haitoi majibu sahihi.

"Miezi 15 bila mafanikio zimeliwa au amepewa mtu mwingine anayehusika au zimekopeshwa kwa watu hawajarudisha? Mimi ni baba mzazi wa marehemu umri wangu naelekea miaka 80 sasa. Naomba kujua tatizo liko wapi kwenye kuandika hundi au kuna jambo lingine?" Alihoji.

Barua kutoka Holiday Inn, yenye kumbukumbu namba EMPL/HOL/CODE.029/16, kutoka kwa Meneja Rasilimali Watu kwenda kwa familia, kuhusu kuthibitisha kifo cha kijana huyo, ilieleza kuwa kijana huyo alianza kufanya kazi Machi Mosi, 2013.

Katika barua hiyo, imeelezwa kuwa michango ya mwanachama huyo ilikuwa ikipelekwa PPF.

Ripoti ya uchangiaji kutoka PPF, ilionyesha kuwa alianza kuchangia Juni, 2013 alichangia Sh. 55,424 kiwango ambacho kiliongezeka kwa kadri mshahara ulivyoongezeka na hadi anafariki dunia alikuwa analipwa Sh. 600,000 na mchango wake kwenye mfuko ilikuwa Sh. 120,000 kwa mwezi na kufanya jumla ya michango 42.

Ripoti hiyo ilichapishwa Agosti 20, 2018 na mtumishi wa mfuko huo aitwaye Hsabaya.

Kwa mujibu wa Sheria ya Hifadhi ya Jamii, iwapo mwanachama atafariki dunia, michango yake wanapewa warithi wake na iwapo atafariki dunia baada ya kufikisha miezi 180 ya uchangiaji warithi wake watalipwa mkupuo na pensheni ya kila mwezi kwa miezi 36.

# Meneja kizimbani tuhuma ubadhirifu

**Na Ibrahim Yassin, KYELA**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) mkoani Mbeya, imempandisha kizimbani Meneja wa zamani wa Kyela FM, Maisha Ambangile, kwa makosa manne ya kujipatia pesa kwa njia za udanganyifu kutoka kwa mwajiri wake wa zamani Kyela FM. Hata hivyo baada ya kutoka mahakamani meneja huyo, alikamatwa tena na kuwekwa rumande akiendelea kuchunguzwa na bado hajapata dhamana. Alifikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Kyela mbele ya Hakimu Mkazi wa Mahakama hiyo, Mabula Barnabas.

Ilidaiwa mtuhumiwa anakabiliwa na mashtaka manne yote yakiwa ni ya kujipatia fedha kwa njia za udanganyifu mali ya mwajiri wake.

Hata hivyo, baada ya kusomewa mashtaka hayo, alikana na kesi imeahirishwa mpaka Oktoba 16, nwaka huu.

Ambangile alipelekwa rumande baada ya kushindwa kutimiza masharti ya dhamana, huku ndugu zake wakiendelea na jitihada za kumwekea dhamana.

## Uagizaji bidhaa nje kupungua

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali itaendelea kupunguza uagizaji wa baadhi ya bidhaa zinazozalishwa nje.

Badala yake amesema ununuzi wa bidhaa zinazozalishwa ndani utaongezwa ili kukuza viwanda vya ndani hususan bidhaa za mbao na mafuta ya kula.

"Napenda kuwahakikishia kuwa, bidhaa zetu ni nzuri na zinapendwa na watu wengi hata wa nje ya nchi. Mnachotakiwa kukifanya ni kuzalisha bidhaa kwa wingi na kwa kutumia malighafi zinazopatikana kwenye maeneo yenu, hii itawezesha kuwa na uzalishaji wenye gharama ndogo na kuwa na bei shindani katika soko."

Waziri Mkuu ameyasema hayo juzi wakati akifungua Maonyesho ya Shirika la Viwanda Vidogo (Sido) kitaifa yanayofanyika katika viwanja vya Bomberdia Manispaa ya Singida.

Alisema serikali itaendelea kujenga mazingira mazuri ya kuwa na viwanda vya kuongeza thamani ya madini nchini.

"Niwasihi Watanzania wote hasa wale wanaofikiria kuwa bidhaa zinazotoka nje ya nchi ndizo zenye ubora kuliko za hapa nchini, kuachana na dhana hiyo potofu, kwani bidhaa zetu ni bora na zina viwango vinavyostahili."

Alisema wakizalisha bidhaa kwa kutumia malighafi za ndani itawezesha ajira endelevu kuwapo kwa vijana, itasaidia malighafi kutoharibika lakini bidhaa zitakazozalishwa zitakuwa na thamani kubwa badala ya kuuza malighafi kwa bei ya chini.

Pia Waziri Mkuu alisema serikali imedhamiria kujenga uchumi wa viwanda ili kuifikisha nchi kwenye kipato cha kati ifikapo mwaka 2025.

Alisema uanzishwaji wa viwanda umejikita zaidi katika uongezaji wa thamani wa mazao ya kilimo na maliasili yanayopatikana nchini, kama kilimo, mifugo, misitu, uvuvi na madini kwani wananchi wengi wanategemea mazao na rasilimali hizo kwa maisha yao.

Waziri Mkuu alisema serikali itaendelea kuhimiza uongezaji thamani wa mazao husika kwa kuwa ndiyo njia sahihi. "Kwa misingi hiyo, usindikaji, uchakataji na uchenjuaji, vitachangia kupunguza upotevu unaotokea msimu wa mavuno, kuongeza ajira na thamani ya mazao kwa lengo la kuwapatia wazalishaji kipato."

Alisema uongezaji thamani utahitaji teknolojia (mashine na ujuzi), ambapo baadhi ya teknolojia hizo zimeonyeshwa kwenye maonyesho hayo.

"Vilevile maonyesho hayo yametoa fursa ya kuonyesha teknolojia zinazoweza kurahisisha uzalishaji na kuleta ufanisi zaidi ili kuongeza tija na kuhimili ushindani katika soko la ndani na nje."

Mapema akitoa taarifa kuhusu maonyesho hayo, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa SIDO, Prof. Elifas Bisanda, alisema wamekuwa wakiandaa maonyesho hayo ili kuwahamasisha wajasiriamali wadogo na wa kati wapate mbinu mpya juu ya viwanda vidogo.

# Mamlaka yapatiwa bil. 330/- za maji

Na Said Hamdani, LINDI

SERIKALI imeipatia Mamlaka ya Majisafi na Salama Wilaya ya Lindi Jumla ya Sh. 330,000,000 kwa ajili ya kuboresha miundombinu, ikiwamo kujenga vituo vipya ili kutatua tatizo la upatikanaji wa huduma hiyo.

Wananchi waliokuwa wakikabiliwa na tatizo hilo ni wa Kata ya Rutamba.

Tamko la serikali, lilitolewa na Waziri wa Maji, Prof. Makame Mbarawa, alipozungumza na wakazi wa kata hiyo pamoja na uongozi wa jumuiya ya watumia maji, alipofanya ziara ya kukagua na kusikiliza matatizo yanayowakabili wananchi wa mkoa wa Lindi.

Waziri Mbarawa alitoa fedha hizo kufuatia maelezo kutoka kwa Katibu wa Jumuiya ya Watumiaji Maji wa Kata ya Rutamba, Kasimir Mponda, aliposema upungufu wa ukusanyaji maduhuri yanachangiwa na baadhi ya wateja wake kutokubali kulipia kwa kile kilichoelezwa ni kutopata huduma hiyo kutokana na uchakavu wa miundombinu yake.

Mponda alisema Kata ya Rutamba yenye wanachama watumiaji maji 2,000, anakusanya maduhuri sio zaidi ya Sh. 350,000 kwa mwezi kutokana na uchakavu wa miundombinu iliyopo. "Kata yetu ina watumia maji 2,000 na kwa mwezi, kila mmoja anapaswa kulipia Sh. 1,000, lakini baadhi yao hawataki kulipa wanadai maji hawapati, walipeje," alisema Mponda.

Alisema iwapo kaya zote 2,000 zingekuwa zinalipia huduma ya maji, wangekusanya Sh. 2,000,000 kila mwezi, lakini inashindikana kutokana na uchakavu.

Mkuu wa Wilaya ya Lindi, Shaibu Ndemanga, alisema awali kata hiyo ilikuwa inakaliwa na wakimbizi kutoka Msumbiji na walikuwa wakitumia huduma hiyo bila malipo, hivyo ipo haja ya kuwapatia elimu ili waweze kulipia.

Waziri Mbarawa akizungumza na baadhi ya wananchi na uongozi wa Jumuiya ya watumia maji, Prof. Mbarawa aliwataka wakazi hao kulipia matumizi ya maji kwa fedha zinazokusanywa zitasaidia kufanyia matengenezo chombo kinapoharibika.

Aidha, Prof. Mbarawa alisema fedha hizo zitatumika kuboresha miundombinu, kulifanyia matengenezo tangi la kuhifadhia maji la kata hiyo na kujenga vituo vingine vipya.

Aliagiza fedha watakazopelekewa zitumike kukarabati tangi la maji, ujenzi wa matangi mengine matatu, kukarabati vituo 12 na kujenga vingine sita ili kuwaondolea wananchi tatizo la upatikanaji wa huduma hiyo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Ruwasa, Idd Pazzy, alisema utekelezaji wa kazi hiyo zinahitajika Sh. 330,000,000 ambazo Waziri ameahidi kuzipeleka mwezi huu.



Naibu Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Sekondari St. Francis ya Kongwa, katika mahafali ya nane ya shule hiyo, wilayani Kongwa mkoani Dodoma juzi

# Waziri atembelea kiwanda bila kukuta wafanyakazi

Na Mwandishi Wetu

NAIBU Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, amefanya ziara ya kushtukiza katika kiwanda cha nyuzi Tabotex mkoani Tabora na kukuta hakina wafanyakazi.

Wafanyakazi hao walimkimbia msimamizi wa kiwanda hicho, na kumsababisha ashtuke mbele ya Naibu Waziri na Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri.

Video fupi inayoonyesha namna msimamizi wa kiwanda hicho, alivyoshtuka baada ya kujikuta yupo peke yake, mbele ya viongozi hao, ilianza kusambaa juzi kwenye mitandao ya kijamii.

Katika ziara hiyo, Bashe alikuta uzalishaji duni wa nyuzi tani 6,200 kwa mwaka, tofauti na malengo ya kiwanda hicho, huku mwekezaje naye akisusua katika uendeshaji.

Bashe alilazimika kuanza kumuhoji msimamizi wa kiwanda hicho, ambaye alianza kujiuma uma huku akiwa hana uhakika na kile anachokijibu.

"Kwa mwaka tunazalisha tani 6,200 za uzi na 'input' (pembejeo) tani 100 hadi 200 kwa mwezi," alijibu huku akitafuta wenzake wamsaidie.

"Niko peke yangu hapa.... kumbe wenzangu wamenikimbia."

Alipoulizwa kama kuna wafanyakazi alisema wapo 180 na wanapokezana kuingia kazini watu 60 kwa zamu tatu.

Alisema pia wanafanya mazungumzo na wawekezaji wa sekta binafsi kwa ajili ya kushirikiana na kiwanda hicho katika uzalishaji.

Alipoulizwa sababu za kutozalisha licha ya kuwapo kwa miundombinu na pembejeo kupatikana, hakuwa na jibu.

Naye Mwanri alisema miaka minne iliyopita, mwekezaji huo alishaahidi kumtafuta mwekezaji raia wa China ambaye atawekeza Dola za Marekani milioni 500.

Alisema alishaomba reli ijengwe kufika eneo hilo la kiwanda kwa ajili ya kurahisisha usafirishaji wa bidhaa zinazozalishwa na kiwanda hicho.

# Waliosoma China kuzindua Saccos

Na Mwandishi Wetu

JUMUIYA ya Watanzania waliosoma China (CAAT) imeandaa mkutano wa kimkakati jijini Dar es Salaam kuwakutanisha wasomi wote waliosoma China kujadili fursa zilizopo kati ya nchi hizo mbili na kuzindua chama cha kuweka na kukopa (Saccos).

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Mwenyekiti wa CAAT, Dk. Liggyle Vumilia, alisema mkutano huo wa Ijumaa, utatengeneza mtandao utakaochagiza maendeleo nchini sambamba na azma ya serikali kujenga uchumi wa kati na viwanda ifikapo 2025.

"Tungependa kuona vijana wengi hasa wale ambao wamehitimu masomo yao China, washiriki katika mkutano huu muhimu kwani ni nafasi ya pekee kwao kuona namna wasomi wenzao waliosoma huko wanavyopambana kujiendeleza kiuchumi na kushiriki katika shughuli mbalimbali za kimaendeleo wakiwa kama viongozi na hata wafanyabiashara," alisema Dk. Vumilia. Alisema Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Idd, ambaye ni mlezi wa jumuiya hiyo, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika mkutano huo wa siku moja.

"Balozi Seif amewahi kuwa Balozi wa Tanzania nchini China miaka ya nyuma ambapo ataambatana na Balozi wa China nchini, Wang Ke, katika ufunguzi huo," alisema. Alisema pia watakaoshiriki ni Waziri Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angela Kairuki, Balozi mstaafu Abdulrahaman Shimbo, Dk. Maua Daftari na wengine wengi ambao pia waliwahi kusoma na kufuzu masomo yao China. Mkutano huu pia utawashirikisha wadau mbalimbali wakiwamo wawekezaji, Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Shirikisho la wenye Viwanda Tanzania (CTI) ili kuweza kujadiliana namna bora ya kuchangia shughuli za maendeleo na uchumi.

"Kutakuwa na ushiriki wa maofisa watendaji wakuu kutoka benki mbalimbali hapa nchini kama CRDB na NMB yenye Dawati la Uchina na wa kampuni kubwa za China zinazofanya shughuli ya ujenzi Tanzania pamoja na wafanyabiashara wakubwa kutoka China," alisisitiza.

Alisema mada mbalimbali za kimkakati zitawasilishwa na kujadililiwa na washiriki. Tanzania ni moja ya marafiki asilia wa Serikali ya China, Taifa lenye uchumi mkubwa duniani. Pamoja na uzinduzi wa Saccos ya jumuiya hiyo itakayowawezesha wanachama kuweka na kukopa fedha kwa riba nafuu, Dk. Vumilia alisema siku hiyo pia itatumika kufungua Jumuiya ya Wanawake itakayohamasisha ushiriki wa wanawake katika sekta mbalimbali za uchumi.

# Shule kuanzisha mfuko kusaidia wanafunzi

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

MKUU wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, amezishauri shule mbalimbali kuanzisha mfuko maalumu kwa ajili ya kusaidia watoto waishio mazingira hatarishi ili waweze kuendelea na masomo yao na kutimiza malengo yao waliyojiwekea.

Aliyasema hayo jana, wakati akizungumza katika mahafali ya 15 ya wanafunzi wa darasa la saba katika shule ya mchepuo wa Kiingereza ya Engarenarok Lutheran Tetra, iliyopo mjini hapa ambayo jumla ya wanafunzi 52 wamehitimu masomo yao.

Muro alisema, uwapo wa mfuko huo katika shule mbalimbali utasaidia kuwezesha watoto hao kupata elimu kwa urahisi kupitia mfuko huo.

Alisema, kumekuwapo na changamoto kubwa ya watoto hao kukosa elimu kutokana na ukosefu wa fedha kwa familia wanazotoka, huku wanafunzi wengine wakikutana na matatizo hayo baada ya kufiwa na wazazi wakiwa shuleni, hivyo uwepo wa mfuko huo utawasaidia watoto hao kuendelea na masomo yao kama kawaida.

"Nimeona shule hii wameweza kuanzisha mfuko maalumu kwa ajili ya kuwasaidia watoto kupata elimu baada ya kukumbana na matatizo mbalimbali wakiwa shuleni, kwa kweli utaratibu huu ni mzuri sana na unapaswa kuigwa na shule zingine kwa ajili ya kuwasaidia watoto hao kuendelea na masomo kama wengine," alisema Muro.

Aliwataka wanafunzi waliohitimu, kuendelea kujiwekea malengo yao ya baadaye kwa kujiepusha na makundi yasiyofaa pindi wanapokuwa mtaani wakisubiri matokeo yao, badala yake watumie muda huo kujiunga na kozi fuji zitakazowasaidia baadaye.

Aliwataka wazazi, walezi pamoja na wanafunzi kuendelea kuchangamkia fursa ya uwapo wa elimu bure inayotolewa na serikali ya awamu ya tano ili kupata fursa ya kila mtoto kunufaika na elimu hiyo kama yalivyo malengo ya serikali kuhakikisha kila mtoto anapata elimu.

Naye Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Jenifa Mollel, alisema shule hiyo ilianzishwa mwaka 1998 na wamekuwa wakifundisha watoto hao kujiajiri pindi wanapohitimu masomo yao kwa kuwafundisha masomo ya ujasiriamali.

Alisema kuwa, shule hiyo ilianzisha mfuko wa kusaidia watoto yatima baada ya wanafunzi watatu kufiwa na wazazi wao waliokuwa wanawategemea na hivyo wakafikia hatua ya kuanzisha mfuko huo baada ya kuona ulipaji ada ukisuasua.

Jenifa alisema, walimu wa shule hiyo wamekuwa wakijichanga fedha zao kwa ajili ya kusaidia watoto hao na alizitaka shule mbalimbali kuanzisha mfuko maalumu utakaowasaidia watoto waishio mazingira hatarishi ili waweze kutimiza ndoto zao kama ilivyo kwa watoto wengine.



Mwenyekiti wa Bodi ya Kiwanda cha Happy Sausage, Andrew Mollel (wa tatu kulia), akitoa maelezo kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo na Mifugo, Prof. Elisante ole Gabriel (aliyeshika nyama), jinsi wanavyochambua nyama kwa ajili ya kutengeneza "sausage", alipotembelea kiwandani hapo, mkoani Arusha juzi. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Halmashauri yatenga mil. 71/- kuboresha lishe

**Na Jaliwason Jasson,**
MANYARA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Babati mkoani Manyara imetenga Sh. milioni 71.136 katika mwaka wa fedha 2018/2019 ili kuokoa watoto walioko kwenye hatari ya kupata udumavu.

Ofisa Lishe wa Halmashauri hiyo, Bernadetha Tembo, alisema hayo wakati akizungumza na Nipashe kuhusu bajeti inayotengwa kwa ajili ya kitengo cha lishe chenye dhamana ya kusaidia watoto ili wasipate magonjwa ya udumavu na utapiamlo.

Alisema walianza kutenga bajeti hiyo baada ya kupata mwongozo kutoka Wizara ya Afya na walitakiwa kutenga fedha hiyo kwa ajili ya kusaidia watoto walioko chini ya miaka mitano na mwongozo huo ulikuja mwaka 2017.

Bernadetha alisema, baada ya mwongozo kufika halmashauri hiyo ilitenga Sh. milioni 71.136 kwa mwaka wa fedha 2018/2019, lakini Sh. milioni 11.127 ndizo zilitumika kwa ajili ya kazi mbalimbali ikiwamo chanjo ya vitamini A kwenye maadhimisho ya Wiki ya Unyonyeshaji na fedha nyingine ilitumika kuwatibu watoto waliopata ugonjwa wa utapiamlo.

"Mfano tulikuwa na watoto 42 waliopata utapiamlo mwaka 2018/2019, hivyo tulitumia fedha nyingine kutembelea kaya zilizokuwa na watoto wenye ugonjwa huo na kuwapatia elimu na vyakula vya kusaidia kuongeza lishe," alisema.

Bernadetha alisema baada ya kupokea mwongozo kutoka wizarani walitakiwa kama halmashauri kuwatengea kila kichwa cha mtoto Sh. 1,000 kwa ajili ya kusaidia kutoa elimu ya lishe vijijini wakisaidiana na watoa huduma wa afya waliotambuliwa.

Katika kuhakikisha elimu ya lishe inawafikia wananchi vijijini, aliagiza vijiji vyote 102 vya halmashauri hiyo kuwateua wahudumu wawili wa kike na kiume ili wasaidie kubaini watoto wenye shida ya kiafya hasa wenye udumavu au utapiamlo na kuwabaini wajawazito ili waweze kuwasaidia kuwapa elimu ya kwenda kliniki kwa ajili ya ushauri wa vyakula vya kutumia ili wasipate watoto wenye matatizo ya kiafya yanayosababishwa na kukosa lishe.

Waziri Mkuu, Kassimu Majaliwa, akifungua mkutano wa wadau wa lishe jijini Dodoma Oktoba 3, mwaka huu, aliwataka viongozi wa ngazi za mikoa na halmashauri zote nchini kuhakikisha hatua za mpango jumuishi wa taifa wa lishe zinajumuishwa katika mipango na bajeti kila mwaka na kutoa fedha hizo kwa ajili ya utekelezaji.

Naye Martha John, mkazi wa Babati alisema licha ya halmashauri kutenga fedha hizo, wanatakiwa kujikita kwenye utoaji wa elimu kwa wananchi hasa wa vijijini.

Kwa upande wake, Jackline Sanka wa Dareda, alishauri serikali kuwatumia wataalamu wa kilimo kusimamia kupandwa kwa mazao ya kusaidia kuongeza lishe na kutoa mwongozo wa mazao hayo kutouzwa kwa bei kubwa ili kila mtu aweze.

# Vijana wapewa mbinu kujiajiri, kuajiri

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

VIJANA wametakiwa kuongeza ujuzi na kuwa wajasiriamali ili waweze kujiajiri na kuajiri wengine baada ya vijana 800,000 kukosa ajira kila mwaka nchini.

Kauli hiyo ilitolewa mjini hapa jana na Mkurugenzi wa Fedha na Utawala, Joshua Silayo wa Asasi ya Anza, inayojishughulisha na ufundishaji vijana masuala ya ujasiriamali na kuboresha mawazo ya biashara.

Changamoto hiyo imeisukuma Anza na Asasi ya Climate Launch Pad kuendesha shindano kwa vijana 10 ili kupata mawazo bora ya biashara zinazo lenga kutunza mazingira yatakayoshindanishwa kidunia.

Akizungumza wakati wa kutafuta washindi watatu kati ya 10 walioshiriki mafunzo ya masoko, fedha na wateja kwa miezi miwili, Silayo aliyataja malengo yao kuwa ni kukuza ajira tano mpaka 10 kwa kila biashara.

"Tunalenga kukuza mapato ya vijana ili wakidhi mahitaji yao na jamii inayowazunguka, kuendeleza elimu kwa vijana wengine na kukuza jamii ya kijasiriamali kwani kila mwaka vijana 800,000 hukosa ajira," alisema na kuongeza:

"Mwaka jana katika mashindano kama haya kidunia tulipata biashara iliyoshinda Euro 2,500 kwa wazo la biashara kijani. Vijana washiriki mashidano haya ili kukuza biashara zao," alisema Silayo.

Alisema washindi watatu watakaopatikana watakwenda kushiriki mashindano ya kidunia nchini Amsterdam na wazo la biashara litakaloshinda litapata Euro 10,000, wa pili 5,000 na wa tatu Euro 2500," alisema Silayo.

Kwa upande wake Jaji Kiongozi wa shindano hilo ambaye ni Mchumi na Mtafiti Mapolu John, alisema wameangalia ujuzi wa vijana hao na wanautumia vipi katika maisha ya kila siku hasa biashara zinazotunza mazingira.

"Vijana wamefanya vizuri, lakini walio wengi wana elimu ya kitabuni na wanakosa utafiti mkubwa katika masuala ya takwimu wanalinganisha takwimu zilizopitwa wakati," alisema.

"Hawajui masoko, baadhi wameshindwa kuoanisha biashara anayofanya, masoko, sera na sheria za nchi," alisema Mapolu.

Akifafanua kuhusu suala la mitaala shuleni, Mapolu alisema ni wakati mwafaka kwa mitaala ya shule na vyuo vya serikali na binafsi kuanza kufundisha ujasiriamali kwa kuwa una kitu kikubwa.

"Vijana wengi hawana ajira na kuwasomesha shule ya vyeti inakuwa haina mpapaso mkubwa kwenye uchumi," alisema Mapolu.

Pia alisema mitaala ikianza kubadilika na wanafunzi kufundishwa namna ya biashara kuandika miradi, kutunza vitabu, kulipa kodi na faida zake inaweza kuwa ukurasa mpya katika eneo la ajira.

# Matumaini kushuka ukatili kijinsia

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

RIPOTI ya 11 ya utekelezaji wa mradi wa ushirika wa huduma endelevu za msaada wa kisheria katika mkoa wa Kilimanjaro, imeonyesha njia ya kuwapo kwa matumaini makubwa ya kushuka kwa takwimu za matukio ya ukatili wa kijinsia, baada ya wananchi kuanza kuelewa umuhimu wa kuwatumia wasaidizi wa kisheria.

Jana katika kikao cha siku moja cha wadau kilichoandaliwa na Shirika la kiraia la Kwieco, kwa ufadhili wa Legal Service Facility (LSF), Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Manispaa ya Moshi na Mratibu wa Dawati la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi, Sapiencia Mugarula, alisema yapo matokeo chanya yanayoonekana wazi kutokana na juhudi kubwa iliyofanywa na wasaidizi hao, kati ya mwezi Julai hadi Septemba mwaka huu. "Ukiangalia taarifa za utekelezaji wa robo iliyoisha (Julai hadi Septemba), utaona kesi ambazo zimeripotiwa katika kata 21 za Manispaa ya Moshi kupitia kwa wasaidizi wa kisheria, zinatia moyo kwamba wananchi wanaelewa sasa waanzie wapi kusaidiwa utatuzi wa matatizo yanayowakabili kama matunzo ya watoto, ukatili wa kijinsia, wanawake kunyang'anywa ardhi na kadhalika," alisema Mugarula.

Wakati Ofisa wa Polisi, Koplo Oscar Magege, ameeleza kuwa dawati la malalamiko la jeshi hilo limekuwa likipokea taarifa nyingi za ukatili zinazotolewa na wasaidizi hao wa kisheria, zikiwa na ushahidi wa kutosha wa kufikisha baadhi ya kesi mahakamani.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Shirika la Wasaidizi wa Kisheria Moshi Mjini (Washemom), Shaban Mkwizu, alisema wasaidizi wa kisheria wamefanikiwa kuisambaratisha ndoa feki nyingi ikiwamo inayodaiwa kuwa ya mtu na kaka yake wa kuzaliwa katika Mtaa wa Matindigani, Kata ya Pasua, baada ya mke halali wa ndoa kufukuzwa yeye na wanawe wawili.

Kwa mujibu wa Mkwizu, umuhimu wao ulijulikana vyema na wananchi, baada ya kufanikiwa kumsaidia mama huyo wa watoto wawili aliyefukuzwa na mumewe (jina limehifadhiwa), kurejea tena katika ndoa yake baada ya kujifungua mtoto wa pili.

Akifungua kikao hicho, Ofisa Mwandamizi wa Kitengo cha Ufuatiliaji, Tathimini na Taarifa wa Kwieco ambalo ni walezi wa wasaidizi hao wa kisheria, Peter Mashingia alisema wameamua kukutana na wadau mbalimbali ili kushirikishana taarifa za utekelezaji wa mradi huo.

Wadau hao ni polisi dawati, maofisa maendeleo ya jamii, wanawake mashuhuri, wasaidizi wa kisheria, viongozi wa dini, viongozi wa mila na waandishi wa habari.

"Tulikuwa tunaangalia nini kilichofanyika kama kuna mafanikio, changamoto na kuweka mikakati ya pamoja ili kuweza kutoa huduma ya msaada wa kisheria, kuendelea kuelimisha jamii kuhusu haki zao, masuala ya jinsia, lakini suala la ulinzi na usalama wa watoto katika jamii," alieleza Mashingia.

Mradi huo unatekelezwa katika halmashauri zote saba za mkoa wa Kilimanjaro na watekelezaji wakubwa ni wasaidizi wa kisheria.




Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai, Yohana Sintoo, akikinga maziwa yanayouzwa kwenye mashine maalum kwa njia ya kadi ya ATM, zilizofungwa wilayani humo, mkoani Kilimanjaro juzi. Serikali imezindua ATM ya kwanza ya maziwa wilayani humo. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Mwarobaini uharibifu wa tembo wapatikana

**Na Godfrey Mushi,** SAME

TATIZO la tembo kuvamia mara kwa mara makazi ya watu na kuharibu mazao ya chakula katika Wilaya ya Same mkoani Kilimanjaro, hatimaye limepata mwarobaini, baada ya Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (Tawiri) kuanza kuchukua hatua ya kuwadhibiti.

Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule, amethibitisha kupokea timu ya wataalamu wa taasisi hiyo kutoka Kanda ya Kaskazini chini ya Dk. Edward Kohi ambao wamekwenda moja kwa moja katika Kata za Vumari na Kisiwani kujionea maeneo yanayoathirika zaidi.

"Ni kweli wamekuja hao watu wa Tawiri, kutatua kero ya mwingiliano wa wanyamapori hasa tembo na binadamu katika maeneo hayo. Kuna uharibifu mkubwa wa mazao, mali na hofu ya tembo kuendelea kuvamia makazi ya watu na kuzua taharuki, ndio maana serikali ikaamua kuwaleta ili kutafuta ufumbuzi wa kudumu," alisema Senyamule.

Wataalamu hao walikuwa wameongozana na Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Kilimanjaro, Patrick Boisafi na Mkurugenzi wa Tume ya Taifa ya Mipango ya Ardhi (NLUPC), Dk. Stephen Nindi.

Baadhi ya wananchi wa Kata ya Vumari, Asia Sefue na Hamdan Saweji kwa nyakati tofauti, wakitoa maelezo kuhusu tembo hao kwa maofisa wa Tawiri, wametaka kuwapo kwa mpango mkakati wa kudhibiti wanyamapori wanaovamia vijiji na kuharibu mazao, huku wakitishia maisha ya wananchi.

Kwa mujibu wa Sefue, kuna wimbi kubwa la makundi makubwa ya wanyama hao kuingia na kuvamia maeneo ya makazi na mashamba ya wananchi kila wakati. Tembo hao wanadaiwa kuingia kwa makundi na kuvamia mashamba, nyumba na maghala ya akiba za vyakula vya aina mbalimbali hasa nafaka kama mahindi mtama na viazi vitamu.

Mazao mengine yanayovamiwa mashambani au bustanini ni miwa, maboga, matikiti maji, matango na bustani zilizoko kandokando ya mito. Tawiri ilianzishwa kwa Sheria Sura 260 kwa lengo la kusimamia, kufanya na kuratibu utafiti wa wanyamapori nchini.

Taasisi hiyo ina wajibu wa kutoa ushauri kuhusu uhifadhi endelevu wa wanyamapori kwa kutumia matokeo ya utafiti wa kisayansi.

Aidha, Tawiri ina wajibu wa kufanya sensa ya makundi mbalimbali ya wanyamapori ili kushauri wahifadhi na serikali.

## Maadhimisho ya ushirika leo

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MAADHIMISHO ya Siku ya Kimataifa ya Ushirika wa Akiba na Mikopo nchini (Saccos) yanafanyika leo jijini Arusha.

Kaimu Mrajis Mkuu wa Vyama vya Ushirika, Tito Haule ndiye atakayefungua maadhimisho hayo kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mwenyekiti wa Bodi ya Chama Kikuu cha Ushirika wa Akiba na Mikopo Tanzania (SCCULT Ltd-1992), Dk. Gervas Machimu.

Kwa mujibu wa Dk. Machimu, awali mkutano huo ulikuwa ufunguliwe jana, lakini kutokana na sababu zilizo nje ya uwezo wao, Kaimu Mrajis wa Vyama vya Ushirika nchini, Tito Haule, amethibitisha atafungua mkutano huo leo.

Vyama hivyo pamoja na mambo mengine vitatafakari na kushirikishana namna bora ya kufanikisha adhima ya utoaji wa huduma rafiki na jumuishi za kifedha kwa Watanzania.

Alisema zaidi ya vyama 200 vya ushirika wa akiba na mikopo nchini, vimejiandikisha kushiriki ili kupata uzoefu wa kubadilisha maisha ya watu na kufanikisha ndoto za wananchi na hasa wenye kipato cha chini ndani ya jamii ya Watanzania.

"Kwa sababu nia yao ni kuwainua kiuchumi, vinataka kuwahakikishia Watanzania kipato endelevu kitakachowawezesha kumudu gharama za maisha," alieleza.

Aidha, alisema maadhimisho hayo kwa Tanzania yametangulia kufanyika ili kutoa fursa kwa Saccos za Tanzania kuungana na Saccos nyingine za Afrika katika maadhimisho yatakayofanyika Mombasa, Kenya.

Kauli mbiu ya mwaka huu ni iliyotolewa na Baraza la Vyama vya Akiba na Mikopo Ulimwenguni ni 'huduma kwa kijamii, kuufikia ulimwengu'.



Ukurasa 18

**Jasusi wa Marekani aliyevujisha siri ya nyuklia kwa Urusi**

## Fungamano dhidi ya Iran lafifia



Ukurasa 20


# siasa

JUMATANO OKTOBA 9, 2019

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU




Ukurasa 14

**Magufuli na harakati za ukombozi wa pili**

# AJENDA YA MWANAMKE TURUFU YA USHINDI UCHAGUZI 2019/20120

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

USHIRIKI wa Wanawake katika nafasi mbalimbali za maamuzi hususani kisiasa bado ni mdogo, hali ambayo inakinzana na azma ya kujenga jamii isiyokuwa na ubaguzi kama ilivyobainishwa kwenye dira ya Taifa 2025.

Dira hiyo imehimiza usawa kwenye mgawanyo wa madaraka, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977 pamoja na sheria mbalimbali za nchi.

Taasisi ya Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) kwa kushirikiana na Asasi mbalimbali za kupigania haki za wanawake nchini ikiwamo Mtandao wa Wanawake na Katiba, Women Fund Tanzania, zimeandaa Ilani ya Uchaguzi ya Wanawake katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2019 na Uchaguzi Mkuu wa Tanzania 2020.

Ilani ya Uchaguzi ya Wanawake ambayo ilizinduliwa Septemba 27 mwaka huu wakati wa kilele cha Maadhimisho ya Tamasha la 14

**INAENDELEA UK.16**



Ukurasa 15

**Nigeria ilivyofufua uhusiano na taifa la Afrika Kusini**



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) Selemani Jafo. **PICHA: MTANDAO**

**IMF mbioni kurejesha msaada wa fedha DRC** Ukurasa 17

# Magufuli na harakati za ukombozi wa pili



Rais John Magufuli (katikati) wakati akizindua ujenzi wa mradi wa kufua umeme wa Stieglers Gorge kwenye mto Rufiji Julai 26, mwaka huu. **PICHA: MTANDAO**

**Na Reubeni Lumbagala**

DESEMBA 9, 1961, Tanzania ilipata uhuru wake kutoka katika mikono ya wakoloni.

Huu ulikuwa ni ukombozi wa kwanza wa kisasa ambao ulileta furaha na matumaini mapya kwa Watanganyika walioishi kwa miaka mingi katika utumwa na manyanyaso kutoka kwa wakoloni.

Baada ya Tanzania kutoka katika minyororo ya ukoloni na kupata ukombozi wa kwanza, jitihada za kuleta ukombozi wa kiuchumi (ukombozi wa pili) zilichukua nafasi yake.

Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Jemadari wa vita vya uchumi Rais John Magufuli imepania kwa vitendo kuhakikisha mapambano ya ukombozi wa pili wa kiuchumi yanafanikiwa kwani ndiyo malengo na dira ya nchi katika kuleta ustawi na ukuaji wa maendeleo ya kweli.

**DIRA YA MAENDELEO YA UCHUMI WA VIWANDA**

Rais Magufuli amesimama imara katika kuhakikisha dira ya maendeleo ya nchi yetu ya kuifanya Tanzania kuwa nchi ya viwanda na ya uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025 inafanikiwa.

> “Kumekuwa na kasi kubwa ya ujenzi wa miundombinu hii kote nchini ili kuchochea maendeleo ya kiuchumi.

Ndiyo maana serikali ikaweka mazingira mazuri kwa ajili ya wawekezaji wa ndani na wa nje ya nchi kuwekeza nchini kwa kujenga na kuendeleza viwanda vikubwa, vya kati na vidogo ili kufikia dira hii. Ujenzi wa viwanda zaidi ya 3000 kote nchini umefanyika ambapo vijana wengi wamepata ajira za kudumu na za muda, hali iliyoboresha maisha ya vijana hao.

Wakulima na wafugaji wadogo na wakubwa wameweza kupata masoko kwa ajili ya kuuza mazao yao ambayo hutumika kama malighafi za kulisha viwanda hivyo.

Hii imesaidia kukuza sekta ya kilimo na mifugo kwa kiwango kikubwa. Pia, serikali imeweza kukusanya kodi kupitia viwanda hivi, hali inayochagiza ongezeko la mapato ya nchi na hivyo mapato hayo kutumika katika ukuzaji wa sekta nyingine kama elimu, nishati, afya, maji, miundombinu, mawasiliano, kilimo nk.

Mwelekeo wa kuifikisha Tanzania katika nchi ya viwanda na ya uchumi wa kati unaenda vizuri, na hakika tutafika kama nchi.

**UBORESHAJI MIUNDOMBINU YA USAFIRISHAJI**

Ukombozi wa pili wa kiuchumi unakwenda sambamba na ujenzi na uboreshaji wa miundombinu ya barabara, reli, madaraja na viwanja.

Kumekuwa na kasi kubwa ya ujenzi wa miundombinu hii kote nchini ili kuchochea maendeleo ya kiuchumi.

Wakulima, wafanyabiashara na wajasiriamali wamewekewa mazingira rafiki kwa ajili ya usafirishaji wa mazao na bidhaa zao ili kupunguza gharama kubwa za usafirishaji.

Wakala wa Barabara nchini (Tanroads) na Wakala wa Barabara za vijijini (Tarura) wanafanya kazi kubwa katika usimamizi wa ujenzi na uboreshaji wa barabara.

Aidha, ujenzi wa reli ya mwendo kasi (SGR) unaendelea ambapo wananchi wa mikoa ya Dar es Salaam na Morogoro wataweza kusafiri kwa urahisi na kuokoa muda wa safari.

Pia, reli katika mikoa ya Tanga-Kilimanjaro imekamilika ambapo wafanyabiashara wanaweza kusafirisha bidhaa zao kwa bei nafuu.

Ujenzi wa meli katika mikoa ya kanda ya ziwa na maeneo mengine ya nchi yetu unaendelea ili kuwarahisishia wananchi usafiri huo.

Usafiri wa anga nao umeboreshwa kwa kiwango kikubwa, ambapo serikali imeboresha na kujenga viwanja vingi vya ndege katika mikoa mbalimbali.

Aidha, serikali imenunua ndege kwa ajili ya kuwahudumia abiria wa ndani na wa nje ya nchi katika safari zao za kikazi, kibiashara, kiutalii na za kimapumziko.

Mapato yanayopatikana katika usafiri wa anga unachangia ukuaji wa uchumi na hatimaye kuchagiza ukombozi wa pili.

**MRADI WA UMEME WA JULIUS NYERERE**

Kutokana na ongezeko la mahitaji ya nishati ya umeme katika kuendesha shughuli mbalimbali za kijamii na za kiuchumi, Rais Magufuli aliamua kutimiza ndoto za Mwalimu Nyerere za kujenga Bwawa kubwa kwa ajili ya kufua umeme wa maji katika Mto Rufiji.

Mradi huu utagharimu dola za Marekani bilioni 2.9 sawa na shilingi trilioni 6.5 za Kitanzania na kufanikisha uzalishaji wa Megawati 2115.

Megawati 2115 ni kiasi kikubwa kuliko kinachotumika sasa kwa nchi nzima.

Umeme huu utamaliza kabisa mahitaji ya nishati ya umeme. Kama hiyo haitoshi, kukamilika kwa mradi huu kutaiwezesha Tanzania kuuza umeme kwa Watanzania kwa bei nafuu na kuziuzia nchi nyingine.

Hivyo basi, mradi huu ni utekelezaji wa dira ya maendeleo ya kuhakikisha shughuli za kiuchumi hasa za viwandani na huduma nyingine za kijamii kama afya na elimu zinapata nishati ya umeme ili kuongeza uzalishaji.

**KUONGEZA MAKUSANYO NA MATUMIZI BORA YA MAPATO**

Ili kufikia maendeleo na ukombozi wa kiuchumi, ni lazima kodi ikusanywe kutoka kwa wananchi.

Tangu serikali ya Awamu ya Tano iingie madarakani, kumekuwa na ongezeko la makusanyo ya kodi kutoka sh. bilioni 800 hadi trilioni 1.43.

Mafanikio haya yametokana na nia njema ya Rais Magufuli katika kuhakikisha kodi inakusanywa na kutumika katika uwekezaji wa miradi mikubwa na midogo ya maendeleo kwa ajili ya ustawi wa wananchi na nchi kwa ujumla wake.

Kutokana na mafanikio ya makusanyo ya kodi, serikali imeongeza uwezo wake wa utekelezaji wa shughuli za kimaendeleo.

Ukombozi wa pili wa kiuchumi ndiyo ajenda ambayo wananchi wanaitaka kuisikia na kuona serikali yao ikiisimamia kwa vitendo kwani ni katika ukombozi huu ndipo yalipo maendeleo ya kweli ambayo yanawagusa wananchi moja kwa moja. Tafakari.

***Mwandishi ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.***

***Maoni: (+255) 764 666349***

# Nigeria ilivyofufua uhusiano na taifa la Afrika Kusini

**Na Mashaka Mgeta**

OKTOBA 3, mwaka huu, Rais wa Nigeria, Muhammadu Buhari amekuwa kiongozi wa kwanza wa Nigeria kuzuru Afrika Kusini katika kipindi cha miaka sita iliyopita.

Ziara hiyo ilifanyika takribani mwezi mmoja baada ya raia wake kuwa miongoni mwa walioathirika kwa vurugu, uporaji na uharibifu mali za raia wa kigeni.

Buhari alifanya ziara ya kiserikali huku kukiwa na kumbukumbu za namna nchi mbili hizo zilivyoingia katika mzozo na 'vita ya maneno' kiasi cha kutishia uhusiano wa kidiplomasia na kiuchumi kati yao.

Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa akampokea Rais Buhari huku kukiwa na kumbukumbu zinazohusu raia kadhaa wa kigeni kuuawa kikatili na baadhi ya wananchi wa Afrika Kusini.

Hakuna kiongozi kutoka Nigeria aliyefanya ziara rasmi nchini Afrika Kusini, kwa kipindi cha miaka sita iliyopita.

Peter Fabricius wa taasisi inayotathmini masuala ya usalama jijini Pretoria, amekaririwa akisema uhusiano kati ya Afrika Kusini na Nigeria, sio mzuri kabisa ingawa marais hao wawili wanahusiana kwa namna inayofaa.

Kwa mujibu wa Fabricius, uhusiano wa nchi mbili hizo zenye uchumi mkubwa barani Afrika, unakabiliwa na ukinzani wa muda mrefu.

Kabla ya ziara hiyo, Serikali ya Nigeria ikatangaza kuwa Rais Buhari na mwenyeji wake Rais Ramaphosa watajadili usalama wa raia wa Nigeria nchini Afrika Kusini wakati Nigeria ikiamini kuwa miongoni mwa maeneo yanayolengwa katika vurugu na machafuko dhidi ya raia wa kigeni ni yale yanayomilikiwa na wanigeria.



Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa (kushoto) akiteta neno na Rais wa Nigeria, Muhammadu Buhari, wakati rais huyo alipofanya ziara nchini Afrika Kusini. **PICHA: MTANDAO**

Nigeria iliishutumu Afrika Kusini kwa machafuko yaliyotokea hivi karibuni ambapo raia wa Taifa hilo lenye nguvu kubwa za kiuchumi Kusini mwa Afrika, waliwashambulia, kuwapora, kuwajeruhi na kuwaua raia wa mataifa mengine ya Afrika wanaofanya shughuli mbalimbali za kiuchumi na biashara.

Miongoni mwa sababu zilizotajwa kuwa chanzo cha vurugu hizo ni madai kuwa raia wa kigeni waliopo Afrika Kusini, wanachukua ajira na fursa za kiuchumi zilizowastahili wenyeji, hivyo kuwasababishia maisha magumu na kadhia nyinginezo.

Katikati ya machafuko hayo, Afrika Kusini ikazifunga ofisi za ubalozi wake nchini Nigeria huku kukiwa na ulipizanaji visasi wa Wanigeria kwa raia wa Afrika Kusini waliokuwa wamewekeza nchini humo hususani katika jiji la Lagos.

Lunga Ngqengelele, Msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje ya Afrika Kusini, akawaambia waandishi wa habari kuwa hatua ya kuzifunga ofisi hizo ilitokana na kupokea vitisho kutoka kwa baadhi ya Wanigeria katika miji ya Abuja na Lagos.

Wakati hali ikizidi kuwa mbaya kwa mataifa hayo, Tanzania ambayo ni Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) ikaelezea kusikitishwa na mashambulizi hayo.

> hali ilivyo kwa nchi hiyo (Afrika Kusini) ilipaswa kufananishwa na Ujerumani kwa namna ilivyoathiriwa kwa 'chembechembe' zilizoachwa na utawala wa Adolf Hitler.

Hata hivyo, Tanzania kupitia kwa Waziri wa Mambo ya Nje wa Tanzania Profesa Palamagamba Kabudi, ikatangaza kuunga mkono karipio lililotolewa na Rais Ramaphosa kulaani mashambulizi hayo.

Profesa Kabudi akasema Tanzania inaendelea kuwa na mawasiliano ya karibu na Afrika Kusini, kama ilivyo kwa nchi nyingine barani Afrika na kwingineko duniani.

Lakini mvutano wa kidiplomasia ulipoongezeka kati ya Nigeria na Afrika Kusini, taifa hilo la Magharibi mwa Afrika likatangaza kususia Kongamano la Kiuchumi Duniani kuhusu Afrika lililofanyika mjini Cape Town, Afrika Kusini.

Kongamano hilo lilitarajiwa kuhudhuriwa na Makamu wa Rais wa Nigeria, Yemi Osinbajo pamoja na viongozi wengine kadhaa wa Afrika.

Wakati Afrika Kusini ikizifunga ofisi zake hizo, Nigeria ikamuita nyumbani Balozi wake nchini Afrika kwa mazungumzo, kisha ikatangaza nia ya Rais Buhari kupeleka mjumbe kwa Rais Ramaphosa, kuelezea kusikitishwa kwake na mashambulizi hayo.

Kwa upande mwingine, Afrika Kusini ikaonekana kufifisha dhana ya uhusiano wake mbaya na Nigeria, ambapo kupitia kwa Waziri wa Mambo ya Nje, Naledi Pandor, ikasema maofisa wa Nigeria na Afrika Kusini wamekuwa kwenye mawasiliano ya mara kwa mara wakijaribu kuituliza hali ya mambo.

Prisca Cornel, mmisionari mtawa aliyesomea masuala ya uhusiano wa kimataifa anasema ziara ya Rais Buhari nchini Afrika Kusini ilitoa tafsiri nyingi, miongoni mwa hizo ni kuirejesha hadhi ya raia wa nchi hiyo, walioonekana kuwa wakatili na wasiokuwa na upendo kwa Waafrika wenzao.

Cornel anasema machafuko ya Afrika Kusini yaliashiria mbegu ya chuki iliyopandwa kwa baadhi ya raia wake tangu nyakati za utawala wa makaburu, na hivyo kuonekana kwamba inaendelea hata baada ya kuondoka kwa watawala hao waliopingwa katika ukanda wa Afrika na kwingineko duniani.

"Unajua kwa historia, Afrika Kusini ina matukio mengi yenye taswira ya ukatili dhidi ya ubinadamu, hivyo hata matukio yaliyotokea, yaliendeleza hisia hizo na hivyo kuwafanya raia wake kuonekana kuwa tofauti na wengine," anasema.

Cornel anasema hali ilivyo kwa nchi hiyo (Afrika Kusini) ilipaswa kufananishwa na Ujerumani kwa namna ilivyoathiriwa kwa 'chembechembe' zilizoachwa na utawala wa Adolf Hitler.

"Kwa hiyo Rais Buhari alipofanya ziara yake nchini humo, inaweza kuwa sehemu ya kuionyesha dunia kwamba pamoja na kuwa Nigeria iliingia katika mzozo mkubwa na Afrika Kusini, lakini bado nchi hiyo inapaswa kuheshimika na sehemu kubwa ya raia wake wanathamini utu wa binadamu," anasema.

Kwa upande wake, Kasmir Masawe ambaye ni mwanaharakati wa masuala ya ukuzaji uchumi wa kikanda anasema, Nigeria inatambua umuhimu wa Afrika Kusini katika mukhtadha wa ukuzaji uchumi na biashara kwa watu wake, hivyo ziara ya Rais Buhari ni moja ya ushawishi utakaofanikisha kujenga mazingira salama kwa raia wake nchini humo.

Anasema, hivi sasa Nigeria ni miongoni mwa nchi ambazo raia wake wameenea kwenye mataifa mengi ndani na nje ya Afrika, hivyo kinachofanyika kwa nchi hiyo iliyopo Magharibi mwa Afrika ni kuhakikisha yanakuwepo mazingira bora kwa watu wake.

"Hata kama vurugu zile zingedhibitiwa kwa haraka na vyombo vya dola na hivyo kujenga imani kwamba serikali ya Afrika Kusini ilichukizwa na hivyo kuchukua hatua, lakini bado serikali ya Nigeria inapaswa kuchukua hatua zenye kuwanufaisha raia wake wanaofanya kazi na biashara kwenye mataifa mengine ikiwamo Afrika Kusini," anasema.

# AJENDA YA MWANAMKE TURUFU YA USHINDI UCHAGUZI 2019/20120

INATOKA UK.13

la Jinsia lililofanyika kwenye ofisi za TGNP- Mtandao Mabibo jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na makundi mbalimbali ya wananchi kutoka kila pembe ya nchi pamoja na viongozi, imetoa madai mbalimbali ikiwemo haki za kushiriki katika uchaguzi kama wapiga kura na wanaowania nafasi za uongozi.

Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP-Mtandao Lilian Liundi anasema Ilani hiyo ya Uchaguzi ya Wanawake inawahamasisha kukataa kuendelea kutumiwa kama wapiga debe, wasindikizaji katika kampeni, waburudishaji na wahanga wa ufukara na umaskini.

Badala yake amesema lengo ni wanawake wote wahamasike na kushikamana ili kupambana na mifumo kandamizi hususani mfumo dume ambao huathiri upatikanaji wa haki na hatimaye kudumaza uchumi na maendeleo ya jamii yote.

"Tunaamini ilani hii ya uchaguzi ya wanawake, itamjengea uwezo wa namna ya kusimama mwenyewe kuwania nafasi mbalimbali za uongozi kwa kuzingatia kanuni na sheria ukilinganisha na ilivyokuwa awali ambapo wanawake wengi wanatamani kugombea lakini kutokana na mfumo dume uliopo na masuala ya rushwa inakuwa kikwazo kwao," anasema Liundi.

Liundi anasema sio wanawake pekee ambao ni walengwa wa Ilani hiyo ya uchaguzi bali imelenga makundi mengine vikiwemo vyama vya siasa ambavyo ni njia pekee ya kuingia kwenye kinyang'anyiro cha uchaguzi, hivyo vinatakiwa kuwa walinzi wa lango la kuingia kwenye siasa za uchaguzi ambazo huamua nani aingie na nani aachwe.

Walengwa wengine ni Serikali kuu iliyoko madarakani na taasisi zake, ina wajibu mkubwa wa kuhakikisha kuwa uwanja wa ushindani wa kisiasa ni huru na salama kwa makundi yote hususani wanawake.

Vilevile Ilani hiyo inalenga vyombo vya habari kwa uwezo wao wa kugusa mtazamo wa jamii kuhusu nafasi ya wanawake katika uongozi na maendeleo ya taifa.

Lakini pia inalenga wapiga kura wote wanawake kwa wanaume, vijana kwa wazee kutambua kwamba kura ni zao ni Turufu ya Ushindi kwa vyama vyao vya siasa na wagombea.

### MADAI YA WANAMTANDAO WANAWAKE WA KATIBA NA UCHAGUZI

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa TGNP- Mtandao, Asseny Muro anasema miongoni mwa madai ya wanamtandao wa wanawake na katiba na uchaguzi kwa Serikali iliyoko madarakani ni pamoja na

Kuhakikisha wadau wote wa uchaguzi wanazingatia misingi ya ushindani wa haki na usawa wa jinsia kama ilivyoainishwa kwenye katiba, sheria, sera, mipango ya nchi na kubainishwa kwenye mikataba ya kimataifa na kikanda ambayo serikali imeridhia.

Kuhakikisha na kusimamia vyombo vyote vya dola vilivyopewa dhamana ya kusimamia uchaguzi vizingatie miongozo, sheria zenye kulinda wanawake dhidi ya matendo ya udhalilishwaji wakati wa uchaguzi.

Mahakama kushughulikia kesi za uchaguzi kwa kutumia hekima ambayo haiendelezi ukiukwaji wa haki za wanawake na watu wenye ulemavu.

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Takukuru, kudhibiti na kupambana na rushwa ikiwemo ya ngono kama ilivyobainishwa kwenye kifungu 25 cha sheria namba 11 ya mwaka 2007 ya kuzuia na kupambana na rushwa wakati wa uchaguzi.

Msajili wa vyama vya siasa ahakikishe anatoa miongozo kwa vyama vya siasa yenye tafsiri ya kuongoza vyama kuzingatia haki za wanawake na watu wenye ulemavu kwenye kushiriki katika uongozi wa vyama vyao kama ilivyoainishwa kwenye Katiba ya Nchi, mikataba ya kimataifa na kanda pamoja na sheria ya vyama vya siasa 2019 kifungu (6A) pamoja na kutoa elimu ya urai na mpiga kura.

"Wanawake wapiga kura wanatambua kwamba Serikali iliyoko madarakani pamoja na vyombo vyote vya dola na taasisi zake ina wajibu wa kuweka mazingira wezeshi na salama kwa wanawake na watu wenye changamoto za kimaumbile wakati wote wa zoezi la uchaguzi hivyo tusiwe nyuma kushiriki kwenye uchaguzi," anasema Muro.

Amewasisitiza wanawake kuwa ushindi wao unategemea sana uamuzi wa wapiga kura, wake kwa waume kuzingatia kuwa ni kundi kubwa zaidi hivyo wanapojitokeza wenye uwezo na wenye kubeba ajenda ya ukombozi wa mwanamke kimapinduzi, hivyo wahamasike kuwapigia kura wenzao bila kujali itikadi za vyama.

Rais wa kwanza mstaafu wa Bunge la Afrika, Getrude Mongela, anasema kumekuwa na wimbi kubwa la wanasiasa kubaka siasa akiwa na maana kuwa wengi wao hawajiamini kwenye kupata nafasi za uongozi kwa haki, badala yake wanatumia rushwa.

Anasema kundi hilo la wabakaji wa siasa limekuwa kikwazo kikubwa cha maendeleo kwa sababu wengi wanaopata madaraka kupitia rushwa hawana uwezo wa kuwatumikia wananchi.

Amewaasa wanawake kujitokeza kwa wingi kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa ili kubeba ajenda ya ukombozi wa mwanamke kimapinduzi.

Mongela anasema mwanamke ndiye mbeba maono ya taifa, hivyo akipewa dhamana ya uongozi atafanya vizuri ukilinganisha na mwanaume.

Spika mstaafu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Anne Makinda, anasema kumekuwa na tabia ya wanawake kutumika kwenye kampeni za siasa bila faida yeyote, tabia ambayo ameilaani na kwamba ni wakati wao kuingia kwenye vinyang'ang'iro vya uchaguzi kuliko kuwa vibaraka.

Makinda anasema miongoni mwa sababu zinasababisha wanawake walio wengi kuwa vibaraka kwenye chaguzi ni kutokujiamini na woga, aliwasisitiza kuachana na mtindo huo kwani wanaweza.

Diwani wa Kata ya Mshewe iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Esther Mbega anasema siri yeye kushinda udiwani ilikuwa ni kujiamini na kuthubutu kuwa anaweza kuongoza.

Anasema licha ya kupata changamoto mbalimbali kwenye mchakato wa uchaguzi uliopita, lakini alipambana kuhakikisha anashinda ili kutimiza lengo la kuwatumikia wananchi wa Kata ya Mshewe.

Ofisa Habari wa Taasisi ya Mtandao wa Jinsia Tanzania TGNP-Mtandao, Monica John anasema Tamasha la 14 la Jinsia limetoa fursa kwa Watanzania kujadili masuala mbalimbali yanayohusu usawa wa kijinsia kuelekea uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Anasema Tamasha hilo ambalo limebeba kauli mbiu isemayo "Wanaharakati mbioni kuibadilisha dunia" italeta tija endapo kila mmoja kwa nafasi yake atawajibika kwa kufuata misingi na taratibu za nchi na kuzingatia usawa wa kijinsia.



Matukio ya kujitokeza kwa wingi kwa kinamama kama haya yasiishie kwenye maadhimisho tu, sasa yapanuke kwenye uchaguzi wakianzia na ule wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu mwakani. **PICHA: MTANDAO**

> Mwanamke ndiye mbeba maono ya taifa, hivyo akipewa dhamana ya uongozi atafanya vizuri ukilinganisha na mwanaume.



Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP- Mtandao, Lilian Liundi (kushoto), akionyesha Ilani ya Uchaguzi ya Wanawake 2019/2020 mara baada ya uzinduzi. **PICHA ZOTE: GRACE MWAKALINGA**

> licha ya kupata changamoto mbalimbali kwenye mchakato wa uchaguzi uliopita, lakini alipambana kuhakikisha anashinda ili kutimiza lengo la kuwatumikia wananchi wa Kata ya Mshewe.

## IMF mbioni kurejesha msaada DRC



Rais wa sasa wa DRC, Felix Tshisekedi (kushoto) na rais wa zamani wa nchi hiyo Joseph Kabila. **PICHA: MTANDAO**

SERIKALI ya Kinshasa inasema Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), linafikiria kuidhinisha upya ushirikiano wa kifedha na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), katika kipindi cha miezi sita ijayo, Reuters linaripoti.

IMF lilisitisha msaada wa kifedha kwa serikali ya DRC, miaka takriban miaka saba iliyopita chini ya utawala wa Rais Joseph Kabila, baada ya serikali hiyo kushindwa kutoa taarifa za kutosha kuhusu mauzo ya madini kwa kampuni ya ng'ambo.

Katika taarifa yake kufuatia kikao cha baraza la mawaziri, serikali imesema:

"IMF litakagua katika muda wa miezi sita mpango wa muda mfupi wa serikali."

Hata hivyo, taarifa hiyo haikutoa maelezo zaidi kwa mujibu wa vyombo ya habari.

IMF linafikiria ushirikiano mpya wa kifedha na DRC, kufuatia majadiliano mapya kati ya pande hizo mbili, Jarida la Bloomberg limemnukuu waziri mkuu wa nchi hiyo, Sylvestre Ilunga.

Katika ripoti yake mapema wiki hii, IMF limeeleza kuwa wakurugenzi wake wamekaribisha majadiliano mapya ya serikali ya Kinshasa na IMF na kusisistiza kuwa mageuzi ya amani ya kisiasa nchini humo yanatoa fursa kuidhinisha mageuzi yatakayoweza kuimarisha mifumo ya fedha za umma, kushinikiza ukuaji wa sekta na kukabiliana na ufisadi na umaskini nchini.

Kadhalika shirika hilo limeeleza kuwa linatambua DRC inahitaji msaada wa jamii ya kimataifa kwa ajili ya kujenga uwezo wake.

DRC imebarikiwa kuwa na madini mengi pamoja na maliasili, lakini imeathiriwa na vita vinavyosababishwa na vikundi vya waasi, rushwa, machafuko ya kisiasa na hivi sasa janga la Ebola.

Taifa hilo ni mchimbaji mkubwa wa madini ya cobalt, shaba, dhahabu, tin na almasi, lakini linasalia kuwa mojawapo ya mataifa yanayoshuhudia maendeleo duni duniani.

**BBC**

TUJIKUMBUSHE

# THEODORE HALL

- Mwanasayansi mwenye umri mdogo kufanya kazi katika mradi maarufu uliotengeneza bomu la kwanza la atomiki duniani
- Jasusi wa Marekani aliyevujisha siri ya nyuklia kwa Urusi

AGOSTI 29 mwaka 1949, iliyokuwa Muungano wa Nchi za Kisoviet za Kirusi (USSR) ama Urusi ya sasa ilikuwa rasmi "taifa la atomiki" ilipolipua silaha yake ya kwanza ya nyuklia, bomu lililojulikana kama RDS-1.

Serikali za Magharibi ziligutushwa sana na suala hilo kwa mujibu wa rekodi za Shirika la Ujasusi la Marekani (CIA). Majasusi wa Marekani walifikiria Wasovieti hawangeweza kutengeneza bomu la nyuklia kabla ya mwaka 1953.

Cha kushangaza ni kwamba ni mwanasayansi wa Marekani, Theodore Hall, aliyeisaidia Moscow kufikia azma yake ya kumiliki silaha za nyuklia kwa kuipatia taarifa.

Ni kweli kwamba Hall hakuwa raia wa pekee wa Marekani aliyevujisha siri ya uundaji wa bomu la atomiki kwa maadui wa nchi hiyo.

Lakini kilichompatia umaarufu ni jinsi alivyoweza kutekeleza kazi yake kisiri bila kutambuliwa.

Je, mzaliwa huyu wa New-York, aliyesomea sayansi ya nyuklia katika Chuo Kikuu cha Harvard, aligeuka vipi kuwa jasusi?

Haikuwa jambo la kushangaza kuwa bomu la RDS-1 lilifanana sana na bomu la atomiki lililorushwa na Marekani katika mji wa Nagasaki nchini Japan 9 Agosti 9, 1945.

Taarifa za kina kuhusu muundo wa bomu hilo ilifichuliwa kwa Wasovieti kutoka kwa msiri wa ndani wa mradi wa Manhattan, jina fiche lililotumiwa kuelezea mpango wa uundaji wa silaha za atomiki, uliokuwa unaongozwa na Washington, kwa ushirikiano na Uingereza na Canada.



Theodore Hall. **PICHA: MTANDAO**

### SIRI KUBWA

Kuweka siri ilikuwa kigezo kikubwa. kulingana na nukuu ya taarifa iliyochapishwa katika jarida la Life Magazine mwaka 1945, "Bila shaka ni watu wachache sana kote Marekani waliojua maana halisi ya Mradi wa Manhattan."

Mmoja wa watu hao alikuwa Hall. Alizaliwa Oktoba 20 Mwaka 1925. Mamake mzazi alikuwa mke wa nyumbani na baba yake alikuwa mfanyabiashara.

Hall alikuwa na nyakati ngumu sana kimaisha kama ilivyokuwa kwa Wamarekani wa kawaida.

Hata hivyo, hali hiyo haikumzuia kufikia malengo yake kimasomo hasa katika somo la hisabati na fizikia.

Akiwa na umri mdogo wa miaka 16, alipata nafasi ya kujiunga na Chuo Kikuu cha Harvard, ambako alifuzu mwaka 1944.

Uwezo wake wa kimasomo uligunduliwa na maofisa wa Marekani waliokuwa wakitafuta watu watakaowafanyia kazi katika mradi mpya wao wa nyuklia.

Theodore Hall alihojiwa na kupewa nafasi ya kuhudumu katika maabara ya kisiri ya Los Alamos mwanzoni mwa mwaka 1943.

Lakini kile ambacho maofisa wa Marekani hawakukifahamu ni kuwa mwanafizikia huyo mchanga alikuwa amefanyiwa usaili mwingine kama huo.

> "Wasovieti walipigana na Wanazi kishujaa, hatua ambayo huenda ilisaidia washirika wake wa Magharibi kutoshindwa.

Hall alikuwa mwanachama wa kundi la wanafunzi wa Harvard wanaoegemea falsafa ya Karl Marx, akiwa na mwanafunzi mwenzake aliyefahamika kama Saville Sax.

Sax alikuwa mwana wa kiume wa wahamiaji wa Urusi na alikuwa mfuasi sugu wa Kikomunisti, japo alizaliwa na kulelewa mjini New York.

Ukweli ni kuwa Sax ndiye aliyemshawishi Hall kujiunga na Wasovieti na kuwa ajenti wa kutoa siri za nyuklia kwa Wasovieti.

Mwezi Desemba 1944, mwanasayansi huyu mchanga, kwa ushirikiano na mwanafunzi mwezake wa zamani, walivujisha kwa mara ya kwanza kabisa siri kubwa kutoka Los Alamos, iliyohusisha namna ya kuunda bomu la platoniki.

"Wakati huo mwaka 1944, nilikuwa na hofu kuhusu hatari ya Marekani kuwa mmiliki pekee wa silaha za atomiki baada ya vita ya dunia," alisema Hall katika taarifa iliyoandikwa na kuchapishwa na Gazeti la New York Times mwaka 1997, miaka miwili kabla hajafariki dunia kutokana na saratani ya figo.

Hall alidai kuwa USSR kumiliki ni njia bora zaidi ya kuidhibiti Marekani

"Muungano wa Sovieti wakati huo haukuwa adui, bali mshirika wa Marekani." Hall alisema na kuongeza:

"Wasovieti walipigana na Wanazi kishujaa, hatua ambayo huenda ilisaidia washirika wake wa Magharibi kutoshindwa."

Alijulikana na Wasovieti kama "The Youngster" na aliendelea kuifichulia Moscow siri kuhusu teknolojia ya mawasiliano, hasa jinsi ya kulipua mabomu yaliyoundwa kwa madini ya plutonium.

Bomu lililodondoshwa na Marekani katika mji wa Nagasaki nchini Japan, liliundwa kutokana na madini ya plutonium, tofauti na lile lililolenga Hiroshima, ambalo liliundwa kutokana na madini ya uranium.

### UJUMBE WA KISIRI

Marekani na USSR huenda walipigana dhidi ya adui mmoja wakati wa vita Vikuu vya Pili vya Dunia, lakini huenda hatua hiyo haikuzuia Moscow na Washington kuchunguzana.

Ukweli wa mambo ni kuwa Marekani katika hatua ya kukabiliana na ujasusi wa Wasovieti, ilianzisha mradi uliofahamika kama Venona ambao ulianza kazi mwezi Februari mwaka 1943.

Mwezi Desemba mwaka 1946, majasusi wake walifanikiwa kudukua mawasiliano kutoka NKVD, wizara ya mambo ya ndani ya Muungano wa Sovieti.

Mawasiliano ya Wasovieti yaliyodukuliwa na Marekani yalibaini kuwa Wasovieti wamekuwa wakichunguza kisiri Mradi wa Manhattan.

Mamlaka ya Marekani iligundua kuwa Hall aliwasiliana na Urusi mwaka 1944.

Hall alikuwa akifanyia kazi mradi wake wa PhD katika Chuo Kikuu cha Chicago mwaka 1950, wakati maofisa wa upelelezi wa Marekani FBI walipombishia mlango.

Alifahamika kama mshirika wa Moscow wa ujumbe wa siri.

Jasusi mwingine wa Los Alamos, alikuwa mwanafizikia wa Ujerumani Klaus Fuchs, ambaye alikamatwa mwaka uliotangulia, baada ya kukiri jukumu lake katika kuwatumia maadui wa siri za nyuklia za Marekani.

Hata hivyo, wapelelezi wa FBI hawakupata ushahidi wowote kutoka kwa Hall na Sax ambaye pia alichunguzwa.

### SAFARI YA KWENDA UINGEREZA

Wanasayansi hao hawakupatikana na madai ya kutoa siri kwa Urusi kwasababu uchunguzi haukuonyesha ushahidi kutokana na ukweli kuwa Hall hakujihusisha na masuala hayo baada ya mradi wa Manhattan.

Kulikuwa na nyaya za Moscow za mawasiliano ya Moscow ambazo zilitumika kama ushahidi lakini Mamlaka ya Marekani hazikutaka kuzitumia mahakamani, kwasababu hatua hiyo ingelifichua kuwa walidukua mawasiliano ya Wasovieti.

Mwisho wa siku, Hall alipona mashtaka na wala hakuchukuliwa hatua kama watu wengine waliofungwa jela na wengine kunyongwa kwa kutoa siri za nchi.

Licha ya hayo Hall na mke wake walihofia usalama wao. Aliachana na wadhifa wake wa kielimu mjini Chicago na kuangazia shughuli za utafiti katika hospitali za New York.

Mwaka 1962, alipata kazi katika Chuo Kikuu cha Cambridge, hali iliyomfanya kuhamia Uingereza na mke wake.

Hall alistaafu mwaka 1984 na kuamua kuishi maisha ya kisiri.

Lakini mwaka 1996, mambo aliyofanya zamani yalifichuliwa baada ya mawasiliano kati yake na Urusi kutolewa hadharani.

Wakati huo mashahidi wote waliofahamu mienendo ya Hall walikuwa wamefariki dunia akiwamo Sax.

"Inadaiwa kuwa niligeuza mkondo wa historia," Hall aliwaambia waandishi wa New York Times na kuongeza: "Pengine kama mkondo wa historia haukugeuzwa huenda mngeliongoza vita vya silaha za atomiki kwa miaka 50... Kwa mfano bomu hilo lingedondoshwa China mwaka 1949 ama mwanzoni mwa miaka ya 1950."

Anasema kwamba alifanikiwa kubadili matukio hayo, "Nakiri makosa," anasema.

Hakujawahi kuwa na mashambulio ya nyuklia tangu yalipofanyika mashambulio ya Hiroshima na Nagasaki miaka 74 iliyopita na Hall alifariki akiamini kuwa alichangia kutomika tena kwa silaha hiyo ya maangamizi. **BBC**

# Nini nafasi ya wanawake kutamba uchaguzi ujao?

• Profesa 'm-mama' ataja kilichoko • Wanga'aka dhana 'hatupendani' • Safari ile 'waliwafunika' kinababa

**Na Christina Mwakangale**

UCHAGUZI wa serikali za mitaa unatarajiwa kufanyika mnamo Novemba 24 mwaka huu, kwa kushirikisha jumla ya halmashauri 185 nchini.

Ni uchaguzi unaofanyika kupata viongozi katika nafasi za ngazi ya mitaa, wanawake wanatajwa kuwa wadau wakuu wa ushiriki.

Akizungumza mwishoni mwa wiki na wananchi katika mji mdogo wa Laela, Mkoa wa Rukwa, Rais Dk. John Magufuli, aliwasisitiza wananchi wajitokeze kujiandikisha utakapofika wakati na watumie fursa ya uchaguzi kuwapata viongozi wanaowafaa, vivyo hivyo kwa wanaowania uongozi wajitokeze.

Kimsingi, ndicho alichokihimiza Waziri wa Ofisi ya Rais (Tawala za mikoa na Serikali za Mitaa- Tamisemi), Suleiman Jaffo, kuwataka wananchi kujitiokezakatika uandikishaji

Mwaka mmoja kutoka sasa, nako kutakuwa kumetimu miaka mingine mitano ya uchaguzi mikuu kufanyika kumpata Rais, wabunge na madiwani.



Kinamama wakiwa katika foleni ya kupiga kura. **PICHA: MTANDAO**

**KINAMAMA WALIPO**

Katika makundi hayo ya kijamii na kisiasa, kinamama nao wanahimizwa kushiriki katika hilo, kuwania nafasi, pia kujitokeza kupiga kura na kuna baadhi ya vyama vya siasa vimeenda mbali kuliainisha hilo.

Mtaaluma wa Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam (UDSM), Profesa Bertha Koda, anasema mbali na changamoto zilizopo, wanawake hushiriki katika hatua anazoziorodhesha hizo jumla yake ziko nne.

Msomi huyo mwenye mzizi kutoka Taasisi ya Taaluma ya Maendeleo ya UDSM, anazitaja kuwa: Kabla ya uchaguzi; wakati wa upigaji kura; kuhesabu; utoaji matokeo na baada ya uchaguzi.

Akiwasilisha mada kuhusu haki za wanawake katika mchakato wa uchaguzi kwa madiwani wanawake kutoka mikoa tofauti nchini, mwezeshaji huyo wa masuala ya kijinsia, Profesa Koda anasema takwimu zinabainisha asilimia 53 ya wapiga kura za uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, zilikuwa za kinamama.

Anaieleza hatua ya awali ni kabla ya uchaguzi, ambako kuna hatua azozitaja kuwa ni: Uchambuzi na maboresho ya sheria, utayarishaji miongozo, ugawaji majimbo, uboreshaji daftari la wapiga kura na uandikishaji wapiga kura

Profesa Koda anasisitiza umuhimu alioutaja, pia kinamama kuwa sehemu ya maandalizi na kushiriki uchaguzi, ambao katika mchakato wake unaanza mapema, suala la jinsia linachukua nafasi kudai maboresho kisheria, maelekezo na miongozo.

Anasema, changamoto mojawapo kabla ya uchaguzi ni mazingira yasiyo rafiki ya kufikia vituo vya kujiandikisha, ambavyo havizingatii majukumu ya wanawake katika kaya.

Msomi huyo anasema tafiti zilizofanywa na mtandao, zilibaini hamasa kubwa waliyo nayo wanawake kutimiza haki yao kwenye uchaguzi, wengi wanakatishwa tamaa na foleni ndefu na umbali wa vituo vya kujiandikisha.

> Elimu duni ya uraia kwa wapiga kura isiyozingatia mengi ya kijinsia, ikiwamo ukatili wa kijinsia kwenye kampeni, ni mambo yanayopaswa kukomeshwa.

"Mfano tulibaini kuwa katika vituo hivi, wanawake hujitokeza kujiandikisha zaidi majira ya saa nne asubuhi hadi mchana, baada ya hapo huondoka kwenda kuendelea na majukumu katika kaya zao, vituo viwe jirani, tuzingatie usawa wa kijinsia, ili mwanamke huyu akichota maji, akishapikia familia yake arudi tena kujiandikisha," anasema Profesa. Koda.

Anafafanua kuwa elimu duni ya uraia kwa wapiga kura isiyozingatia mengi ya kijinsia, ikiwamo ukatili wa kijinsia kwenye kampeni, ni mambo yanayopaswa kukomeshwa.

Pia, mtaaluma huyo anafafanua kwamba katika michakato inayofuata hatua hiyo, kama vile upigaji na kuhesabu kura, pia kutangaza matokeo, itakwenda sawa baada ya maandalizi kabla ya uchaguzi kutekelezwa ipasavyo.

"Usalama wa wanawake wagombea wakati wa upigaji kura, wasimamizi wa zoezi la kupiga kura kuelimishwa namna ya kutambua matukio ya udhalilishaji ni muhimu, ni sehemu ya maandalizi kwa wanawake kuondolewa vikwazo kabla ya uchaguzi," anasema Profesa Koda.

**TAKWIMU ZIKOJE?**

Katika hilo Profesa Koda anasema, ongezeko la asilimia 4.4 la wapiga kura wanawake kati ya asilimia 95 waliojiandikisha mwaka 2015, lilitokana na wadau wanawake kutambua kuwa kura zao ni turufu ya ushindi.

Anaeleza takwimu za Tume ya Uchaguzi (NEC), zilibaini ongezeko hilo, huku uchambuzi uliofanywa na Mtandao wa Wanawake na Uongozi kupitia Mfuko wa Wanawake (WFT), unabaini uchache wa viongozi wanawake kwenye ngazi za maamuzi licha ya kwamba ni wapiga kura wazuri.

"Tunaweza kutafsiri kuwa, ushiriki wa wanawake katika kupiga kura au mchakato wote, unatokana na wao kujitambua, kuelimishwa, kushirikishwa, lakini bado wanawake hawajaandaliwa au kuondolewa vikwazo kufikia uongozi," anasema Prof. Koda.

**MDAU MUHIMU**

Gema Akilimali ni kati ya washiriki waliochangia mada katika warsha hiyo, anasema uchache wa wanawake kwenye ngazi za maamuzi kunachelewesha kufikiwa kwa masuala ya kijinsia kikamilifu.

Anasema changamoto za huduma ya afya ya uzazi, maji safi na salama, hususan kwa maeneo yaliyo pembezoni, zinatokana na msukumo hafifu katika vipaumbele vya kijinsia na kupitishwa bajeti finyu.

"Anayefahamu maana halisi ya tatizo la upatikanaji wa maji umbali mrefu wa zaidi ya mita 400 ni mwanamke ambaye anaamka alfajiri kufuata maji, wanawake haohao ndio wachache kwenye uongozi, nani atawatetea," anasema Akilimali.

Diwani, Anna Mgella kutoka Kata ya Singisa, katika Manispaa ya Morogoro, anasema kuna dhana kutoka kwa baadhi ya wanawake kwamba 'hawapendani' jambo linokwamisha kujiamini na uthubutu kwa viongozi watarajiwa.

"Kauli kwamba wanawake 'hatupendani' si sahihi na dhana hii ifutwe. Ni vizuri kuwaandaa wanawake watarajiwa kwenye uongozi ili tuongezeke katika ngazi za maamuzi nchini na kufikia malengo," anasema Mgella.

**MKAKATI ULIVYO**

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro na Diwani wa Kata ya Ngerengere, Kibena Nassoro, anasema mkakati wa wanawake ni kwamba ifikapo 2025, idadi ya wenyeviti kwenye halmashauri iongezeke.

Kibena ambaye pia ni mwenyekiti wa Wanawake wa Serikali za Mitaa (Wasemi), anasema wataendelea kuhamasisha wanawake kujitokeza kugombea na kushinda, bila kukata tamaa.

"Mimi ni miongoni mwa wanawake watano wenyeviti wa halmashauri nchini, kati halmashauri zote 180, hapa mtaona bado tuna kazi kubwa ya kuhakikisha tunafika ngazi za maamuzi hususan wenyeviti wa halmashauri ili kuhimiza masuala ya kijinsia kwenye jamii," anasema Kibena.

**Mwandishi anatumikia Kituo cha Taarifa kwa Wananchi (TCIB)**

# Fungamano dhidi ya Iran lafifia

• Ni pale Marekani iliposita kujibu kushambuliwa Saudia Arabia



Mwanamfalme wa Saudi Arabia, Mohammad bin Salman (kushoto) na kiongozi wa Iran, Ayatollah Ali Khamenei. **PICHA: MTANDAO**

**Na Ani Jozeni**

ZIPO dalili kuwa Saudi Arabia na Iran zimekubali kuanzisha majadiliano kwa kutumia wajumbe tofauti ili kupunguza uhasama ulioko baina ya nchi hizo mbili, hasa kuhusiana na vita ya muda mrefu nchini Yemen na kushambuliwa kwa makombora kwa medani kubwa ya mafuta huko Saudia.

Ni hatua ambayo inaonyesha dalili kuwa hapatakuwa na vita hivi karibuni eneo la Mashariki ya Kati, kwani nyendo za kuizunguka Iran kutoka Kusini kwa muungano wa Marekani, Saudia na Israel, licha ya nchi nyingine za Ghuba, sasa zinafifia.

Kwa upande wa pili, baadhi ya wachunguzi wanaamini mawasiliano hayo yatasaidia kutatua migogoro iliyopo sasa.

Wachambuzi wa habari wanasema mabadiliko katika mwenendo wa matukio eneo hilo yanatokana na Rais Donald Trump wa Marekani kukataa kufanya shambulizi la moja kwa moja dhidi ya Iran kutokana na kushambuliwa medani kubwa ya mafuta nchini Saudia.

Mazingira yalionyesha kuwa Saudia haiungwi mkono katika nchi za Ulaya na hata nchini Marekani licha ya kuwa ni mshirika muhimu wa kibiashara, kwani shambulizi hilo linahusiana angalau kwa kiwango fulani na vita ya Yemen.

Ni mapambano yasiyo na viwango vyovyote vya kujali haki za binadamu, hasa kutokana na washirika wa Saudia kupiga kokote mradi huenda wako wapiganaji.

> “Vita ya Yemen ikiisha kwa ushindi wa Wahuthi, ni wazi kuwa matazamio ya ushindi wa u-Shia yataenezwa katika nchi zilizobaki za Ghuba, ikiwemo Saudia.

Gazeti mashuhuri la New York Times nchini Marekani lilisema kuwa serikali ya Saudia imekiri kuwa Iraq na Pakistan zimejitolea kusuluhisha Saudia na Iran lakini taarifa ya Saudia ilikataa hisia kuwa mwanamfalme Mohammed bin Salman aliandaa hatua hizo za kidiplomasia.

Taarifa ya serikali ya Saudia ilisema “juhudi za kupunguza hali ya mvutano lazima zitokane na upande ulioanzisha hatua ya kupandisha utambi na kufanya mashambulizi, na siyo ufalme wa Saudia.”

Gazeti hilo hata hivyo lililisisitiza kuwa kutokuaminiana kati ya pande hizo mbili ni kwa kina kirefu na kuwa mazungumzo ya ana kwa ana bado yako mbali, ila hata ‘kugusia tu’ inasaidia.

Endapo juhudi za kutafuta angalau eneo la muafaka au kutafuta muafaka zitapiga hatua fulani, huenda migogoro mikubwa inayoikumba Mashariki ya Kati, hasa ile ya Lebanon, Syria, Iraq na Yemen inaweza kuanza kutulia, hata kama si kupatiwa ufumbuzi.

Moja ya maeneo makuu ya mgongano ambalo kwa sasa haielekei kuwa litakuwa na majibu ni hitaji la Iran kutaka Saudia isishirikiane na maadui wakuu wa Iran, yaani Israel na Marekani.

Hivi sasa kampeni ya kuibana Iran kwa kiwango cha juu inavyowezekana inaendelea kuilazimisha kuachana na mipango yake ya kufikia umiliki wa silaha za nyuklia na kuacha kuchochea migogoro, kusaidia wapiganaji kote.

Baadhi ya wachunguzi wanasema kuwa kusita kwa Rais Trump kuidhinisha kipigo dhidi ya Iran baada ya medani ya mafuta kushambuliwa, wakati mwanzoni alionekana kuwa tayari kwa jambo hilo, kumeleta hisia tofauti nchini Saudia.

Baadhi ya washauri wa Mfalme Salman wameanza kuhoji kama Marekani itasimamia kwa dhati usalama wa Saudia, hivyo kuulazimisha utawala wa Mohamed bin Salman kuangalia upya mwenendo wa nchi hiyo katika eneo la Ghuba.

Kwa maana hiyo Saudia inatafuta mlango wa kutokea isipambane na Iran ana kwa ana kwani endapo kunatokea shambulio kama lile la medani ya mafuta halafu Marekani isijibu, ni kama vile haioni kuwa Saudia ni mshirika wa dhati.

Ni kujiona imeachwa pekee katika uhusiano na Marekani.

Gazeti la New York Times liliainisha kuwa utayari wa Iran kukutana na wajumbe wanaowakilisha hisia za Saudia unatofautiana kabisa na udhati wa kutotaka mawasiliano yoyote na Marekani, likitoa mfano wa Rais Hassan Rouhani ‘kukwepa’ kuchukua nafasi ya kukutana na Rais Trump hivi majuzi.

Lilisema marais hao wawili walikuwa ‘wanahudhuria’ mkutano wa mwaka huu wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, maelezo ambayo siyo sahihi. Wakuu hao wawili walifanya tu safari kwa wakati unaohitajiwa, kufika kabla ya muda wa kutoa hotuba kuanza, kutambulishwa kwa wajumbe wa baraza hilo wanaohudhuria, yaani mawaziri wa mambo ya nje na mabalozi.

Ina maana kuwa Rais Rouhani hakukwepa kukutana na Rais Trump ila hapakuwa na maandalizi yoyote ya mkutano kama huo yaliyoombwa na upande wa Iran au Marekani.

Isitoshe, tangu mashambulizi dhidi ya medani ya mafuta ya Saudia yafanyike, Rais Trump hajaonyesha kuwa na haja ya kufanya mazungumzo na Iran na katika hotuba yake mbele ya Baraza Kuu alisema kuwa “kila taifa lina wajibu wa kuchukua hatua dhidi ya Iran,” ambao siyo usemi wa kuashiria kuwa tayari kwa hatua zozote za kutafuta suluhu.

Marekani iliongeza vikwazo kugusa wakuu wa Iran kuanzia majenerali wakuu wa jeshi lake, kundi la wapiganaji, Revolutionary Guards ambalo pia linamiliki rasilimali, kufanya biashara na nchi tofauti, na kiongozi mkuu Ali Khamenei, mwisho Benki Kuu ya Iran ikatajwa katika vikwazo, kuwa anayefanya biashara na Marekani asihusike nayo.

Ambacho kinafahamika kwa usahihi ni kuwa baada ya mashambulizi dhidi ya medani ya mafuta ya Saudia na katika mazingira ambako Marekani bado ilikuwa inashereheka kuondoka kwa mshauri wa usalama wa taifa John Bolton, Rais Trump hakuona asimamie wapi ili kuipiga Iran.

Hivi sasa Marekani haiungwi mkono hata na washirika wake wa NATO kujitoa katika mkataba wa nyuklia na Iran, wakati utawala wa Saudia ulikuwa unalaaniwa tena hivi karibuni, kwenye kumbukumbu ya mwaka mmoja ya mauaji ya mwandishi Jamal Khashoggi katika ubalozi wa Saudia jijini Istanbul, Uturuki.

Hakuna nchi ya Magharibi inataka vita kuisaidia Saudia hivi sasa.

Hata hivyo, jitihada za hivi sasa za Saudia hazionyeshi kuwa zitazaa matunda kwani tofauti kati ya Iran na Saudia ni za msingi, zinazotokana na aina za tawala za kiimla zinazoongoza nchi hizo, na mizozo ya kidhehebu isiyo na suluhisho.


Siyo rahisi kuona, kama wachambuzi wa New York Times na kwingine wanavyotaka, kuwa Iran ishambulie mafuta Saudia halafu iyaishe tu, kwa kutaka kufanya mazungumzo na kuacha kuendelea na vita ya Yemen, na kuacha kushirikiana na Israel na Marekani dhidi ya Iran.

Vita ya Yemen ikiisha kwa ushindi wa Wahuthi, ni wazi kuwa matazamio ya ushindi wa u-Shia yataenezwa katika nchi zilizobaki za Ghuba, ikiwemo Saudia.

Kwa maana hiyo utayari wa Iran kutaka mazungumzo na Saudia na siyo Marekani ni kufurahia ushindi wake, wa kupiga eneo muhimu zaidi la kiuchumi la Saudia bila majibu, halafu tukio hilo limekuja wakati Rais Trump ana mizozo na Bunge.

Kinachoonekana ni kuwa Iran itapata moyo kuwa sera zake zinafanya kazi, na siyo ajabu ikaendelea na sera za kuteka meli kuzuia biashara ya mafuta, kwani mazungumzo na wajumbe wa nchi marafiki kwa niaba ya Saudia, kama Iraq na Pakistan, hayawezi kubadili chochote katika vikwazo.

Utawala wa Teheran utaendelea kubanwa kiuchumi na jeshi lake linataka liendelee kufanya operesheni tofauti kupata mwanya wa kuibana Marekani iondoe vikwazo hivyo linaweza kuisaidia Hezbollah, Hamas au Huthi iinue shambulio kubwa kwa mfano dhidi ya Israel au dhidi ya Saudia tena, halafu Trump akose uvumilivu kabisa.



# Chunya walilia mnunuzi tumbaku

**Na Grace Mwakalinga,**
CHUNYA

WAKULIMA wa tumbaku katika Halmashauri ya Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya wameiomba serikali kuwatafutia mnunuzi mbadala wa TLTC.

Kampuni ya TLTC iliyokuwa inanunua zao hilo imefungasha virago na kuondoka nchini ikiwaacha wakulima bila kujua hatima yao.

Wakizungumza na Nipashe juzi wakulima hao walieleza kuwa mpaka sasa tumbaku imejaa kwenye maghala na hakuna mnunuzi aliyejitokeza, hali inayoendelea kuwatia hofu kwamba huenda msimu ujao wa kilimo wakakosa fedha za kuhudumia mashambani.

Miongoni mwa wakulima hao Pius Lanzala alisema hadi sasa wamebaki njia panda kwani hawajui kama wataendelea na kilimo cha tumbaku au vinginevyo kwa sasa hawana mnunuzi mwingine mkubwa ambaye anaweza kununua mazao yao yakiwa ghalani.

"Tumbaku kwa ukanda wao ndiyo tegemeo katika kuendesha maisha ya familia zao na limewasaidia kujikwamua na umaskini hivyo kuondoka kwa mnunuzi wa kampuni ya TLTC kumeleta mashaka ya namna watakavyoishi," alisema Lanzala.

Hata hivyo, Mbunge wa Lupa (CCM), Victor Mwambalaswa, alisema kuwa atafikisha kilio hicho kwa Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, ili kusaidia kutafuta mnunuzi mwingine mapema iwezekanavyo.

Alisema kukosekana kwa mnunuzi mkuu wa zao hilo kumesababisha upenyo wa madalali na 'makanjanja' kuwalangua wakulima ambao hununua tumbaku hizo kwa bei ya chini.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Maryprisca Mahundi, alisema wanaendelea na jitihada za kutafuta masoko kupitia kampuni na wadau wa tumbaku, huku akitoa onyo kwa madalali kutotumia mwanya huo kuwalangua wakulima.

Alisema zao hilo ni miongoni mwa vyanzo muhimu vya mapato katika wilaya hiyo na kwamba wanafanya kila jitihada kuhakikisha wakulima wanapata mnunuzi wa uhakika. Aliongeza kuwa endapo kilimo cha tumbaku kitasitishwa na wakulima kwa kukosa mnunuzi, Chunya itapata hasara ya zaidi ya Sh. bilioni moja ambazo ni fedha za makusanyo ya ndani zinazotokana na kodi ya zao hilo kwa mwaka.



Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Shinyanga, Anthony Gwandu, akitoa elimu ya usalama barabarani kwa watu wenye ulemavu Shinyanga Mjini jana, ili kuwasaidia kuepukana ajali hasa kwenye maeneo ya vivuko. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Mbunge kuboresha wenye ulemavu

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

IMEELEZWA kuwa watoto wenye ulemavu katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya wanashindwa kuzifikia ndoto zao kielimu kutokana na miundombinu isiyo rafiki.

Hayo yalisema juzi na Mbunge wa Mbeya Vijijini, Oran Njeza, wakati wa mahojiano na Nipashe.

Alieleza kuwa kupitia mfuko wa jimbo katika bajeti ya mwaka 20119/2020 asilimia 80 imeelekezwa kwenye sekta ya elimu kwa ajili ya miundombinu ya vyoo na vyumba vya madarasa na njia maalumu za kutembea wenye ulemavu.

Miundombinu hiyo ni changamoto kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari kwenye maeneo mbalimbali vikiwamo vyoo. Alisema watoto wenye ulemavu hasa wa miguu na mikono wanakabiliwa na changamoto ya kutembea hasa madarasani na vyooni hali inayowalazimu kuomba msaada kwa wengine.

Njeza alisema baadhi ya shule za msingi na sekondari alizozitembelea alibaini madarasa yanayotumika kufundishia si rafiki na watoto hao lakini pia vyoo vilivyojengwa havikuzingatia kundi hilo.

"Tumesisitiza katika ujenzi mpya wa shule lazima uzingatie miundombinu ya watoto wenye ulemavu sambamba na vyumba maalum vya watoto wa kike kujisitiri wakati wa hedhi," alisema Njeza.

Ofisa Elimu Msingi Wilaya ya Mbeya, Shirley Swai, alisema jukumu la kuboresha miundombinu ya elimu ni la kila mwananchi hivyo wanapaswa kuwa mstari wa mbele badala ya kusubiri ruzuku ya serikali.

Alisema serikali imejitahidi kutoa fedha ili watoto wasome bure, lakini kwa muktadha kwamba si kila kitu kitafanywa na serikali badala yake wazazi na walezi wachangie baadhi ya mahitaji ya watoto wao.

Alisema kuwa kwa mujibu wa maelekezo ya serikali ruzuku ilitakiwa itolewe kwa asilimia 100 kila shule, lakini sasa inatolewa kwa asilimia 60 na kati ya hiyo asilimia 40 inatumika kununua vitabu.

"Tukiendelea kuilaumu serikali kwamba haitusaidii tutakuwa tunaikosea kwa sababu ina mzigo mzito wa kuhudumia shule zote hapa nchini, tuhamasishane wenyewe kwa wenyewe ili tuboreshe miundombinu ya shule zetu," alisema Swai.

# Wazazi wapewa tiba ya kudhibiti ngono

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAZAZI na walezi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya wameshauriwa kuanzisha vikundi vya kutoa elimu ya malezi na makuzi kwa vijana wa kiume ili waweze kujitambua na kukabiliana na vishawishi vinavyowatumbukiza kwenye ngono.

Ushauri huo ulitolewa na mtaalamu wa jenda na uchumi kutoka Shirika la TGNP- Mtandao, Rebeka Mrema, wakati akizungumza na wanavituo vya taarifa na maarifa kutoka kata saba zinazofanya kazi na mtandao huo wilayani Mbeya.

Alisema nyakati za sasa vijana wengi wa kiume wameingia kwenye mahusiano ya kingono na wanawake waliowazidi umri na matokeo yake wanapoteza dira ya maisha yao, kutumikishwa kingono na kupata maambukizi ya VVU na Ukimwi.

Rebeka alidai ili kukomesha tabia hiyo wazazi waanzishe vikundi mbalimbali vya kutoa elimu ya malezi na jinsia ili vijana hao waepukane na vishawishi watakavyokutana navyo.

"Zipo sababu mbalimbali zinazosababisha vijana hao kujiingiza kwenye mahusiano hayo ikiwamo uvivu wa kufanya kazi, tamaa ya kuwa na maisha mazuri pamoja na umaskini, matokeo yake wanapoteza dira," alisema Mrema.

Aliongeza, "baadhi ya vijana wetu wa kiume siku hizi wanapenda 'umarioo', hawajishughulishi na kazi yeyote wanasubiri wawapate wamama ili wawalee kazi yao kubwa ni kushinda ndani tu wakisubiriwa waletewe kila kitu," alisema Mrema.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti baadhi ya wazee kutoka katika kata ya Igale walisema tabia hiyo ya vijana kujihusisha na ngono na wanawake waliowazidi umri inatokana na misingi waliyojengewa katika familia zao.

Mmoja wao Uswege Mwashibanda alisema baadhi ya wazazi wamekuwa chanzo cha kusababisha vijana wao kuanzisha mahusiano na wamama kwa madai ya kutokemea pindi wanapoona hali hiyo.

"Kijana wetu aliingia kwenye mahusiano na `jimama' ambaye alikuwa mwalimu wa shule ya msingi ana umri wa miaka 75 sasa familia ilimruhusu kuishi na mwalimu huyo kwa lengo la kusoma masomo ya ziada ya jioni matokeo yake alianzisha uhusiano wa kimapenzi ambao umemgharimu mpaka sasa ameshindwa kutimiza ndoto zake za kusoma," alisema Mwashibanda.

Lydia Mwakalinga alifafanua kuwa mbali na kuanzisha vikundi vya kutoa elimu ya malezi na makuzi lakini serikali inatakiwa kutoa elimu ya ujasiriamali na mikopo ili waepukane na tamaa ambazo wanazipata kwa kinamama hao.





# Waziri Jafo atangaza kufuta halmashauri 31

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imetangaza nia ya kufuta halmashauri zote zitakazoshindwa kuhamia kwenye jengo lake la utawala ndani ya siku 30.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, alisema halmashauri yoyote itakayozembea kuhamia kwenye eneo lake la utawala ndani ya siku 30, itafutwa mara moja.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini cha Ofisi ya Tamisemi, ilizitaja halmashauri 31 ambazo ofisi zake zipo nje ya maeneo yao ya utawala, hivyo zinapaswa kuzihamishia kwenye maeneo yao, ndani ya mwezi mmoja kuanzia Jumatatu wiki hii.

"Hatua hii ya waziri imetokana na maelekezo ya Rais John Magufuli, kuhusu halmashauri zinazotekeleza majukumu yake nje ya maeneo yake ya utawala ambazo zimeagizwa kuhamishia shughuli zao ndani ya majengo yao," ilisema.

Taarifa ya Tamisemi ilizitaja halmashauri hizo kuwa ni Arusha, Kondoa, Geita, Iringa, Mufindi, Bukoba, Mpanda, Kasulu, Kigoma, Moshi, Lindi, Babati, Mbulu, Musoma na Bunda.

Zingine ni Tarime, Mbeya, Kilombero, Mtwara, Masasi, Newala, Njombe, Kibaha, Sumbawanga, Mbinga, Shinyanga, Bariadi, Singida, Nzega, Korogwe na Handeni.

Maagizo hayo ya serikali yameanza kutekelezwa kuanzia juzi Oktoba 7, 2019.



Msimamizi wa maduka kampuni ya Vodacom Kanda ya Kati, Suzana Mwaipopo (kulia), akiwagawia zawadi wananchi wa Wilaya ya Bahi, mkoani Dodoma jana, baada ya kuzindua duka la kampuni hiyo, kama sehemu ya maadhimisho ya Wiki ya Huduma kwa Wateja. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## DC ataka watoe EFD

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Katambi, amewataka wafanyabiashara jijini Dodoma kutekeleza maagizo ya Mamlaka ya Mapato (TRA) ya kutumia mashine za kutoa risiti za kielektroniki (EFDs).

Katambi aliyasema hayo jijini Dodoma wakati wa ziara ya kushtukiza kwa wafanyabiashara wa maduka na wale wadogo ambao wanatumia vitambulisho.

Mkuu wa Wilaya alisema hakuna sababu ya wafanyabiashara kuwakimbia na kuacha biashara zao kinachotakiwa ni kutekeleza agizo la utumiaji mashine hizo ikiwamo kutoa risiti kwa mteja ambaye amenunua bidhaa hizo.

"Naomba mtumie mashine za EFDs mkifanya hivyo mtakuwa mmerahisha hata ufanyaji biashara zenu," alisema Katambi.

Aidha, Meneja Msaidizi wa ukusanyaji madeni, TRA Dodoma Castro Angelo, alisema wameamua kufanya zoezi hilo la ukaguzi wa risiti za mashine za EFD ili kuwataka watu wafanye biashara kihalali na kuiingizia serikali mapato.

Alisema hakuna sababu kwa wafanyabiashara kukimbia pale wanapowaona TRA, wanakuja katika biashara zao kinachotakiwa ni kusubiri kupatiwa elimu ya matumizi ya EFD mashine kwa wanunuzi wa bidhaa zao.

"Kuna maduka mengine tumeenda tumekuta kuna watoto ndio wamewaachia maduka, huku wenyewe wakionekana kutukimbia," alisema Angelo.

Alisema hakuna sababu ya wao kuendelea kukimbia bali wanapaswa kubaki dukani kueleza changamoto zinazopelekea washindwe kutekeleza maagizo ya TRA.

# Waomba kupunguziwa gharama ya vifungashio

**Na Peter Mkwavila,** CHAMWINO

WAJASIRIAMALI wenye ulemavu wameiomba serikali kuwapunguzia gharama ya vifungashio vya bidhaa wanazozalisha ili waweze kutimiza azma ya kuwa sehemu ya Tanzania ya viwanda.

Ombi hilo lilitolewa jana na watu wenye ulemavu wanaojihusisha na ujasiriamali wilayani Chamwino wakati wa mafunzo yaliyotolewa taasisi isiyo ya kiserikali ya Nakua na Taifa Langu.

Mmoja wa wajasiriamali hao, Mariam Sangula, alisema gharama kubwa iliyopo kwenye vifungashio vya bidhaa wanazotengeneza, itakuwa ni ndoto kujikwamua kiuchumi kama serikali inavyotaka.

"Tunaiomba serikali kupitia wizara husika kutoa punguzo kwa makundi haya ya watu wenye ulemavu ili waweze kumudu utengenezaji wa bidhaa kwa ubora unaokubalika na hatimaye wafikie ndoto ya kuwa sehemu ya uchumi huu wa viwanda," alisema Sangula.

Alibainisha kuwa kutokana na gharama kubwa wanashindwa kutengeneza bidhaa ambazo wataweza kuziingiza kwenye ushindani wa masoko.

Kwa upande wake, Diwani wa Kata ya Buigiri, Keneth Yindi, alisema ili makundi hayo yafanikiwe serikali haina budi kuyaunga mkono.

Alisema kuwa pamoja na ukubwa wa gharama za vifaa mbalimbali vikiwamo vifungashio, makundi hayo ili kujinasua wanatakiwa kuungana kwa pamoja kwenye vikundi na wawezeshwe kupata mikopo itakayowafikisha kwenye hatima yao na kumudu kukabiliana na changamoto.

Alisema kuwa mafunzo hayo yametolewa ili kutatua changamoto ya utegemezi kwa watu hao ili waweze kujikwamua kiuchumi.

"Hili ni muhimu kwa upande wao waunde vikundi vitakavyowawezesha kupata mikopo," alisema.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Nakua na Taifa Langu, Jessica Mshama, alisema kuwa makundi hayo ya watu wenye ulemavu takribani 200, yamejifunza namna ya utengenezaji wa bidhaa za ujasiriamali kwa vitendo ikiwamo kufungasha ubuyu na karanga na mafuta ya alizeti.



# 'Ambulance' ya boti kuzinduliwa leo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI imeanza kuchukua hatua za kudhibiti vifo vya wazazi na watoto na leo itazindua matumizi ya boti ya kuhudumia wajawazito na wazazi visiwa kikiwamo kisiwa cha Gando kilichoko Pemba.

Aidha, pamoja na boti, itazindua mpango mkakati wa kupunguza vifo vya kinamama na watoto wachanga vitokanavyo na mambo yanayohusiana na uzazi.

Akitoa taarifa kwa wanahabari kuhusu hatua hizo, Naibu Waziri wa Afya, Harusi Suleiman, alisema mpango huo utasaidia kupunguza vifo vya kinamama na watoto nchini.

Naibu Waziri alisema katika mpango mkakati huo serikali inazindua boti mpya ya kusafirisha wagonjwa (ambulance boat) ambayo itatoa huduma za usafiri kwa mama wajawazito kufika kwa wakati hospitali.

Alisema boti hiyo itafanya kazi katika visiwa vidogo vilivyopo Pemba ikiwa ni pamoja na kisiwa cha Gando kuwaondoshea usumbufu wanaoupata wazazi wa visiwa hivyo wanapohitaji kujifungua. Alisema zaidi ya Sh. milioni 200 zimetumika kununulia boti hiyo na kuwataka wananchi kuitunza na kuitumia kwa malengo yaliyokusudiwa ili kuendeleza juhudi za serikali katika kupambana na vifo vya mama na watoto wachanga. Hatua hiyo inachukuliwa kutokana na kutoridhika na idadi kubwa ya wanawake na watoto wanaokufa kutokana na uzazi. Alisema mpango huo utakwenda sambamba na uzinduzi wa mkakati wa miaka mitano wa afya ya uzazi ya mama na mtoto ambao utajumuisha upatikanaji wa huduma muhimu kama vifaa vya matibabu na watoa huduma za afya.

Alisema malengo ya serikali ni kupunguza vifo vya kinamama na watoto wachanga ifikapo mwaka 2023, ili kuimarisha ustawi wa mama na mtoto nchini.

balimbali zinazochukuliwa na serikali lakini bado idadi ya vifo imekuwa tatizo kutokana na baadhi ya wazazi kutohudhuria kliniki kwa wakati na wengine kuendelea kujifungulia nyumbani.

Alisema takwimu zinaonyesha kwamba kila mwaka wastani wa wajawazito wengi hufariki kwa matatizo ya uzazi hali ambayo inarejesha nyuma jitihada za kumaliza tatizo hilo nchini.

Kwa upande wake Mratibu wa Afya ya Uzazi na Mtoto, Wanu Bakari Khamis, aliwataka wazazi kuhudhuria kliniki kwa wakati ili kupata elimu ya kujihudumia pamoja na kumlinda mtoto akiwa tumboni.

Alisema takwimu za serikali za mwaka 2015-18 zinaonyesha kuwa mama wajawazito 377 hufariki dunia katika vizazi hai 100,000 na kwamba lengo la serikali ifikapo mwaka 2023 idadi hiyo kushuka hadi kufikia wazazi 130 kati ya vizazi hai 100,000.

Ofisa Uhamasishaji Kitengo Shirikishi Afya ya Mama na Mtoto, Kassim Issa Kirobo, aliwataka kinababa kutoa huduma stahiki kwa wajawazito ili kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi.

"Iwapo kinababa hawatotoa huduma stahiki kama lishe kwa wajawazito watoto watakaozaliwa tutawakosa," alisema.

Mpango mkakati huo pamoja na boti ya wagonjwa wa dharura wa visiwani utazinduliwa leo na kauli mbiu yake "Wajibika, Hakikisha Uzazi Salama".



Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe Juma, akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Msingi Mkunazini, mjini Zanzibar jana, wakati alipofika kukagua uchakavu wa shule hiyo. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mwakilishi aijengea serikali sekondari

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MWAKILISHI wa kuteulia, Ahmada Yahya Abdulwakili, ametangaza nia ya kujenga shule ya sekondari ya mchepuo wa biashara ambayo ikimalizika anaikabidhi serikali.

Alisema anajenga shule hiyo ambayo ni sadaka yake kwa Wazanzibari pamoja na watoto na kwamba ni jambo la kihistoria analotaka kuiachia nchi yake.

Abdulwakili, alisema aliamua kujenga shule ya sekondari ya biashara kutokana na kuvutiwa na kazi kubwa ya Rais wa Zanzibar Dk. Ali Mohamed Shein, anayofanya katika kuimarisha sekta ya elimu tangu alipoanza kuiongoza nchi mwaka 2010, hivyo anapenda kumuunga mkono.

Alisema hayo alipokuwa akizungumzia maendeleo ya ujenzi wa shule hiyo unaoendelea katika Mtaa wa Mombasa kwa Mchina Mjini Zanzibar. Alieleza kuwa unaelekea kukamilika.

"Nimeguswa na maendeleo makubwa yanayoendelea katika sekta ya elimu chini ya uongozi wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Shein, nimeona kuweka kitu cha historia katika maisha." Alisema.

Abdulwakili ambaye ni mfanyabiashara maarufu Zanzibar, alisema shule hiyo itakuwa na uwezo wa kusomesha watoto 600.

Alisema amechagua biashara kwani ina umuhimu mkubwa kwa wanafunzi Zanzibar, wakati huu inapoendelea kutekeleza mpango wake wa kuelekea katika uchumi wa kati na wa viwanda.

Aidha, alisema kukamilika kwa ujenzi wa shule hiyo pia kutasaidia kupunguza tatizo la msongamano wa wanafunzi katika baadhi ya shule za sekondari za Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja.

"Alisema Rais Shein tangu kuingia madarakani amefanya kazi kubwa kwa kuimarisha sekta ya elimu, kujenga shule za kisasa za ghorofa katika visiwa vya Unguja na Pemba.

"Shule hii nimeamua kutoa sadaka yangu baada ya kugusswa na maendeleo makubwa ya sekta ya elimu yanayoendelea kuonekana Zanzibar," alisema mwakilishi huyo.

Alisema kuwa baada ya ujenzi kukamilika wa ataikabidhi Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa ajili ya kuratibu na kuendeshaji.

Aidha, alisema mkakati wa serikali wa kuondoa upungufu wa madawati kwa wanafunzi Zanzibar, umeanza kuonyesha tija tangu kuundwa kamati ya kuondoa tatizo baada ya madawati kuanza kusambazwa katika shule za Unguja na Pemba.

Kwa wanafunzi wa shule hiyo ya biashara walisema wingi wa wanafunzi madarasani unaotokana na uhaba wa vyumba vya madarasa ambao umekuwa changamoto kwao katika kupata elimu.

"Tunampongeza Mwakilishi Abdulwakili ambaye amejitolea kujenga ghorofa kwa ajili ya shule hii ya biashara tunawaomba na wafanyabiashara wengine kuiga mfano wake na ambaye pia ni mfanyabiashara na mtumishi wa wananchi," alisema Ali Juma mwanafunzi wa shule hiyo.

## Serikali, Mji Mkongwe kukarabati shule

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe Juma, ameitaka Mamlaka ya Uhifadhi na Uendeshaji wa Mji Mkongwe kushirikiana na wizara yake kuzifanyia matengenezo shule zilizochakaa.

Shule hizo ni zile zilizopo ndani ya hifadhi ya mji huo ili kuweka usalama wa wanafunzi wanaosoma katika taasisi hizo.

Akizungumza wakati wa ziara ya kuangalia hali ya uchakavu wa shule ya msingi za Mkunazini Mjini Unguja, alisema kutokana na uchakavu wa shule hiyo ni lazima mamlaka ya hifadhi ya mji huo, kuchukua hatua za haraka kuandikia ripoti ya utekelezaji kwa lengo la kuweza kuifanyia kazi ili kuepusha maafa yasije kutokea.

Alisema Wizara ya Elimu Zanzibar, itashirikiana na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa, Idara Maalum na Vikosi vya SMZ, ili kuifanyia matengenezo kwa haraka.

Alisema serikali inaendelea kutekeleza ahadi zake kwa kuhakikisha wanafunzi wanapata elimu katika mazingira bora na salama.

Aidha, aliwataka walimu na wasimamizi wa shule za serikali kuzitumia ruzuku za kila mwezi wanazopatiwa kutoka serikalini kwa kufanya matengeneo madogo ya shule, ili kupunguza athari kuwa kubwa zaidi.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe, Issa Saliboko Makarani, alisema Shule ya Mkunazini itafanyiwa marekebisho na ukarabati.

Ofisa takwimu za elimu kutoka Baraza la Manispaa Mjini, Haji Ali Amour, alisema uchakavu wa jengo la Shule ya Mkunazini, umeshagundulika na umeingizwa kwenye bajeti ya mwaka 2019-2020 kwa ajili ya kufanyiwa ukarabati.

# Lukuvi abana fedha za maadhimisho

**Na Munir Shemweta,** WANMM

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, ameahirisha sherehe za maadhimisho ya Siku ya Makazi Duniani na kuagiza fedha iliyopangwa kwa ajili ya sherehe hiyo Sh. milioni 23 kutumika kuboresha mfumo wa mapato na utoaji huduma za ardhi.

Katika salamu zake za Siku ya Makazi Duniani yenye kauli mbiu 'Matumizi ya Teknolojia Bunifu Kubadili Taka kuwa chanzo cha Mapato', Lukuvi ametaka maadhimisho ya mwaka huu kutofanyika sherehe na badala yake yatumike kutafakari kauli mbiu na kujipanga upya kutekeleza agizo la Rais alilolitoa muda mrefu la kuwataka wananchi kujitolea kufanya kazi za usafi katika maeneo ya miji na wanayoishi.

Kwa mujibu wa waziri huyo, kauli mbiu ya maadhimisho ya mwaka huu inaelekeza kutafakari kwa kina namna changamoto ya uwapo wa taka mijini kuwa fursa ya kujiongezea kipato kwa kutumia teknolojia rahisi.

Alisema mwaka huu inaelekezwa kuingia kwa undani zaidi kutumia ubunifu kubadili taka kuwa mtaji na kuongeza kipato kwa wananchi bila kuathiri afya za wakazi wa mijini na mazingira na hatimaye kupunguza gharama za udhibiti taka.

"Mamlaka za miji zina wajibu wa kukusanya taka kama mojawapo ya huduma wanazotakiwa kuzitoa kwa wananchi na kwa upande mwingine wananchi wanao wajibu wa kulipia huduma hiyo kwa mujibu wa sheria iliyoanzisha mamlaka za mitaa," alisema Lukuvi.

Aliwaasa wananchi kuepuka kutupa taka kando ya mito, maeneo ya wazi, barabarani na katika mitaro ya maji ya mvua kwa kuwa kufanya hivyo kunasababisha uharibifu wa mazingira, kuziba kwa mitaro ya maji ya mvua na kutengeneza mafuriko.

Aidha, amealika wadau wote wenye teknolojia rahisi ya kuchakata taka ngumu kushirikiana na mamlaka za miji nchini ili kutumia ujuzi huo kupambana na changamoto ya wingi wa taka ngumu na kwa njia hiyo wataweza kutengeneza ajira kwa jamii, huku miji ikiendelea kuwa safi na afya za wananchi kuimarika.



Mkurugenzi wa Masoko na Ukuzaji Biashara wa Benki ya TPB, Deo Kwiyukwa (kushoto), akifafanua jambo kwa mteja aliyetembelea tawi la Kijitonyama, Ansilla Chingwi Settebe (katikati), wakati wa madhimisho ya Wiki ya Huduma kwa Wateja, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Meneja wa Tawi hilo, Emmanuel Kimola. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Shirika lasaidia afya macho kwa bil. 5.6/-

**Na Beatrice Philemon**

SHIRIKA la Kimataifa la Sightsavers Tanzania imezindua mradi wa miaka mitatu ili kuweka usawa katika huduma za afya ya macho kwa kuwafikia watu wote wakiwamo watu wenye ulemavu na wasio na ulemavu hapa nchini.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi Mkazi wa Sightsavers Tanzania, Gosbert Katunzi, wakati wa uzinduzi wa mradi wa Boresha Macho utakaotekelezwa katika mkoa wa Morogoro na Singida.

Alisema mradi wa miaka mitatu unaojulikana kama ' Boresha Macho Project' uliofadhiliwa na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Uingereza (DFID) ambalo limetoa Paundi milioni 2 (Sh. bilioni 5.6) kwa Sightsavers Tanzania ili kutekeleza upimaji macho, kufanya upasuaji wa mtoto wa jicho kwa wagonjwa na kutoa msaada wa miwani kwa watu wenye uono hafifu.

Akisema katika mkoa wa Morogoro, mradi huu utakelezwa katika halmashauri tano na mkoa wa Singida mradi huu utatekelezwa katika halmashauri saba.

"Mpaka mwisho wa mradi huu, tunatarajia tutapima macho watu 150,000, zaidi ya watu 13,500 watapata upasuaji wa mtoto wa jicho, zaidi ya watu 6,000 watapa miwani na zaidi ya watu 500 watapata mafunzo wakiwamo watumishi wa afya nao watapata mafunzo ya kuwawezesha kutoa huduma ya macho kwa ufanisi zaidi," alisema. Alishukuru DFID kwa kuwapatia fedha hizo ili kusaidia wananchi wa Tanzania mikoa ya Morogoro na Singida ili kutoa matibabu kwa watu wenye matatizo ya macho, kuboresha huduma ya afya ya macho na kusaidia watu kuona tena ili waweze kufanya shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii.

Fedha hizo zitasaidia kufikia watu wengi zaidi wenye uhitaji, kusaidia watu kupata huduma bora ya macho, kuboresha huduma ya macho na kushughulikia vyanzo au visababishi vinavyosababisha upofu.

Mradi huu utahakikisha huduma ya afya ya macho inapatikana kwa kila mtu na aliomba taarifa hizi ziwafikie walengwa katika kila eneo ambapo mradi huu unatarajiwa kutekelezwa ili kila mtu aweze kupata matibabu ya huduma ya afya ya macho kwa usawa ikiwamo kinamama, wazee na watu wenye ulemavu.

"Tunajua kuwa huduma ya afya ya macho bado haijawafikia watu wengi zaidi wenye uhitaji katika mikoa ya Morogoro na Singida na upasuaji wa mtoto wa jicho utasaidia maelfu ya wananchi kuona tena na wengine ambao hawakupata huduma ya upasuaji kupata miwani," alisema.

Alisema katika utekelezaji wa mradi huu wadau wakuu katika mradi huu ni Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Tamisemi, Shirikisho la Vyama vya Watu wenye Ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA), Singida Saidia Wazee Tanzania, Chama cha Wazee Mkoa wa Morogoro na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP).

Naye Katibu Tawala Msaidizi, Mkoa wa Morogoro, Noel Kazimoto, aliishukuru DFID kwa kushirikiana na Sightsavers Tanzania kwa kupeleka mradi huo mkoani humo, ambao utabadilisha maisha ya watu.

# Wakulima mwani waibua malalamiko

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

WAKULIMA wa mwani shehia ya Kiungoni Wilaya ya Wete Pemba, wameiomba serikali kufanya utafiti wa kina juu ya soko la kuuzia mwani kimataifa, ili wajue jinsi ya kupambana nalo na kujipatia kipato cha kuridhisha.

Walisema , wamekuwa wakilima kilimo hicho kwa muda mrefu sasa, ingawa bado soko limekuwa ni kikwazo kikubwa kwao, kutokana na bei ndogo wanayouzia, ambayo huzorotesha shughuli zao za kilimo cha mwani.

Walieleza kuwa, iwapo serikali itafanya utafiti wa kina kuhusu soko la kuuzia mwani kimataifa na kujua kitu kinacholifanya soko hilo kuwa la kiwango cha chini ili kusaidia wakulima hao kujua kiwango kinachohitajika na kuweza kupambana na soko hilo na kujipatia kipato cha kuridhisha.

Chumu Ali Hamad alisema ni vyema kwa serikali kusimamia kwa kulifanyia uchunguzi jambo hilo, ili kuwarahisishia wakulima kujua kiwango kinachotakiwa na kujua bei za kimataifa, jambo ambalo litaweza kuwasaidia kujikwamua na umaskini.

"Tumeamua kulima kilimo hiki ili tujikwamue na maisha duni yanayotukabili, lakini bado bei ya mwani inatuumiza vichwa, kwani kazi ni kubwa na kipato kidogo," alisema Chumu.

Fatma Salum Hamad, alieleza kuwa wanahitaji vihori, kamba na viatu vitakavyowasaidia kurahisisha shughuli zao za kilimo cha mwani.

"Pamoja na changamoto hizo, lakini bado tunajituma kwa kilimo hicho kwani hatuna njia nyingine ya kufanya, tunaiomba serikali itusaidie kwani wananchi wake tunateketea," alieleza.

Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Uvuvi Pemba, Sharif Mohamed Faki, alisema jambo linalosababisha soko kuwa la kiwango cha chini duniani ni kutokana na kuwapo kampuni mbili tu za kununulia mwani, jambo ambalo linakosa ushindani kwani wanapanga wenyewe bei wanayoitaka.

"Kwa kweli bei ya soko la dunia ni ya kiwango cha chini, ambapo kampuni hupanga bei wenyewe, hali iliyopelekea wakulima kulalamikia soko kila siku, naamini kungekuwa na masoko mengi basi bei ingekuwa kubwa," alisema Mkuu huyo.

Alieleza kuwa, pia ukosefu wa ofisi maalumu ya kununulia mwani inasababisha kuwapo kwa bei ndogo, kutokana na gharama za usafirishaji kuwa ni kubwa kwa wanunuzi wa mwani.

Naye Meneja wa kampuni ya kununulia mweni tawi la Pemba 'ZANQUE AQUE FARMS', Issa Khamis Mohamed, alisema wanalazimika kununua mwani kwa bei ndogo kulingana na soko la Dunia kuwa wanapanga bei wenyewe kwa kuangalia zaidi gharama zao.

"Kwa kweli kipato ni kidogo kwa wakulima na hata sisi wanunuzi, kwani sasa hivi kilo ya mwani ni Sh. 500, jambo ambalo linazorotesha maendeleo ya kilimo hicho," alisema.

Aliwataka wakulima wa mwani wasivunjike moyo na waendelee kulima kilimo hicho kwa wingi, ili kupata kipato cha kutosha, kwani licha ya bei ndogo lakini iwapo watalima kwa wingi watajiongezea fedha zitakazowasaidia kujikwamua kimaisha.

HABARI KIMATAIFA

# Bibi harusi afa maji akipiga 'selfie'

**NEW DELH,** India

WANANDOA wawili na watu wengine watatu wa familia moja wamekutwa wamefariki katika bwawa la maji baada ya kujaribu kujipiga picha ya selfie.

Maofisa wa polisi kutoka Jimbo la Kusini mwa India la Tamil Nadu wamethibitisha kutokea kwa tukio hilo.

Taarifa iliyotolewa na Jeshi la Polisi ilieleza kuwa waliofariki ni miongoni mwa watu sita walioshikana mikono na kusimama katika kina kirefu cha maji karibu na bwawa la Pambar kabla ya mmoja wao kuteleza na kujaribu kumwokoa mwengine.

**Mume wa mwanamke huyo aliweza kumwokoa dada yake, lakini wengine walifariki. India ina idadi kubwa ya watu wanaofariki kutoka na vifo vya 'selfie'.**

Mume wa mwanamke huyo aliweza kumwokoa dada yake, lakini wengine walifariki. India ina idadi kubwa ya watu wanaofariki kutoka na vifo vya 'selfie'.

Tukio hilo lililotokea siku ya Jumapili katika Jimbo la Tamil Nadu wakati wanandoa hao wakitoka eneo la Bargur walikuwa wakiwatembelea ndugu zao walioko katika eneo la Uthangarai.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa watatu hao waliingia katika maji hayo wakiwa na vijana watatu wa familia moja kabla ya mmoja wao mvulana mwenye umri wa miaka 14 kuteleza na kuwashika dada zake wawili mmoja wao akiwa na miaka 18 na mwingine wa miaka 19, pamoja na wanandoa hao wawili na dadake bwana harusi.

Dada huyo alivutwa na ndugu zake lakini wengine wanne wakapotea ndani ya maji. Maofisa wa polisi wanasema kwamba miili yao baadaye ilipatikana na uchunguzi unaendelea.

Tukio hilo ni mojawapo mwa matukio la kupiga 'selfie' nchini India. Wataalamu walionya kwamba watu wanafanya hatari ili kuwafurahisha watu wa familia zao katika mitandao ya kijamii.

Kulingana na utafiti uliofanywa na Shirika la Maabara ya Tiba nchini Marekani kati ya mwaka 2011 na 2017 India iliripoti vifo vya watu 259 ikifuatiwa na Urusi, Marekani na Pakistan.

Katika Jimbo la Haryana Mei, vijana watatu waliokuwa wakipiga picha za selfie katika reli waliruka kutoka katika njia ya treni walipoona gari moshi likikaribia walikokuwa, kabla ya kugongwa na treni lingine liliokuwa linatokea kutoka upande mwingine wa reli.

Mwaka 2017, Jimbo la India la Karnataka lilizindua kampeni ya kuwaonya watu kwamba selfie zinaweza kuua baada ya kifo cha wanafunzi wanne. **BBC**



Askari wa kundi la wapiganaji la Al Shabaab akiwa amebeba silaha. **PICHA: AFP**

## Mchungaji akamatwa kisa kuvuruga amani

**KIGALI,** Rwanda

MUHUBIRI raia wa Marekani, Gregg Schoof ambaye alitarajiwa kufanya kikao na waandishi wa habari mjini Kigali, amekamatwa na polisi mjini humo kwa madai ya kuvuruga utulivu.

Polisi ya Rwanda ilimkamata mhubiri huyo ambaye alitarajiwa kufanya kikao na waandishi wa habari mjini Kigali jana na ambaye kituo chake cha redio nchini humo kilifungwa na mamlaka mwaka jana.

Msemaji wa Jeshi la Polisi nchini Rwanda, John Bosco Kabera alieleza kuwa Schoof alikamatwa kwa kosa la kuvuruga utulivu.

Maofisa nchini Rwanda mwaka jana walikifunga kituo cha redio kilichomilikiwa na Schoof, cha Amazing Grace baada ya kurusha hewani mahubiri ambayo wanaharakati wa haki za wanawake walisema yalieneza chuki dhidi ya wanawake.

Mahubiri hayo yaliwaelezea wanawake kuwa watu wabaya sana.

Schoof alitaka kuwahutubia wanahabari kabla ya kuondoka nchini humo lakini akakamatwa na polisi katika sehemu ambayo kikao hicho cha wanahabari kilitarajiwa kufanyika. Alikabidhiwa kwa Idara ya Upelelezi ya Rwanda ili kuhojiwa zaidi. **DW**

## Hofu yatanda kuibuka tena IS

**DAMESKI,** Syria

TAHARUKI imetanda kwa washirika wa Marekani wa Kikurdi baada ya jeshi la nchi hiyo kuondoka nchini Syria, huku Uturuki ikiwa inajiandaa kuanza operesheni ya kijeshi.

Kwa muda wa miezi kadhaa Rais wa Uturuki, Recep Tayyip Erogan, amekuwa anatishia kupeleka majeshi yake katika nchi jirani ya Syria.

Mwanzoni mwa wiki Rais huyo alisema ataitekeleza hatua hiyo kwa kuwapeleka askari wa anga na wa nchi kavu kwa lengo la kutenga ukanda wa usalama kwenye mpaka kati ya Uturuki na Syria.

Lengo la Rais Erdogan ni kuyarudisha nyuma majeshi ya Wakurdi wa Syria yanaoongozwa na kundi la YPG.

Hata hivyo, Uturuki inayaona majeshi hayo kuwa ni tishio kwa usalama wa taifa lake ambapo majeshi hayo ya Wakurdi ndiyo yaliyoshirikiana na majeshi ya Marekani katika harakati za kupambana na kuwashinda wapiganaji wanaojiita dola la kiislamu la IS. Marekani imekuwa inatafuta suluhisho la kuiridhisha Uturuki na wakati huohuo ikijaribu kuyazingatia maslahi ya Wakurdi.

Hata hivyo, mkakati huo haukufua dafu na badala yake Rais wa Marekani, Donald Trump siku ya Jumapili alitangaza hatua ya kuyaondoa mara moja majeshi ya Marekani yaliyokuwa yanashirikiana na majeshi ya Wakurdi.

Jana, majeshi ya kidemokrasia ya Syria SDF yalithibitisha kuanza kuondoka kwa majeshi ya Marekani kutoka kwenye eneo lililokuwa linadhibitiwa na majeshi ya Wakurdi.

Pamoja na hayo, Marekani imesema kwamba majeshi yake hayatayalinda majeshi hayo ya SDF ikiwa majeshi ya Uturuki yataivamia sehemu hiyo ya kaskazini mwa Syria.

Wachambuzi wa masuala ya siasa wameeleza kuwa uamuzi wa Rais Erdogan utasababisha maafa siyo tu kaskazini mwa Syria na kwenye ukanda huo bali duniani kote.

Idadi kubwa ya wapiganaji wanaojiita dola la kiislamu pamoja na wale wanaowaunga mkono wanashikiliwa kwenye kambi za Wakurdi Kaskazini mwa Syria. Mbunge wa chama cha CDU nchini Ujerumani, Roderich Kiesewetter alitahadharisha juu ya hatari ya wapiganaji hao kukimbilia nchini Irak. Alisema jambo hilo litahatarisha usalama wa dunia.

Mbunge huyo pamoja na wanasiasa wengine wa Umoja wa Ulaya (EU) wanahofia kuimarika kwa wapiganaji wa IS baada ya Marekani kuyaondoa majeshi yake na pia kutokana na uamuzi wa Rais Erdogan wa kuivamia Syria Kaskazini.

Kamishna wa EU, Kocijancic alisema ingawa jumuiya hiyo inayatambua maslahi ya Uturuki lakini inaunga mkono mamlaka ya Syria juu ya mipaka yake.

Alieleza kuwa hatua ya Uturuki ya kuivamia sehemu ya kaskazini mwa Syria haina uhalali.

Kamishna huyo alisema mapigano mapya Kaskazini Mashariki mwa Syria yataleta maafa makubwa zaidi kwa raia pamoja na kusababisha idadi kubwa ya wakimbizi wa ndani na kuvuruga juhudi za kuleta amani zinazoungwa mkono na EU. Mjumbe wa Baraza la Uhusiano wa Nje EU, Julien Barnes-Dacey, alitahadharisha kwamba Uturuki haijaandaa mipango yoyote endapo magaidi wa dola la Kiislamu wataibuka tena.

Mjumbe huyo alisema Uturuki inalenga kuhakikisha kwamba majeshi ya Wakurdi yanaondolewa Kaskazini Mashariki mwa Syria.

Maalfu ya wapiganaji wanaojiita dola la kiislamu kutoka Ulaya bado wanashikiliwa kwenye kambi za Wakurdi, baadhi yao ni raia wa Ujerumani. **DW**

HABARI KITAIFA

# Sababu kushuka mfumuko bei

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MFUMUKO wa bei kwa mwaka ulioishia Septemba 2019 umepungua na kufikia asilimia 3.4, huku bidhaa zisizo za vyakula ikiwamo petroli na dawa ya kuulia wadudu nyumbani zikitajwa kuchangia hali hiyo.

Hayo yalisemwa jana na Kaimu Mkurugenzi wa Sensa ya Watu na Jamii, Ruth Davison, alipokuwa akizungumza na wanahabari kuhusu mfumuko wa bei.

Alisema mfumuko huo kwa Septemba umepungua kutoka asilimia 3.6 kwa mwaka ulioishia Agosti, mwaka 2019.

"Hii inamaanisha kasi ya mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma kwa mwaka ulioishia Septemba 2019, imepungua ikilinganishwa na kasi iliyokuwapo kwa mwaka ulioishia Agosti, 2019," alisema.

Davison alisema kushuka kwa mfumuko huo kumechangiwa hasa na kupungua kwa bei za bidhaa zisizo za vyakula.

Alitaja bidhaa hizo ni mafuta ya taa kwa asilimia moja, petroli (3.3), majiko ya gesi (1.5), dawa za kuulia wadudu nyumbani (2.2) na mafuta ya nywele (1.3).

Hata hivyo, alisema mfumuko wa bei wa bidhaa za vyakula na vinywaji baridi kwa mwaka ulioishia Septemba 2019, umeongezeka hadi asilimia 4.0 kutoka asilimia 3.7 kwa mwaka ulioishia Agosti, 2019.

Akizungumzia hali ya mfumuko kwa nchi za Afrika Mashariki, alisema Kenya mfumuko wa bei kwa mwaka ulioishia Septemba 2019 umepungua hadi asilimia 3.83 kutoka asilimia 5.00 kwa mwaka ulioishia Agosti, 2019.

"Kwa upande wa Uganda mfumuko wa bei kwa mwaka ulioishia Septemba 2019 umepungua hadi asilimia 1.9 kutoka asilimia 2.1 kwa mwaka ulioishia Agosti, 2019," alisema.



Ofisa Rasilimali Watu wa Kiwanda cha Bia cha TBL Tawi la Mwanza, Dora Nyambalya, akiwakabidhi taulo za kike walimu wa Shule ya Sekondari Mtoni, Rhoda Magesse na Jacqueline Joseph (kushoto), zilizonunuliwa kutokana na michango ya wafanyakazi kwa ajili ya wasichana wa shule za sekondari. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Takukuru yataja vinara rushwa

**Na Beatrice Shayo**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Temeke imesema taasisi zilizoongoza kulalamikiwa kwa vitendo vya rushwa ni Manispaa ya Temeke, Mahakama, Polisi, Ofisi za Serikali za Mitaa na Mabaraza ya Ardhi.

Kadhalika, Takukuru imeeleza kupokea taarifa 58 zinazohusiana na vitendo vya rushwa na baada ya kuzifanyia kazi wamefanikiwa kuokoa zaidi ya Sh. milioni 37.9.

Naibu Mkuu wa Takukuru Temeke, Ramadhani Ndwatah, alisema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akitoa taarifa ya mwezi Julai, mwaka huu.

Alisema Sh. milioni 37.9 walizoziokoa katika miradi ya maji iliyopo Somangila Kigamboni, walibaini mkandarasi wa mradi huo alilipwa fedha mara mbili hivyo kumtaka areje fedha alizolipwa awamu ya pili.

Ndwatah alisema fedha hizo zimetokana na fedha za Mfuko wa Jimbo la Temeke ambazo zilitolewa, lakini hazikutumika, eneo la mishahara hewa na waliokoa kiasi cha milioni 6.7 na waliokoa fedha za chanjo ya surua ambazo hazikutumika.






## Uandikishaji wapigakura Dar, Dom waanza kwa kusuasua

**Na Waandishi Wetu**

MVUA zilizonyesha katika Jiji la Dar es Salaam jana zimesababisha wananchi wengi kushindwa kujitokeza kujiandikisha kwa ajili ya maandalizi ya uchaguzi wa serikali za mitaa katika maeneo mbalimbali katika jiji hilo.

Katika maeneo mengi vituo vilionekana kuwa wazi, huku wananchi wakijitokeza mmoja mmoja kwa kusuasua.

Katika vituo vya Kata ya Msimbazi kwenye mitaa ya Mtambani Idrisa na Mwinyi Mkuu, wananchi walikuwa wanajitokeza mmoja mmoja. Kadhalika katika Kata ya Magomeni katika mitaa ya Makuti A, Sunna, Dossi na Makuti B nako wananchi walionekana kujitokeza kwa kusuasua.

Akizungumza na Nipashe, Mjumbe wa Baraza la Usuluhishi katika Kata ya Magomeni, Habiba Mondoma alisema, wanaamini baada ya mvua kumalizika wananchi wengi watajitokeza kujiandikisha.

"Kwa kweli mpaka sasa, wananchi wanaojitokeza kujiandikisha ni mmoja mmoja, tunaamini kwamba imesababishwa na mvua hizi zinazoendelea kunyesha, kwa sababu hata sisi wenyewe tuliokuja kujiandikisha tumekubali kukanyaga haya maji," alisema Mondoma.

Katika mitaa 16 iliyoko Kata ya Buyuni hali haikuwa mbaya sana kama ilivyo katika maeneo mengine. Mwenyekiti wa Mtaa wa Kigezi Juu uliopo katika kata hiyo ya Buyuni, Saleh Salehe, alisema vituo vilifunguliwa mapema saa mbili asubuhi na watu walikuwa wamejitokeza kiasi.

Katika kata hiyo, baadhi ya vituo ambako uandikishwaji ulikuwa unafanyika ni katika Shule ya Msingi ya Kigenzi na mtaa wa Kigenzi wenyewe na ofisi ya serikali ya mtaa wa Buyuni.

Sehemu nyingine ambako wananchi walikuwa wanajiandikisha ni katika ofisi za mtaa wa Nyegulu na Shule ya Msingi ya Nyegulu, ofisi za mtaa wa Tuliani.

Sehemu nyingine ni katika ofisi ya mtaa wa Mgeule Juu, ofisi za serikali ya mtaa wa Zavalana, Shule ya Msingi ya Zavala.

Waziri wa Ofisi ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa(Tamisemi), Selemani Jafo, akizungumza katika Mji wa Nyamanyere mkoani Rukwa katika ziara ya Rais John Magufuli, alisema uandikishwaji huo unatarajia kumalizika OKtoba 14.

Aliwataka wananchi kujitokeza kwa wingi kwenda kujiandikisha ili wapate sifa ya kushiriki katika uchaguzi huo.

"Rais Magufuli amezindua uandikishwaji hapa Namanyere, naomba niwaombe wananchi wajitokeze kwenda kujiandikisha ili wapate sifa za kuchagua viongozi hao katika mitaa," alisema Jafo na kuongeza:

"Watu wasijione kwamba wana vitambulisho vya taifa ndiyo wakaona kwamba wana sifa ya kwenda kupiga kura hapana, ni lazima waende wakajiorodheshe katika vitabu vya mitaa yao, hapo ndipo watakuwa na sifa ya kupiga kura katika uchaguzi wa serikali za mitaa."

Huko Dodoma imeripotiwa pia kuwa uandikishaji wa daftari la wapiga kura kwa ajili ya uchaguzi huo katika jiji hilo, umeanza kwa kusuasua katika mitaa mbalimbali huku kukiwa na idadi ndogo ya vijana waliojitokeza.

Nipashe ilitembelea baadhi ya vituo vya kata ya Chang'ombe Chilewa A na B, Kishoka, pia vituo vya kata ya Makulu na viwandani na kukuta idadi ndogo ya wananchi kwenye vituo hivyo huku vingine hadi kufikia saa sita na nusu mchana vilikuwa na watu chini ya 100.

***Imeandaliwa na Paul Mabeja, Dodoma na Elizabeth Zaya, Dar***

**TANGAZO**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA / MASHAMBA

**NYUMBA INAUZWA** NYUMBA INAUZWA SINZA LION KUELEKEA KWA MWAIBULA NYUMA YA DEFRANCE HOTEL, BLOCK E PLOT No. 665, 288 SQM. MAWASILIANO: 0713 525954 / 0787 822000.

**VIWANJA/NYUMBA.** Hekari 25 zinauzwa Kisongo Arusha @Mil12. Heka 100 @Mil 8 Meserani Arusha. Nyumba inauzwa Kaloleni Arusha ina frame za biashara,nyenye SQ 59 mil 800. Nyumba inauzwa Usariver ya bedroom4 mil 70, hati ipo. Wasiliana na 0755 907 520.


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311


**JAMHURI YA MUUNGANO WA MUUNGANO WA TANZANIA**

**HATI YA KIAPO**

**Mimi ABDALLAH MZEE KHAMISS wa S.L.P 5252 TANGA, nikiwa Muislamu mtu mzima na nikiwa na akili zangu timamu ninathibitisha yafuatayo.**

1. Kwamba mimi ABDALLAH MZEE KHAMISS ndiye mwenye jina tajwa hapo juu.
2. Kwamba mimi **ABDALLAH MZEE KHAMISS** ni mtoto wa marehemu **MZEE KHAMISS MWINDADI** ambaye ni mmiliki wa nyumba **PLOT NO.5 BLOCK '154' NGAMIANI KUSINI STREET NO.20 Jiji la Tanga.**
3. Kwamba hati ya kumiliki (TITLE DEED) kwa bahati mbaya imepotea, nimefika Polisi kutoa taarifa na kupewa Loss Report **TAN/RB/344311/2019.**
4. Kwamba kwa kiapo hiki naiomba Ofisi ya Mipango Miji inipatie hati ya kumiliki nyingine kwa jina hilo la marehemu **MZEE KHAMISS MWINDADI**

**UTHIBITISHO;** Nathibitisha kwamba maelezo niliyoyaeleza hapo juu ni ya kweli kweli tupu kadri nijuavyo kwa sheria za viapo.

215452502

**KADI YA PIKIPIKI BAJAJ IMEPOTEA**

**SUDI HALUFANI MTORO** wa S.L.P 71439, DAR ES SALAAM anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki BAJAJ yenye usajili wa T337 AFU.

CHASSIS NAMBA. MD2DDDUZZPWG17 na ENGINE NAMBA. DUMBPG96798

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Taarifa Polisi.
**WMB/RB/2497/2019**

215452602

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M. 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
**Katika Mahakama ya mwanzo MJINI -TANGA**
**Usimamizi wa Mirathi NAMBA 131/2019**

Ombi la ZUBERI OMARI SEBU kuteuliwa Msimamizi wa mirathi marehemu SHALI OMARI SEBU

Kwa YEYOTE ANAYEHUSIKA TANZANIA BARA NA VISIWANI

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 28/10/2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 7/10/2019

215452702

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA KAGERA LILILOPO BUKOBA**

**MAOMBI NA: 188/2019**

**ANASTELA ISACK ................................ MDAI**

**DHIDI YA**

**AGNES RUBERT ........................... MDAIWA**

**KWA: AGNES RUBERT.**
**(POPOTE PALE MLIPO)**

Mnaarifiwa/ unaarifiwa kuwa Maombi Na: 188/2019 yamepangwa kutajwa tarehe 30.10.2019 mbele ya mwenyekiti wa baraza , R.Mtei saa 2:00 asubuhi.
Hivyo, unaamuriwa kuhudhuria wewe mwenyewe/ mwakilishi wako mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. Usipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja dhidi yako na hukumu kutolewa.
AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na MUHURI wa baraza hili leo tarehe 25.09.2019.

215453302

**KUPOTEA KWA KADI YA TRECTA**

Ndugu, **BUSUNGE M LUPEMBA** anatangaza kupotelewa na kadi Ya Trecta yenye namba za usajili **T 784 AZV.** kwa atakae iona atoe Taarifa kituo chochote cha polisi kilichopo karibu kwa Kumb: **MWA/NY/RB/361958/2019.**

215453102

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**Mahakama ya mwanzo MAKOLE**
**wilaya ya DODOMA**
**MADAI NAMBARI**

**MDAI : CHIMA MAZENGO**
**DHIDI YA**

**MDAIWA: FELEX RICHARD**
**KWA FELEX RICHARD**

**Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba**

**MADAI YA TSH.1,400,000/=**

Hivyo unahitajika kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya Jumanne tarehe 22/10/2019 saa 2.00 asubuhi kwa kujibu madai hayo, na kwa kuwa siku hiyo ya kukatwa shauri hilo, ni lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

Angalia kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama ikithibitisha kama umepokea kuitwa shaurini hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa Amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 8/10/2019

115451902

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO. 44 OF 2019**

**In the matter of the Estate of the late MARTINI JOHN MZENA of Dodoma Municipality/City at Ntyuka**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY JOHN MARTINI MNYIKONDO**

**GENERAL CITATION**

**(RULE 75 OF PROBATE RULES GN. 369 OF 163)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filled on or before the …9… Day of …10….. 2019.

Dated at Dodoma this …18…. day of …9.. 2019.

115451802

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**

**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika mahakama ya mwanzo MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No; 181/2019**

**Ombi la RAJABU AMIRI Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu AZIZI AMIRI MUHUMBA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 08/10/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 11/09/2019.

115452402


**Uza,**

**Chenye Thamani**

**Kubwa Kwa Kutangaza**

**Nasi Kwa Bei Poa**

**Tupigie 0767 223311**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku

Tupigie
0767 223 311

Nipashe


**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# SYLVINHO ATIMULIWA KAZI YA UKOCHA LYON



**LYON,** Italia

KLABU ya Lyon imetangaza kumfukuza kocha wake, Sylvinho baada ya kuiongoza kushinda mchezo mmoja tu kati ya mechi tisa kwenye mashindano yote msimu huu.

Raia huyo wa Brazil msimu wake wa kwanza akiwa kocha wa klabu hiyo alianza kwa ushindi wa kuvutia wa 3-0 na 6-0 dhidi ya Monaco na Angers kwenye Ligi Kuu ya Ufaransa.

Hata hivyo, Lyon imeshindwa kushinda mchezo wa ligi, ushindi pekee ulikuwa ni wa 2-0 dhidi ya RB Leipzig ya Ujerumani kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Sylvinho alichukua mikoba ya kuinoa timu hiyo Mei mwaka huu.

Lyon imethibitisha kwamba, kocha msaidizi Gerald Baticle atakuwa kocha wa muda wa kikosi cha kwanza, ambacho kilifungwa bao 1-0 na wapinzani wao Saint-Etienne, Jumapili.

Mkurugenzi wa soka, Juninho Pernambucano, ambaye naye katika siku za hivi karibuni alikuwa amekalia kuti kavu, ataendelea na nafasi yake.

Rais wa klabu hiyo, Jean-Michel Aulas alinukuliwa na Gazeti la L'Equipe Jumatatu akisema: "Mara chache tumekuwa kwenye hali hii. Juninho atatakiwa kufikiri. Hatuko sehemu ambayo tunaitaka, hilo kwa uhakika kabisa."

# De Ligt anahitaji Shule ya Kitaliano – Koeman

**TURIN,** Italia

RONALD Koeman amesema Matthijs de Ligt anahitaji njia mpya ya kujifunza haraka jinsi ya kucheza kwenye safu ya ulinzi akiwa na Juventus.

Beki huyo wa kati alijiunga na mabingwa hao wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, Julai kwa ada ya awali ya euro milioni 75 baada ya kuwa na msimu wa kuvutia pale Ajax iliyotinga nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Alianza kwa wakati mgumu katika soka la Italia pindi Juve ikiibuka na ushindi wa mabao 4-3 dhidi ya Napoli, lakini ameonyesha kuimarika kwa upatina wake na Leonardo Bonucci katika wiki za hivi karibuni.

Koeman anafikiri kijana huyo mwenye umri wa miaka 20 bado anatakiwa kupata somo katika "Shule ya Italia" ya ulinzi, lakini kocha huyo wa timu ya Taifa ya Uholanzi, hana wasiwasi kwa sababu mchezaji huyo bado ni kijana mwenye umri mdogo na ana nafasi ya kuimarika zaidi.

"Mara zote nimekuwa nashauri namna ya kuzoea maisha kwenye timu mpya, kwenye nchi mpya na wachezaji wapya," alisema Koeman akiwaambia waandishi wa habari.

"Nafikiri anahitaji kuzoea njia ya mpya ya ulinzi, kwa sababu ni tofauti na namna alivyocheza wakati akiwa pale Ajax. Pengine hiyo ndio shule ya soka la Italia.

"Bonucci alisema hivyo hivyo: Anahitaji kuzoea namna ya ulinzi chini ya kocha Maurizio Sarri na ipo tofauti na ilivyokuwa inacheza chini ya kocha, Massimiliano Allegri.

"Nafikiri Matthijs anahitaji muda. Lakini tayari yupo vizuri kwenye umri wake. Bado atakuwa na nafasi nzuri ya kujifunza zaidi na atakuwa bora zaidi kwa siku zijazo."





# *Tabarez: Suarez bado ataichezea Uruguay*

**MONTEVIDEO,** Uruguay

KOCHA wa Uruguay, Oscar Tabarez, amesema ni mapema mno kudhani kwamba, muda wa Luis Suarez kwenye timu ya taifa umefikia mwisho.

Suarez, ambaye ameichezea Uruguay mechi 111, atazikosa mechi za kirafiki za kimataifa na kikosi hicho dhidi ya Peru Oktoba leo 11 na 15 kutokana na kuendelea kupatiwa matibabu pale Barcelona.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, alitajwa kwenye kikosi cha awali cha timu hiyo kitakachocheza mechi zake mjini Montevideo na Lima, na kuamua kubaki na mabingwa hao wa Hispania.

Alipoulizwa kuhusu Suarez, ambaye alifunga mabao manne katika mechi tatu alizoichezea Barca, kuhusu majaliwa yake ya baadaye ya kikosi hicho, Tabarez aliwaambia waandishi wa habari: "Ni mapema mno kulifikiria hilo.

"Naamini yeye ataendelea kuichezea timu ya Taifa ya Uruguay na si jambo lililofikia mwisho kwa sasa."

HABARI MICHEZO

# LLORIS HATACHEZA TENA 2019, ASEMA DESCHAMPS




**PARIS,** Ufaransa

HUGO Lloris atakosa nafasi ya kucheza kwa kipindi chote cha mwaka 2019 kilichobaki kutokana na kuumia kiwiko cha mkono, kwa mujibu wa kocha wa timu ya Taifa ya Ufaransa, Didier Deschamps.

Kipa huyo wa klabu ya Tottenham, aligeuka kiwiko cha mkono wakati timu yake ikichapwa mabao 3-0 na Brighton and Hove Albion kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya England, Jumamosi.

Spurs haijasema lolote kuhusu lini atapona, lakini Deschamps anamtarajia Lloris kuwa nje ya uwanja hadi mwaka mpya.

"Nimezungumza naye kuhusu kile kilichotokea," alisema Deschamps akiwaambia waandishi wa habari.

"Tulizungumza tena Jumatatu na alikuwa anafanyiwa vipimo zaidi kwa ajili ya majeraha yake.

"Ni vigumu kutoa tarehe kamili ya yeye kurudi uwanjani na hatujui lini atapona. Lakini hatakuwa dimbani kwa kipindi cha mwaka wote huu kilichobaki.

Lloris atakosa mechi za Ufaransa za kufuzu michuano ya Euro 2020 mwezi huu dhidi ya Iceland na Uturuki na pia anaweza kuzikosa mechi za Novemba dhidi ya Moldova na Albania.

## Klopp: Safari ubingwa EPL bado ndefu Liver



**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp hafikirii zaidi kuhusu uwezekano wa Liverpool kuendelea kushinda mechi zake huku akijua kwamba hadi sasa zimechezwa mechi nane tu za Ligi Kuu England.

'Wekundu' hao wameshinda mechi 17 mfululizo katika mashindano yote na sasa inaongoza msimamo wa Ligi Kuu ikiwa inaongoza kwa zaidi ya pointi nane dhidi ya Manchester City.

Lakini huku kukiwa bado kuna safari ndefu ya kwenda ili kushinda taji hilo kwa mara ya kwanza tangu mwaka 1990, Klopp kwa sasa anaangalia zaidi kila mechi inayokuja mbele yake.

Akizungumza na waandishi wa habari, Klopp alisema: "Tunaheshimu kazi ngumu tuliyofanya. Hadi sasa si mbaya, lakini kuna mechi 30 zinakuja.

"Tunachoangalia hapa ni kuhakikisha tunashinda kila mechi iliyopo mbele yetu na si kuzungumzia ubingwa, kwani safari bado ni ndefu kwetu.

"Tupo mchezoni, hivyo jambo la msingi ni kuangalia tunashinda namna gani mechi zetu zilizopo mbele yetu na si kufikiria kuhusu ubingwa.

## *Mancini sasa amsubiria Martinelli kikosi cha Italia*

**ROME,** Italia

ROBERTO Mancini anajiandaa kumsubiri Gabriel Martinelli wakati Italia ikitaka kupata huduma ya mshambuliaji huyo wa Arsenal kuichezea kwenye mechi za kimataifa kwa siku za usoni.

Martinelli mwenye umri wa miaka 18, alizaliwa Guarulhos nchini Brazil, lakini anahaki ya kuichezea timu ya Taifa ya Italia kupitia kwa baba yake ambaye ni Muitaliano.

Iliripotiwa Jumatatu kwamba, Shirikisho la Soka la Italia (FIGC), liliwasiliana na Martinelli ili kujaribu kumshawishi kuikataa Brazil ili awachezee Azzurri kwa siku zijazo.

Hata hivyo, Mancini amekubali kwamba, itachukua muda kwa mchakato huo kukamilika.

"Kwa kesi ya Martinelli, si rahisi," kocha huyo wa timu ya Taifa ya Italia alisema akiwaambia waandishi wa habari Jumatatu. "Unatakiwa kutuma maombi na inaweza kuchukua muda mrefu. Ni muda mrefu wa kusubiri kwa wachezaji hawa ambao wana hati mbili za kusafiria (uraia pacha).

Kwa sasa, Mancini hatarajii kufanya mabadiliko makubwa kwenye kikosi chake kabla ya michuano ya Euro 2020. Italia itafuzu kucheza michuano hiyo kama itaifunga Ugiriki Jumamosi, huku kama Armenia ikishindwa kuifunga Liechtenstein na tayari Mancini analijua hilo.

"Kundi hili bado halijaamuliwa, linaweza kuongezewa mchezaji au kupungua. Wachezaji wawili au watatu wanaweza kuingia au kutoka," alisema.

Hiyo inaweza kuwa habari mbaya kwa Mario Balotelli, ambaye aliachwa kwenye kikosi cha sasa na amecheza mechi mbili tu kwa Brescia msimu huu.

Hata hivyo, amebainisha kwamba, mchezaji huyo wa zamani wa Man City anaweza kurudi kwenye kikosi hicho na yupo kwenye mipango yake kama kiwango chake kitaimarika.



# DONDO OKA MAGAZET LAYA




# WENGER AMWONYA PEPE ATASOTEA NAMBA

Lazima niseme tunao wachezaji makinda wazuri ambao wanaweza kucheza pembeni, hivyo...

**LONDON,** England

KOCHA wa zamani wa Arsenal, Arsene Wenger amemwonya Nicolas Pepe kwamba sasa atapaswa kupigania namba katika timu hiyo kama kiwango chake hakitaimarika.

**Pepe, ambaye alijiunga na Arsenal akitokea Lille kwa ada iliyoripotiwa kuwa pauni milioni 72 kipindi cha majira ya joto, amekuwa akikosolewa kwa kuanza kivivu kuitumikia 'Gunners'.**

Mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 24, amecheka na nyavu mara moja tu kati ya mechi 10 alizoanza katika mashindano yote na amecheza kwa dakika zote 90 kwenye mechi nne tu kati ya hizo.

Na uwapo wa makinda wanaokuja juu kwa kasi kama Bukayo Saka na Gabriel Martinelli wamevutia katika safu ya ushambuliaji msimu huu, jambo ambalo linamfanya Wenger kuamini Pepe anaweza kuanza kuwa katika presha ya kupata nafasi ya kuanza kwenye kikosi hicho cha Unai Emery.

"Ninampenda mchezaji [Pepe] na ninadhani ulikuwa uamuzi mzuri wa [kumsajili]," Wenger aliiambia Omnisport. "Bado hajamaliza kuzoea vizuri, unapaswa kumpa muda kidogo. Kwa sasa anaonekana kidogo kutocheza kwa uhuru kama alivyokuwa akifanya akiwa Ufaransa. "Ninaona aina kidogo ya mchezo wake, haswa akiwa hana mpira, hilo halitokei kwa sasa. Kwa upande mwingine, lazima niseme tunao wachezaji makinda wazuri ambao wanaweza kucheza pembeni, [na] hilo atapaswa kupigania nafasi."

Arsenal imeshinda mechi tano kati ya sita zilizopita katika mashindano yote, na kipigo cha bao 1-0 ilichokitoa dhidi ya Bournemouth Jumapili, kimewapandisha hadi nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu baada ya kushuka dimbani mara nane.

Wenger yuko tayari kumuunga mkono mrithi wake, Emery kwani anajua vizuri mahitaji ya soka la kuvutia lililofanikiwa Kaskazini mwa London.

"Sipo hapa kuhukumu makocha. Mimi ni shabiki wa Klabu ya Soka ya Arsenal, hivyo ninamsapoti yeye tu," Wenger alisema. "Lakini anaweza kushinda mechi na anacheza aina ya mchezo ninaoupenda.

"Klabu kama Arsenal ina jukumu kubwa na moja ya majukumu hayo ni kucheza soka la kuvutia. Baada ya hilo, nadhani kitu muhimu zaidi ni kuisapoti timu na kushinda mechi."

Licha ya kuonyesha mwanzo mzuri wa msimu, Wenger hadhani Arsenal ipo katika nafasi ya kutoa changamoto kwa Liverpool ama Manchester City katika mbio za ubingwa.

"Kwa sasa huwezi kutazama zaidi katika nafasi kwa sababu tofauti ya pointi ni ndogo sana," alisema. "Unaweza kuwa wa saba; unashinda mechi unakuwa wa tatu.

"Sidhani [inaweza kutoa changamoto ya ubingwa] kwa wakati huu kwa nilichokiona. Liverpool ipo mbali sana mbele kwa yeyote yule. Manchester City inaonekana kuwa na uwezo wa kupigana dhidi ya Liverpool, lakini maadamu haupo mbali sana, unaweza kutumaini."

## ZISIKUPITE

### AHOFU MAN KUMTIMUA

OLE Gunnar Solskjaer anahofia kuwa kipigo kikubwa kwa Manchester United mchezo ujao nyumbani dhidi ya Liverpool unaweza kuhatarisha kibarua chake. ***(Mail)***

### CHELSEA YAMKWAZA PULISIC

MSHAMBULIAJI wa Chelsea na Marekani, Christian Pulisic, 21, amekiri kuchanganyiwa kwake kwa kutopata nafasi zaidi ya kucheza tangu alipojiunga na klabu hiyo kwa pauni milioni 58 akitokea Borussia Dortmund. ***(Guardian)***

### KANE AMULIKWA MAN UNITED

OLE Gunnar Solskjaer anahitaji pauni milioni 300 za kutumia dirisha la usajili lijalo kununua mshambuliaji kama wa Tottenham na England, Harry Kane, 26, amesema winga wa zamani wa Manchester United, Lee Sharpe. ***(Talksport)***

### POCHETTINO, LEVY KUTETA

KOCHA wa Tottenham, Mauricio Pochettino anajiandaa kuzungumza na mmiliki wa klabu hiyo, Daniel Levy kuhusu mipango ya usajili kuelekea dirisha la Januari, ikiwa ni pamoja na kutoa uamuzi wa mustakabali wa baadaye wa Kiungo wa Kimataifa wa England, Eric Dier, 25, na Mdenmark Christian Erisken, 27, ambaye anatakiwa na Real Madrid. ***(Star)***

### GUARDIOLA, SILVA WAPISHANA

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola na kiungo wa timu hiyo David Silva walitofautiana kufuatia klabu hiyo kuangukia kichapo kutoka kwa Wolves Jumapili iliyopita. ***(Mirror)***

### DEMBELE AIVUTIA NA EVERTON

EVERTON nayo inajipanga kumfuata straika anayewindwa na Manchester United katika dirisha la Januari, Moussa Dembele. Mfaransa huyo mwenye umri wa miaka 23, anaweza kugharimu pauni milioni 40 kumng'oa kutoka Lyon. ***(Star)***

### WAMCHOKA SOLSKJAER

IDADI kubwa ya wachezaji wa Manchester United wamepoteza matumaini na Ole Gunnar Solskjaer na inaaminika baadhi yao wameacha kumsikiliza. ***(Sun)***

### GABRIEL AWAZA BRAZIL, ITALIA

MSHAMBULIAJI wa Arsenal, Gabriel Martinelli, 18, anakabiliwa na wakati mgumu wa kuchagua timu ya taifa atakayoitumikia kati ya Brazil na Italia. Ni mzaliwa wa Brazil lakini baba yake ni Mtaliano, hivyo anaweza kuchagua nchi mojawapo. ***(Mirror)***

### HODGSON ATAKA STRAIKA

KOCHA Roy Hodgson amesema Crystal Palace lazima isajili mshambuliaji mpya katika dirisha la Januari kama wanataka kutoa changamoto ya kumaliza nafasi sita za juu kwenye msimamo wa Ligi Kuu England, wakati pia akiwinda mabeki wawili wa pembeni wakati dirisha litakapofunguliwa. ***(Standard)***

### JOACHIM ATISHA MAREKANI

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Aston Villa, Julian Joachim, 45, ameichezea kwa mafanikio mechi yake ya kwanza Bourne Town kufuatia kufunga mabao yote manne wakishinda 4-3 Jumamosi dhidi ya Raunds Town kwenye Ligi Daraja la Kwanza kwa nchi za Marekani. ***(Birmingham Mail)***

HABARI MICHEZO

## Miraji abebeshwa mikoba ya Okwi

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI mashabiki na wapenzi wa Simba wakiendelea kumuota Mganda Emmanuel Okwi, Kocha Mkuu wa mabingwa watetezi hao wa Ligi Kuu Bara, Mbelgiji Patrick Aussems, amesema mshambuliaji wake, Miraji Athuman maarufu kama Shevchenko ['Sheva'] sasa anaonekana kuwa Okwi mpya katika kikosi chake.

Sheva aliyejiunga na timu hiyo msimu huu akitokea Lipuli, ameanza na moto mkali na mara nyingi hunoga zaidi akitokea benchi.

Katika mechi nne za Ligi Kuu Bara alizocheza, Sheva amefunga mabao matatu kati ya 10 ambayo yamefungwa na timu hiyo hadi sasa na kuifanya kuvuna pointi zote hivyo kukaa kileleni mwa ligi hiyo. Mashabiki na wanachama wa Simba walikuwa na hofu ya kikosi hicho kukosa makali katika safu ya ushambuliaji baada ya Okwi kukataa kuongeza mkataba, lakini sasa taratibu wanaanza kumsahau kutokana na vitu adimu vya Sheva.

Aussems amesema: "Siwezi kuumia kuondoka kwa Okwi kwa kuwa kama mchezaji kuondoka kwenye timu ni jambo la kawaida, ukiangalia hivi sasa, Miraji ameweza kufanikiwa kwa kiasi fulani katika kuifanya Simba iwepo hapa ilipo sasa.

## Stars kuifuata Amavubi J'Mosi

**Na Somoe Ng'itu**

KIKOSI cha timu ya Taifa (Taifa Stars), kitaondoka nchini Jumamosi kuelekea Rwanda kwa ajili ya kucheza mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya wenyeji (Amavubi), inayotarajiwa kupigwa Oktoba 14, mwaka huu jijini Kigali.

Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja wa Taifa Stars, Danny Msangi, alisema maandalizi ya safari hiyo yako katika hatua za mwisho na wanawashukuru wenyeji wao Rwanda kwa kukubali kujipima nao.

Msangi alisema kikosi hicho kinatakiwa kuwa imara zaidi kuelekea mchezo wa marudiano kuwania kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN) dhidi ya Sudan, kwa sababu tayari wako nyuma kwa bao 1-0.

"Timu itaondoka Dar es Salaam Jumamosi, kila kitu kinakwenda vizuri, kiufundi naamini itakuwa ni kipimo sahihi kwetu na kwa wenyeji pia, hakuna mechi rahisi, kila timu inataka ushindi ili kujiweka katika nafasi nzuri kwenye viwango vya Fifa," alisema Msangi.

Taifa Stars inatarajia kutumia mchezo huo ili kujiandaa na mechi ya kuwania tiketi ya CHAN, dhidi ya Sudan itakayochezwa Oktoba 18, mwaka huu, kwenye Uwanja wa El Merreikh Omdurman.

Hata hivyo katika mchezo huo wa kirafiki, Stars itamkosa nahodha wake Mbwana Samatta ambaye ameomba ruhusa kwa Ndayiragije ili aweze kupona vema na baadaye kuja kuitumikia nchi kwenye michezo mingine.

# MAXIME ALIA GUNDU KUWAGUBIKA KAITABA

**Na Somoe Ng'itu**

KOCHA Mkuu wa Kagera Sugar, Mecky Maxime, amesema kwa sasa timu yake imekuwa na bahati mbaya kwenye uwanja wake wa nyumbani wa Kaitaba, hivyo anajipanga upya kusaka dawa ya ushindi.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Maxime, alisema tangu ameifunga Simba mechi ya msimu uliopita, Kagera Sugar haijapata ushindi ikiwa nyumbani.**

Maxime alisema wachezaji wake wanapambana na kucheza kwa bidii, lakini wanashindwa kufunga na hivyo kujikuta wanapoteza ushindi na kuacha wapinzani wao wakiondoka na pointi tatu.

"Yaani kwa sasa mambo ni magumu tukiwa nyumbani, tumefungwa mechi saba mfululizo, tangu tulipoifunga Simba mchezo wa msimu uliopita, hatujashinda, wakatufunga wengine na baada ya kutufunga hapa majuzi, tukafungwa tena na JKT Tanzania," alisema Maxime.

Aliongeza kuwa msimu huu ligi ni ngumu zaidi, hivyo wataendelea kurekebisha makosa na hatimaye kuvuna pointi na kujiweka mahali pazuri katika msimamo wa ligi.

"Siku hizi hakuna faida ya uwanja wa nyumbani, kuna matokeo mengi ya kushangaza, halafu mara nyingi timu inayocheza mpira mkubwa, huwa haipati matokeo, kikubwa makocha tunatakiwa kuendelea kuwaweka vizuri wachezaji ili wasitoke mchezoni, " alisema kocha huyo.

Kagera Sugar imecheza mechi nne na ina pointi tisa katika msimamo wa ligi hiyo unaoongozwa na mabingwa watetezi Simba wenye pointi 12.

Ligi Kuu Tanzania Bara kwa sasa imesimama kupisha kalenda ya kimataifa ya Fifa ambapo Timu ya Taifa (Taifa Stars) yenyewe imeingia kambini kujiandaa na mechi ya kirafiki dhidi ya Rwanda itakayochezwa Oktoba 14, mwaka huu jijini Kigali.

CHANJA MBUGA....



Mshambuliaji wa Yanga, Mrisho Ngasa (kushoto), akimtoka mchezaji wa Coastal Union ya Tanga, Ayoub Semtawa, katika mchezo wa Ligi Kuu Bara uliopigwa Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## *Azam hakuna kulala hadi kieleweke Simba*

**Na Mwandishi Wetu**

KIKOSI cha Azam FC kitaendelea na mazoezi yake bila kupumzika kwa ajili ya kujiweka imara kuwakabili Simba, katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa Oktoba 23, mwaka huu kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam, imeelezwa.

Ofisa Habari wa Azam FC, Jaffer Idd, alisema jana lengo la kutovunja kambi ni kutaka kuwaimarisha wachezaji wao kuelekea mchezo huo unaotarajiwa kuwa na ushindani kuanzia mwanzo hadi mwisho.

Iddi alisema wanataka kuingia katika mchezo huo kwa lengo moja la kupata ushindi na kujifuta machozi ya kupoteza pointi nne katika msimu uliopita dhidi ya mabingwa hao watetezi.

"Timu ilipewa mapumziko ya siku moja baada ya kumaliza mchezo dhidi ya Namungo, kwa sasa itaendelea na kambi mpaka tutakapocheza na Simba, tunasisitiza kila mechi kwetu ni muhimu na tunahitaji kuonyesha kwamba msimu huu tumeingia kivingine," aliongeza Idd.

Alisema wanahitaji kuvuna pointi nyingi msimu huu ili wakate tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa mwakani wenyewe na si kwa kusubiri "mbeleko".

"Tunaijua Simba na wao pia wanatujua, tunaamini tutapata matokeo mazuri tutakapokutana, matokeo ya msimu uliopita yameshakuwa historia, sasa tunaangalia mchezo uliopo mbele yetu," alisema kiongozi huyo.

Simba na Azam FC zote zimeshatolewa katika mashindano ya kimataifa na nguvu na akili zao zimeelekezwa kwenye Ligi Kuu Bara pamoja na michuano ya Kombe la Shirikisho Tanzania itakayoanza baadaye mwaka huu.

# Michezo

Jumatano Oktoba 9, 2019

Nipashe






Wenger amwonya Pepe Arsenal UKURASA 30





Wachezaji wa Simba wakiendelea na mazoezi jijini Dar es Salaam. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Simba yafuata dawa Azam kwa Warundi

## ●●● Yatangaza mechi tatu kali za kirafiki ikianza na Wakenya Taifa Jumamosi, huku...

**Na Somoe Ng'itu**

KOCHA Mkuu wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, Mbelgiji Patrick Aussems amesema lengo la kuomba timu yake icheze mechi za kirafiki ni kutaka kuwaongezea "kasi" na kuwaimarisha wachezaji ili wafanye vema katika mbio za kutetea taji hilo wanalolishikilia hususan mechi iliyopo mbele yao dhidi ya Azam FC.

**Simba inatarajia kucheza mechi ya kirafiki dhidi ya Bandari kutoka Kenya itakayochezwa keshokutwa, Jumamosi halafu Oktoba 14, mwaka huu itawafuata Mashujaa FC kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani Kigoma na baada ya siku mbili itakutana na Aigle Noir ya Burundi kwenye uwanja huo.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Aussems, alisema kuwa mechi hizo zitakuwa sehemu ya mazoezi na anatarajia kutumia wachezaji wote waliobakia baada ya wenzao kuitwa kwenye timu zao mbalimbali za taifa.

Aussems alisema anahitaji kuona wachezaji wake wanacheza mechi hizo katika kiwango bora kwa sababu wanajiandaa kukutana na Azam FC ambayo pia ina kikosi imara.

Mbelgiji huyo alisema kuwa mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara ni ngumu na hakuna klabu inayoingia uwanjani ikiwa imejiamini inaondoka na ushindi, mpaka pale dakika 90 zitakapomalizika.

"Ni ligi ngumu, ni ligi yenye ushindani, kila timu inaamini inaweza kupata ushindi na hakuna mchezaji anayekata tamaa, hii inatufanya tujipange na kuendelea kujiimarisha ili tuweze kutimiza malengo, naamini kwamba kila mechi ni sawa na fainali," alisema Aussems.

Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu, alisema wamekubali mwaliko wa kwenda Kigoma kwa sababu ya kuendelea kuwajenga wachezaji na vile vile kuwaweka karibu na wanachama na mashabiki wa klabu hiyo walioko mkoani humo.

"Tunajua Kigoma haina timu ya Ligi Kuu, lakini ina mashabiki wa Simba, hii ni zamu yao, wajiandae kutupokea, watapata nafasi ya kuwaona wachezaji wao kwa karibu," Aussems alisema.

Baada ya mechi hizo za kirafiki, Simba watarejea jijini Dar es Salaam kuwasubiri Azam FC kwa ajili ya kukutana katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa Oktoba 23, mwaka huu kwenye Uwanja wa Taifa jijini.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba iko kileleni ikiwa na pointi 12 baada ya kucheza mechi nne, wakati watani zao, Yanga ambao wameshuka dimbani mara tatu wana pointi nne kufuatia kupoteza mchezo mmoja, kushinda mmoja na sare mmoja.

# Zahera sasa awatamani Waarabu Caf

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI leo Yanga ikiwa katika uwezekano wa kuangukia kuvaana na Waarabu wa Misri, Pyramids ama wa Algeria, Paradou AC, Kocha Mkuu wa kikosi hicho, Mwinyi Zahera, amesema haihofii timu yoyote kwenye droo hiyo ya mechi za mchujo kuwania kushiriki hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Yanga imeangukia kucheza mechi ya mchujo baada ya kutolewa na Zesco ya Zambia kwenye mechi ya raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika, ambapo droo ya mechi hizo za mchujo zitachezeshwa jijini Cairo, Misri leo.

Mbali na timu hizo mbili za Uarabuni, pia Yanga inaweza kupangwa kukutana na ESAE ya Benin, DC Motema Pembe (DRC), FC San Pedro (Ivory Coast), Bandari (Kenya), Bidvest Wits (Afrika Kusini), TS Galaxy (Afrika Kusini), Proline (Uganda) ama Triangle United ya Zimbabwe.

Zahera alisema soka la Afrika limebadilika kwa sasa, kwani viwango vya wachezaji vinafanana hali inayompa matumaini ya kufanya vizuri katika mechi hiyo ya mchujo.

Alisema amejifunza mambo mengi kutokana na kutolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, na kwamba atarekebisha makosa waliyoyafanya ili yasijitokeze Kombe la Shirikisho.

"Soka la Afrika hivi sasa limebadilika kwa kiwango kikubwa, awali timu nyingi zilikuwa zinazihofia timu za Waarabu, lakini hivi sasa hawaziogopi kutokana na ubora wao kupungua. Hivyo tupo tayari kukutana na timu yoyote kutoka Uarabuni, na nina uhakika wa kupata matokeo mazuri nyumbani na ugenini," alisema Zahera.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002